# Nipashe

Jumatano Machi 20, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579870

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




## Aliyebambikwa kesi ya mauaji ageuziwa kibao

UKURASA 3



KIMATAIFA:

Uhamaji Afrika unafukuza wenye ubunifu, wagunduzi

Ukurasa 20

MAKALA:

Baada ya maelfu kufa baharini, Afrika yaanza kudhibiti uhamiaji

Ukurasa 14

MSIMAMO WA KUNDI LA G55 ULIVYOMSHANGAZA NYERERE

Ukurasa 18

siasa

JUMATANO MACHI 20, 2019 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

Kilichotokea kwa Lipumba, Seif hatima ya kilichoanza mwaka 2015

Na Beatrice Shayo

HATIMA ya Maalim Seif Sharif Hamad, sasa ni rasmi kuwa haiko ndani ya CUF bali amepewa makao mapya na chama cha ACT- Wazalendo kinachoongozwa na Zitto Kabwe.

Seif anachukua hatua hiyo baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kutangaza rasmi kuwa Profesa Ibrahimu Lipumba ndiye Mwenyekiti halali wa CUF na kumshinda Maalim aliyempeleka mahakamani kupinga kushika wadhifa huo.

Muda mfupi baada ya kutoka mahakamani juzi, ambako alishindwa katika shauri lake la uongozi wa kisiasa dhidi ya Prof. Lipumba, Maalim Seif, alitangaza rasmi kujiunga na ACT -Wazalendo.

Jana Maalim Seif, aliyeambatana na Kiongozi Mkuu Zitto Kabwe, katika makao makuu ya ACT-Wazalendo.

ENDELEA UK 16

Ukawa unavyozidi kutibuka baada ya Lowassa kuibwaga

Ukurasa 15

Sharif Hamad (kushoto) pamoja na Prof. Lipumba enzi za uongozi wa CUF.

UKURASA 13

# Maalim Seif atema nyongo

• **Ni** baada ya kupewa kadi Na. 1 ACT- Wazalendo, atoa ya moyoni kuhusu Lipumba, awataka wabunge CUF kusuka au kunyoa... *Endelea uk. 2*



Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Maalim Seif Sharif Hamad, akionyesha kadi namba moja ya Chama cha ACT - Wazalendo, baada ya kukabidhiwa rasmi na kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe (wa pili kushoto), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**ANNE MAKINDA AFICHUA ALIVYOTUKANWA MATUSI**

SPIKA mstaafu wa Bunge la Tanzania, Anne Makinda, amesimulia alivyotukanwa matusi ya kila aina alipokuwa...

UKURASA WA 3

**MENGI ASIMULIA ALIVYOAGANA NA MKURUGENZI MIPANGO IPP**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, amesimulia alivyoagana na aliyekuwa Mkurugenzi wa Mipango...


## Wadaiwa kufa kwa kunywa gongo

UKURASA 3

## Tanzania yamwaga misaada nchi zilizokumbwa maafa

UK.2


**MICHEZO** CHAMA AWATULIZA MASHABIKI SIMBA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Maalim Seif atema nyongo

**Na Waandishi Wetu**

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Maalim Seif Sharif Hamad, amepokewa rasmi ACT-Wazalendo na kueleza mambo mbalimbali yakiwamo yanayomhusu Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba.

Maalim Seif (75), juzi alitangaza kujivua uanachama wa CUF na kujiunga na Chama cha ACT-Wazalendo muda mfupi baada ya Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, kubariki uamuzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa wa kumtambua Prof. Lipumba kuwa Mwenyekiti wa CUF.

Mapokezi rasmi ya Maalim Seif yalifanyika jana kwenye ofisi za ACT-Wazalendo jijini Dar es Salaam yakishuhudiwa na mamia ya wafuasi wa Maalim Seif waliotangaza kujiengua CUF.

Katika mapokezi hayo, kulikuwa na burudani za ngoma huku bendera za ACT-Wazalendo zikipepea katika mtaa mzima maeneo ya Kijitonyama, ziliko ofisi za chama hicho kinachoongozwa na Zitto Kabwe.

Akizungumza baada ya Zitto kumkabidhi kadi namba moja iliyolipwa ada ya miaka 10, Maalim Seif alisema sasa ni mwanachama rasmi wa ACT-Wazalendo, akiahidi kukisaidia chama hicho kichanga kujijenga.

"Tena mmesema nichukue kadi namba moja, mama yangu weeeee," Maalim Seif alisema baada ya kupewa nafasi ya kuzungumza.

Kadi aliyopewa mwanasiasa huyo mzoefu, awali ilichukuliwa na aliyekuwa Mshauri wa ACT-Wazalendo, Albert Msando. Wakili huyo alijiuzulu uanachama wa chama hicho mwaka 2017.

Katika mkutano huo wa kumkaribisha rasmi ACT-Wazalendo, ambao wanachama wengine 21 wa CUF walichukua kadi za chama hicho kipya, Maalim Seif alisema kuanzia sasa hataki malumbano na hata kulisikia tena jina la Prof. Lipumba.

"Mambo ya Lipumba msinitajie kabisa. Sitaki kulumbana na Lipumba, Lipumba kwangu mimi mwisho," Maalim Seif alisema na kushangiliwa na wanachama wa ACT-Wazalendo waliohudhuria mkutano huo.

Alisema walipokuwa CUF, walijitahidi kujenga taasisi ndiyo maana wakati mwingine alikuwa akiondoka na kukaa nje ya nchi kwa miezi sita, lakini shughuli za chama zilikuwa zinaendelea.

"Aondoke Maalim Seif au afe, hapatakuwa na kitu kitakachoharibika," alisema.

"Nakiri tupo hapa katika kujenga taasisi ya ACT-Wazalendo, siyo kumtegemea mtu.

Tusisahau wananchi nao wana mapenzi yao, kama watu wana imani na Maalim Seif, kwa nini hawana imani na Dk. Ali Mohamed Shein?

"Tujiulize 'kwa nini Maalim Seif?' Jibu ni rahisi ni kwamba sijikwezi, ninatembelea watu vijijini, ninakula na kulala nao, ndiyo maana watu wakaniona ni mwenzao, hiyo ndiyo siri ya uongozi nendeni kwa wananchi."

**MALI ZA CUF**

Katika mkutano huo, Maalim Seif aliulizwa na waandishi wa habari kuhusu bendera za CUF

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (wa tano kulia) na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wakibabidhi misaada ya dawa na vyakula, jijini Dar es Salaam jana, ambavyo serikali ya Tanzania imetoa kwa nchi za Malawi, Msumbiji na Zimbabwe, ambazo zimekumbwa na maafa ya mafuriko kufuatia tufani kali iliyolikumba eneo hilo la kusini mwa Afrika. **PICHA: SULTANI KIPINGO**

## Makinda asimulia alivyotukanwa matusi

**Na Mary Geofrey**

SPIKA mstaafu wa Bunge la Tanzania, Anna Makinda, amesimulia alivyotukanwa matusi ya kila aina alipokuwa akiwania nafasi mbalimbali za uongozi na kwamba aliitwa dikteta alipochaguliwa kuwa Spika wa Bunge.

Makinda aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wanawake wafanyabiashara ndogo ndogo masokoni, wakati wa kuadhimisha siku ya wanawake katika hafla iliyoandaliwa na Taasisi ya Equality For Growth (EFG).

Alisema wanawake hawapaswi kukata tamaa wanapokutana na changamoto za matusi na vitisho wakati wa kuwania nafasi za uongozi au kutekeleza majukumu yao na badala yake wasonge mbele.

"Mimi wakati nagombea nafasi za uongozi nilitukanwa sana lakini sikujali nilisonga mbele. Nikiwa madarakani ilifika

INAENDELEA UK. 8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

19/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 23-03-2019 kampuni ya **GLOBAL LEADER ENTERPRISES (T) LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa.

1. Kutoka **AIRPORT** kuelekea **KINYEREZI kupitia TAZARA,** gari hizo zenye namba za usajili:

**T 569 DHR/ T 179 DBD**

2.Gari hilo linavipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | **22.0** |
| **Upana** | - | mita | **3.20** |
| **Kimo** | - | mita | **4.90** |

Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

15125002


# Tanzania yazisaidia nchi zilizokumbwa na kimbunga

**Na Mwandishi Maalum**

TANZANIA imetoa msaada wa dawa, chakula na vifaa vya kujihifadhi kwa Msumbiji, Malawi na Zimbabwe ili kuwasaidia waathirika wa kimbunga cha Idai kilichosababisha mafuriko yaliyozikumba nchi hizo wiki iliyopita.

Msaada huo ulikabidhiwa jana kwa mabalozi wa nchi hizo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Makabidhiano hayo yalifanyika kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, sehemu ya msaada huo kwenda nchi za Zimbabwe na Msumbiji ikisafirishwa jana kwa kutumia ndege za Jeshi la Ulinzi la Wananchi (JWTZ).

Akizungumza wakati wa kupakia msaada huo kwenye ndege ya jeshi hilo, Prof. Kabudi alisema Rais John Magufuli ameagiza kutolewa kwa msaada huo na kutoa salamu za pole kwa marais wa nchi zilizokumbwa na kimbunga hicho.

"Mheshimiwa Rais Magufuli baada ya kupata taarifa hizi na kuzungumza na marais wenzake wa Msumbiji, Malawi na Zimbabwe, Tanzania imeona ni vyema kutokana na undugu wetu, umoja wetu na ujirani wetu, tuweze kuwapelekea msaada angalau kidogo wa dawa na chakula na pia kuwapa pole kwa maafa haya makubwa yaliyowapata," Prof. Kabudi alisema.

Waziri huyo alisema malori saba yenye shehena ya tani 200 za mahindi, yalitarajiwa kuondoka Mbeya jana kwenda Malawi ambako taarifa zilieleza kuwa watu 122 wamepoteza maisha na zaidi ya 1,000 wamekosa mahali pa kuishi.

Alisema tani saba za mchele, dawa na vifaa vya kujihifadhi zitasafirishwa kutoka Dar es Salaam kwa kutumia ndege ya jeshi kwenda Msumbiji ambako taarifa zinasema watu 221 wamefariki dunia na tani nyingine saba za mchele, chakula na vifaa vya kujifadhi vitasafirishwa kutoka Dar es Salaam kwa ndege ya jeshi kwenda Zimbabwe ambako watu 98 wamefariki dunia.

Waziri Mwalimu alisema serikali imetoa tani 24 za dawa, kila nchi ikipatiwa tani nane zinazojumuisha dawa za kuzuia maambukizo ya magonjwa (antibiotics), dawa za

INAENDELEA UK. 26

## HABARI KITAIFA

# Aliyebambikwa kesi ageuziwa kibao

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi limesema linafanya uchunguzi dhidi ya mfanyabiashara Mussa Adam ambaye ilibainika lilimbambika kesi ya mauaji.

Limedai kuwa wakati linawachukulia hatua baadhi ya askari wake walioshiriki kumbambika kesi, uchunguzi wa awali dhidi ya mfanyabiashara huyo umebaini ni mkora.

Wiki iliyopita, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ilieleza kuwa baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi mkoani Tabora walimbambika kesi ya mauaji mfanyabiashara huyo.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Ahmed Msangi, alidai mfanyabiashara huyo ni mkora.



Alidai alishafungwa miaka 20 jela kwa kosa la kubaka, alishaiba mahali na kukimbia na pingu na tukio la mwisho lililomfanya atiwe mbaroni na polisi na kubambikwa kesi ya mauaji, ni la wizi wa simu ya mwanamke kwenye kituo cha mabasi ambako alipigwa hadi kuvuliwa shati.

Msangi alidai mfanyabiashara huyo ni mtuhumiwa kama wengine, hivyo Jeshi la Polisi linamchunguza na akibainika kutenda kosa, atafikishwa mahakamani.

“Kilichoibuka hapa ni kitendo cha baadhi ya askari kumbambika kesi ambayo nayo tunachunguza ili nao wachukuliwe hatua,” alisema.

Msangi (pichani) aliongeza: “Lakini huyu mtuhumiwa naye ukweli ni kwamba siyo mtu safi, ni msumbufu kwenye jamii, ameshafanya matukio kadhaa.

“Pamoja na ukora wake, polisi hawakutakiwa wafanye walichokifanya (kumbambika kesi ya mauaji). Walitaarifiwa kuwa kuna mtu amepigwa sana huko mtaani, walipofika walimkuta kweli akiwa katika hali mbaya, amepigwa hadi kavuliwa shati, kosa lilikuwa ni wizi wa simu ya mama mmoja, ambaye hata hivyo aliipata baada ya wananchi kumkamata mtuhumiwa.

“Bado ofisa wetu aliyetumwa kwenda Tabora kupeleleza tukio hili yuko huko anaendelea na kazi. Anapeleleza tukio la polisi waliodaiwa kumbambika kesi mtu huyu, lakini pia mtuhumiwa naye anachunguzwa kutokana na kosa au makosa yaliyomfikisha polisi, akibainika ameyatenda, atafikishwa mahakamani kama watu wengine.”

Wiki iliyopita, Msangi akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa taarifa za awali zimeonyesha mfanyabiashara huyo alionewa kubambikwa kesi ya mauaji na baadhi ya askari polisi.

Msangi alisema jeshi hilo lilipokea barua ya malalamiko kutoka kwa mfanyabiashara huyo ndipo Ofisi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ilimtuma ofisa wake mwenye cheo cha juu kwenda Tabora kufanya uchunguzi.

## Wafa kwa madai ya kunywa gongo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WATU wawili wamefariki dunia mkoani Ruvuma, baada ya kunywa pombe aina ya gongo ambayo inasadikiwa kuwa na sumu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa, alisema tukio hilo lilitokea Machi 16, mwaka huu, majira ya saa 3:00 usiku katika kijiji cha Meamtwaro.

Aliwataja waliokufa kuwa ni Rashidi Ally (45), ambaye alikuwa fundi mwashi mkazi wa kijiji cha Kitanda wilayani humo na mwanamke ambaye jina lake halikufahamika ambaye inadaiwa kuwa ndiye alikuwa mpishi wa pombe hiyo.

Marwa alisema siku ya tukio, watu hao walifariki dunia baada ya Rashidi kwenda katika kijiji cha Meamtwaro kwa ajili ya shughuli za ujenzi na baadaye kuanza kunywa pombe hiyo.

Kwa mujibu wa Kamanda Marwa, baada ya wawili hao kufariki dunia, mume wa mwanamke huyo ambaye jina lake halijafahamika, alishirikiana na wenzake kumzika bila kufuata taratibu zinazotakiwa.

Kamanda alisema baada ya kumaliza kumzika mke wake, mwanaume huyo alikimbia na kutokomea kusikojulikana na kwamba polisi ilifanya uchunguzi katika eneo la tukio na kukuta chupa tupu za juisi zilizotumika kuwekea pombe hiyo.

Alisema mwili wa Rashidi ulifikishwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru Machi 17, mwaka huu na kufanyiwa uchunguzi wa awali na kubaini kuwa chanzo cha kifo ni pombe kali bila kula chakula na si sumu kama ilivyodhaniwa awali.

Kamanda alisema hivi sasa wanafanya utaratibu wa kuomba kibali mahakamani ili kufukua mwili wa mwanamke huyo kwa uchunguzi zaidi.

Marwa alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka mume wa marehemu aliyekimbia na watu waliohusika kumzika mwanamke huyo ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa dhidi yao .

## Mengi asimulia alivyoagana na Mkurugenzi Mipango IPP

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, amesimulia alivyoagana na aliyekuwa Mkurugenzi wa Mipango wa IPP, Francis Zangira, aliyefariki Machi 9, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Katika ibada ya kuaga mwili wa Zangira iliyofanyika nyumbani kwake, Mbezi Tangi Bovu, jijini Dar es Salaam, Dk. Mengi alisema alikuwa sehemu ya maisha yake.

“Mengi yamezungumzwa juu ya Francis na mimi niseme machache kwa sababu alikuwa sehemu ya maisha yangu. Juu ya tabia yake nilishuhudia kwa vitendo. Niwape mfano mmoja, siku moja gari lake lilikuwa limeharibika, nikamwambia kwa nini asikodi gari, akakataa akasema ni gharama sana,” alisema Dk. Mengi na kuongeza:

“Francis tulikutana naye mara ya mwisho kabla ya kufariki dunia. Alikuja ofisini kwangu kuniambia kwamba anaomba kupumzika na nikamwambia utaondokaje IPP wakati wewe ni sehemu yake? Lakini yeye alisema amechoka sana anaomba kupumzika. Nilimwambia kwamba hawezi kustaafu hivi hivi kwa sababu alikuwa sehemu ya IPP na ina jasho lake.

“Basi mwanasheria akanipatia barua yake na mimi nikaiidhinisha na nikamwambia unaondoka lakini huwezi kuondoka hivi hivi. Naomba uondoke na ukapumzike lakini upatiwe mshahara na marupurupu yako yote.”

Dk. Mengi alisema baadhi ya vitu ambavyo alimwahidi Zangira kabla ya kufariki dunia ni pamoja na kumpatia usafiri, nyumba na hivyo alitoa maelekezo kuhakikisha mjane anapatiwa vyote pamoja na mshahara aliokuwa akipata mumewe kila mwezi katika maisha yake yote.

“Francis ametuacha wapweke na Mungu atamsaidia huko anakokwenda,” alisema Dk. Mengi.

Akisoma wasifu wa baba yake, mtoto wa marehemu, Lulu, alisema Zangira alikuwa tegemeo na msaada kwa watoto na familia nzima kwa ushauri na alijitahidi kuweka furaha.

“Nashukuru kwamba Mungu alinipa kibali. Tulikuwa naye siku zake za mwisho, nilikuwa naongea naye kila siku na nilikuwa nakutana naye kila wiki. Asiponipata au kumpata mtoto wake yeyote alikuwa anajitahidi kuhakikisha anampata. Alikuwa na ubinadamu, msheshi, mwenye busara, mtu wa watu na mwadilifu,” alisema.

“Hakuwa mtu ambaye alikuwa anajitahidi afahamike kwa alicho nacho. Alijulikana kwa kuweka furaha kwa sura za watu. Tumepoteza si tu baba bali rafiki na yeyote niliyeongea naye alisema hicho kiatu atavaa nani. Alikuwa kiungo katika familia, si kwa mali bali kwa busara, hata kwa marafiki zangu alikuwa kama baba yao,” aliongeza Lulu.

INAENDELEA UK. 8


Tanpack Tissues Limited

PAPER TO DISPOSE?

Recycle Paper, Reduce Pollution, Conserve Environment



Offering Secured Document Destruction & Recycling Solutions for Various Grades of Paper

Partner with us for Recycling
Contact us :

DAR ES SALAAM
Mr. Deep Parmar
82 Soldering road, Mikocheni B, Opp. Sayona
Tel (Gen): +255 22 2773901/3
(Mob): +255 712 424738

ARUSHA
Mr. Suresh Kalyani
Factory Area, Unga Road
Tel (Mob): +255 754 817400

WHITE STAR INVESTMENTS LTD
TRANSPORTER

MADEREVA WA MAGARI MAKUBWA WANAHITAJIKA HARAKA

SIFA: - Awe na uzoefu wa miaka mitano na zaidi.
Awe na uwezo wa kuendesha magari ya SEMI/PULLING
Awe na leseni pamoja na
Hati ya kusafiria (Passport)

Muhimu: Fika ofisini kwa usaili Kiluvia Madukani.

Mawasiliano: 0692 136160
0689 251512

Au email: whitestarmapambano@gmail.com

# Bunge lataka fedha za barabara kusini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeitaka serikali kupeleka fedha kwa mkandarasi anayejenga Barabara ya Mtwara-Newala-Masasi (Km 210), kipande cha Mtwara-Mnivata (Km 50) ili kuongeza kasi ya mradi huo.

Kamati hiyo imeeleza kutokuridhishwa na kasi ya mradi huo ambao mpaka sasa ujenzi wake umefikia asilimia 47 kutokana na mkandarasi kutolipwa fedha kwa wakati.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Selemani Kakoso, alibainisha changamoto hiyo jana wakati wa majumuisho ya ziara ya ukaguzi wa miundombinu mkoani Mtwara. Wajumbe wa kamati hiyo walitembelea na kukagua mradi huo unaotekelezwa na Mkandarasi Dott Services kwa Sh. bilioni 89.

"Kamati hatujaridhishwa na maendeleo ya mradi huu na sababu kubwa ya kucheleweshwa imesemwa hapa ni kuchelewa kwa malipo ya mradi huu, hali hii itachelewesha maendeleo katika mikoa hii, hivyo Wizara ya Ujenzi mjitahidi fedha zije ili mradi ukamilike na wananchi wapate maendeleo," Kakoso aliagiza.

Alisema kamati yake inaishauri serikali kuimarisha miundombinu ya barabara ili kuunganisha Mkoa wa Mtwara na mikoa jirani na kurahisisha usafirishaji wa korosho zinazolimwa mkoani humo.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Elias Kwandikwa, aliihakikishia kamati hiyo wizara itatenga fedha katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha kulipa madeni inayodaiwa na mkandarasi huyo.

Awali, akitoa taarifa ya mradi huo kwa kamati, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Barabara, John Ngowi, alisema mkandarasi huyo anatakiwa kumaliza mradi Agosti mwaka huu na ameshaweka tabaka la kwanza la lami kilomita 5 na la tabaka la pili kilomita nne.

Alisema mkandarasi amemaliza kazi ya ujenzi wa makalvati madogo 31, makalvati makubwa manne na kazi zinaendelea ili kuhakikisha anakamilisha mradi huo ndani ya kipindi cha mkataba.

Kamati hiyo pia ilitembelea na kukagua Uwanja cha Ndege Mtwara ambao uko katika hatua za awali za uboreshwaji wake. Serikali imeupandisha hadhi ya uwanja huo kutoka Daraja 3C hadi 4E.

Kakoso aliiagiza serikali kumsimamia na kuhakikisha kampuni ya M/S Beijing Construction Engineering Group inayojenga barabara hiyo kuongeza kasi ya ujenzi ili kukamilisha kwa wakati ukarabati wa uwanja huo unaotarajiwa kukamilika Septemba mwakani.

Kamati pia iliitaka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha inapata hati miliki ya viwanja vyote vya ndege nchini ili kuepusha migogoro na wananchi wanaovamia maeneo ya viwanja vya ndege.

Kamati hiyo iliipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kwa kutekeleza mradi wa upanuzi wa gati ya Mtwara na kuitaka ihakikishe mradi huo unasimamiwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu za utekelezaji wa mradi.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola (kushoto) na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu (katikati), wakimsikiliza Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, walipotembelea katika eneo la ujenzi wa makao makuu ya idara hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: WMNN**

# PM asema kilimo bado kina nafasi mageuzi ya kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema sekta ya kilimo ina nafasi kubwa ya kuleta mageuzi ya kiuchumi nchini iwapo changamoto zinazoikabili zikiwamo upatikanaji wa pembejeo, mbinu na miundombinu duni ya uzalishaji, usafirishaji, uchakataji wa mazao na masoko zitafanyiwa kazi kwa wakati.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akifungua ofisi za Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa Kanda ya Ziwa na kuutaka uongozi wa benki hiyo ushirikiane na wadau wengine kutatua changamoto hizo. Alisema bado sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zimeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi ambazo kwa kiasi kikubwa zimesababisha tija ndogo hususan kwa wakulima wadogo.

Kutokana na hali hiyo, aliwaagiza viongozi wa TADB kuendeleza kasi ya utoaji huduma ili kuwafikia wakulima na wafuaji wengi zaidi nchini.

"Endeleeni kufanya kazi na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuweka na kutekeleza mipango ya utatuzi wa changamoto zinazowakabili wakulima, wafugaji na wavuvi nchini. Pia panueni zaidi wigo wa huduma hususan utoaji wa mikopo katika kuendeleza miradi ya miundombinu ya kilimo, ufugaji na uvuvi na kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo kwa lengo la kuinua uzalishaji," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alisema kwa kuwa Benki Kuu ndiyo mdhibiti mkuu wa benki zote nchini, hivyo inao wajibu wa kutambua umuhimu wa kuandaa kanuni mbadala na sera za fedha ambazo ni rafiki kwa benki za maendeleo ya kilimo na ujasiriamali.

Alisema lengo ni kurahisisha utoaji wa huduma ya mikopo ya kibiashara tena yenye kuvutia kwenye sekta ya kilimo, hivyo akaitaka Benki Kuu iangalie namna ya kushirikiana na wadau hususan wa kilimo kuandaa kanuni maalumu za usimamizi angalifu wa fedha ambazo zitazingatia mazingira halisi ya kilimo na changamoto zake.

"Sambamba na kushughulikia sera au kanuni ambazo zinarahisisha kufanya biashara katika kilimo. Benki Kuu pia inatakiwa kuendesha kazi hiyo bila kuhatarisha utulivu wa kifedha na kujihami na madhara na hatari zinazoambatana na ukopeshaji," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bushungwa, alisema ufunguzi wa benki hiyo kwa Kanda ya Ziwa ni hatua nzuri ambayo inakwenda kuwasogezea huduma wakulima, hivyo ameutaka uongozi wa benki hiyo uandae utaratibu wakuwafundisha wakulima namna ya kuandika maandiko kwa ajili ya kuomba mikopo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema hadi Februari 28, mwaka huu benki ya TADB imekuza mtaji wake na kufikia Sh. bilioni 68 ikiwa ni ongezeko la asilimia 13 kutoka mtaji wa Sh. bilioni 60 uliotolewa na serikali mwaka 2015.

Mkurugenzi huyo alisema ukuaji wa mtaji wa benki hiyo umechangiwa na malimbikizo ya faida iliyotengenezwa katika kila mwaka wa fedha tangu kuanzishwa kwa benki hiyo mwaka 2015, kutokana na utoaji wa mikopo ya kimkakati inayotolewa kwa wateja wao.

# Bavicha yalipa somo Jeshi la Polisi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA), Wilaya ya Shinyanga Mjini, limelitaka Jeshi la Polisi kuacha kutumika kisiasa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu ujao.

Sambamba na kulipa somo jeshi hilo, Bavicha imelitaka kutekeleza majukumu yake ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

Kwa mujibu wa baraza hilo, kwenye uchaguzi uliopita ukiwamo uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na ule wa marudio katika kata na majimbo mbalimbali, jeshi hilo lilionekana kutumika kisiasa na hasa kwa kuonea vyama ya upinzani na kukibeba chama tawala (CCM) ili kipate ushindi kwa nguvu zote.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa Bavicha Wilaya ya Shinyanga Mjini, Samson Ng'wagi, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari juu ya hali ya kisiasa nchini pamoja na kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Tunaliomba Jeshi la Polisi lisitumike kisiasa na kukipendelea chama tawala bali lifanye kazi yake ya kulinda amani na lisiwe sehemu ya chanzo cha vurugu. Lituache sisi wanasiasa tushindane kwa hoja majukwaani," alisema Ng'wagi.

"Sisi Chadema huwa tunachukizwa sana pale tunapoliona jeshi letu ambalo ndiyo tunalitegemea kulinda usalama wa raia kuwa sehemu ya wanasiasa. Tunatoa wito kwao wasitubague watu wa upinzani ikiwa sisi sote ni Watanzania na wasimamie amani ya nchi iendelee kutawala hasa kwenye kipindi hiki cha uchaguzi," aliongeza.

Katika hatua nyingine, aliwashauri viongozi wa serikali wakiwamo wakuu wa wilaya, kufuata maagizo ya ugawaji wa vitambulisho vya machinga kwa kutolewa kwa wale wafanyabiashara wenye mitaji ya Sh. milioni nne na si kuanza kuonea wafanyabiashara wenye vipato vidogo na kuwadidimiza kiuchumi.

## HABARI KITAIFA

# Canada yapigia debe wanawake kiuchumi

**Na Enock Charles**

SERIKALI ya Canada imezitaka taasisi binafsi kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta muhimu za kiuchumi.

Akizungumza katika maadhimisho ya nane ya jukwaa la Canada na Tanzania katika uwajibikaji wa pamoja kwa jamii, Balozi wa Canada nchini, Pamela Donnell, alisema ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi unaongeza uzalishaji na usawa kwa maendeleo endelevu.

Balozi huyo alisema kampuni binafsi zitafaidika kwa kiwango kikubwa zikiongeza nafasi za ajira kwa wanawake na kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuwa takwimu zinaonyesha kampuni zenye kiwango kikubwa cha uwakilishi wa wanawake katika za uongozi, zilipata uzalishaji mkubwa kulinganishwa na zile zenye uwakilishi hafifu.

"Kampuni zenye kiwango kikubwa cha usawa wa kijinsia katika nguvu kazi yao na uongozi wa juu, huvuna faida nyingi," alisema.

Alisema serikali ya Canada imedhamiria kuweka mazingira mazuri ya kibiashara na kuhakikisha kampuni za nchi hiyo zinazofanya kazi katika mataifa mbalimbali, zinaheshimu haki za binadamu, sheria, miongozo, kanuni na viwango vya kitaifa vya kibiashara kwa ushirikiano wa serikali na jamii.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), John Mnali, alisema kituo hicho kinaelewa kuwa wanawake katika sekta binafsi hukutana na changamoto mbalimbali pamoja na upungufu wa mitaji, hivyo kusababaisha uzalishaji kidogo na usiokidhi mahitaji yao na ya familia.

Alisema Canada na Tanzania ni marafiki na zimeendelea kufanya kazi pamoja katika juhudi za kuvutia wawekezaji wa kimataifa wenye uwezo na viwango katika kufanikisha safari ya Tanzania ya viwanda na kwamba wanawake ni wazalishaji wakubwa wa familia na taifa.

"Tanzania na Canada wamekuwa marafiki wazuri na ninaelewa kuwa serikali ya Canada inaisaidia Tanzania katika kupunguza umaskini kwa kuzingatia mahitaji ya binadamu hasa wanawake na watoto," alisema Mnali.

"Wanawake ndio wazalishaji wakubwa katika familia nyingi. Wanawake wa Tanzania wanapaswa kupewa uwezo na usawa katika kutawala uchumi," aliongeza.

Naye Kiongozi wa timu ya mpango wa ukuaji wa kiuchumi kutoka Canada, Nathalie Garon, alisema Canada ni mshirika mzuri wa Afrika na hasa Tanzania kwa kuwa ina malengo yanayofanana katika kukuza uchumi kwa kuzingatia upatikanaji wa masoko, uwajibikaji wa kibiashara na maendeleo endelevu.

# Wawekezaji Syria wavutiwa kuwekeza Tanzania

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum ya Uwekezani nchini (EPZA), imesema wafanyabiashara na wawekezaji wanaoshiriki maonyesho ya kimataifa ya Syria wameonyesha kuvutiwa na fursa mbalimbali za uwekezaji nchini.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, Grace Lemunge, katika maonyesho ya kimataifa ya Syria yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

"Wawakilishi wa kampuni zinazoshiriki katika maonyesho ya kimataifa ya Syria waliotembelea banda la EPZA, wamevutiwa sana na fursa za uwekezaji hasa kwenye viwanda kupitia mamlaka ya EPZA," alisema.

Alisema lengo la EPZA kushiriki maonyesho haya ni kuwafungulia milango na kuwapa taarifa sahihi zihusuzo fursa za uwekezaji katika viwanda washiriki wa maonyesho hayo.

Lemunge alisema wafanyabiashara na wawekezaji wameahidi kupeleka taarifa hizo muhimu za fursa za uwekezaji zilizoko Tanzania katika nchi zao ili kuwashawishi wawekezaji wengi zaidi kuja nchini.

Alisema uwekezaji kupitia maeneo hayo ya ukanda maalum wa uwekezaji (SEZ), mwekezaji hupata fursa ya soko kubwa la ndani na nje, unafuu mkubwa katika kodi na wafanyakazi wa kutosha.

"Kupitia EPZA kuna fursa za kuwekeza kupitia kwenye maeneo ya ukanda maalum (SEZ). Asilimia 80 ya bidhaa zinazozalishwa huuzwa nje ya nchi na kiwango kilichobaki huuzwa nchini," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mwandamizi Uhamasishaji wa EPZA, Panduka Yonazi, alisema maonyesho kimataifa ya Syria yanayoendelea yamekuwa fursa muhimu kwa wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Syria na nchi zinigine za Asia kupata taarifa muhimu za uwekezaji katika viwanda nchini.

Alisema pia wafanyabiashara na wawekezaji wazawa nao pia wamekuwa mstari wa mbele katika kupata taarifa za fursa mbalimbali zinazotangazwa katika banda la mamlaka ya EPZA yanapofanyika maonyesho hayo.






Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi wa kuwataja waliolipwa fedha za korosho wa kupongezwa

**TANGU** kuanza kwa Operesheni Korosho kutokana na mkanganyiko juu ya bei ya zao hilo kati ya serikali na wafanyabiashara, kumekuwa na taarifa za kutatanisha kuhusu malipo ya wakulima kutoka serikali.

Baadhi ya taarifa zilikuwa zikieleza kuwa idadi kubwa ya wakulima ambao waliiuzia serikali korosho, waliripotiwa kuwa hawajalipwa fedha zao huku habari zaidi zikidai kuwa tani kadhaa zimekataliwa kutokana na kuwa na kiwango duni, hivyo wahusika kupata hasara.

Kwa kiasi kikubwa, lawama nyingi zimekuwa zikielekezwa kwa serikali kuwa imeshindwa kuwalipa wakulima kama ilivyokuwa imeahidi baada ya kuchukua jukumu la kununua korosho baada ya wafanyabiashara kugomea bei ya Sh. 3,300 kwa kilo moja.

Wakati habari hizo zikienea na kuonyesha kuwa uamuzi wa serikali ulikuwa wa kuwakandamiza wakulima, serikali kwa upande wake ilikuwa ikitoa takwimu mara kwa mara juu ya kiasi tani zilizonunuliwa na fedha ambazo wakulima wamelipwa.

Ili kukata mzizi wa fitina wa suala hilo, serikali kupitia Wizara ya Kilimo, imeagiza viongozi wa maeneo mbalimbali kubandika majina ya watu wote waliolipwa fedha za zao hilo pamoja na kiasi walichopata.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema juzi mbele ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyoko ziarani mkoani Mtwara kuwa uamuzi huo unatokana na taarifa alizoziita potofu kuwa baadhi ya wakulima hawajalipwa.

Hasunga alisema kumekuwa na mamalamiko kutoka sehemu mbalimbali katika maeneo yanayozalisha korosho kuwa wakulima hawajalipwa ilhali serikali imeshalipa kiasi kikubwa na inatarajia kumaliza hivi karibuni.

Ili kuhakikisha suala hilo linawekwa bayana, Waziri Hasunga alisema inawezekana wakulima hao wamekuwa wakidai kuwa hawajalipwa ili kukwepa kulipa madeni wanayodaiwa katika maeneo yao ya makazi. Alisisitiza kuwa timu ya Operesheni Korosho inapaswa kubandika majina ya wale wote waliolipwa fedha hizo ili kuweka ukweli bayana.

Pamoja na kuagiza hayo, Waziri aliweka bayana kuwa tangu kuanza kwa mchakato wa operesheni hiyo, serikali imeshawalipa wakulima Sh. bilioni 596.9 kati ya Sh. bilioni 722 zinazopaswa kulipwa kutokana na ununuzi wa korosho hizo.

Hatua hiyo ya serikali ya kutangaza majina ya wakulima waliolipwa fedha kutokana na kuiuzia korosho ni ya kupongezwa kwa sababu itaweka wazi upi ni mchele na zipi ni chuya ili kuondoa mkanganyiko unaoendelea sasa.

Kwa kufanya hivyo, serikali itajisafisha dhidi ya lawama zinazotolewa na baadhi ya watu kuonyesha kuwa imeshindwa kutekeleza azima yake, hivyo kuonekana ilichukua uamuzi wa kuwaumiza wananchi.

Hata hivyo, ni vyema hatua zaidi zikachukuliwa dhidi ya watu ambao wamekuwa wakieneza uvumi huo kuwa hawajalipwa fedha hizo ilhali wameshalipwa. Tunasema hivyo kwa sababu hatua hiyo ni ya uchonganishi na inachafua taswira ya serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wapinzani jitafakarini, migogoro hadi lini?

**HISTORIA** inaonyesha kuwa Chama cha Wananchi CUF kilianzishwa mwaka 1993 kutokana na muungano wa vyama vya Zanzibar United Front (ZUF) na Chama cha Wananchi Tanzania (CCWT) cha Tanzania Bara.

James Mapalala, alikuwa ni mwenyekiti wake wa kwanza na makamu mwenyekiti alikuwa ni Maalim Seif Sharif Hamad, huku Katibu Mkuu akiwa Shaaban Mloo ambaye sasa ni marehemu.

Miaka michache baadaye tangu kuanzishwa kwa chama hicho, Mapalala alifukuzwa ndani ya CUF baada ya kutofautiana na wenzake na kwenda kuanzisha Chama cha Haki na Ustawi (Chausta).

Wakati mwanasiasa huyo mkongwe anatimuliwa ilikuwa pia ni miaka michache tangu serikali kuruhusu Tanzania kuingia kwenye mfumo wa siasa za vyama vingi, ulioanza mwaka 1992.

Baada ya Mapalala kuondolewa, baadaye Profesa Ibrahim Lipumba, alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa chama hicho, CUF ikaendelea na shughuli za siasa na kuonyesha upinzani kwa vyama vingine.

Lakini miaka 22 baadaye CUF ikaingia tena kwenye mgogoro ulioanza mwaka 2016 baada ya Prof. Lipumba kutangaza kurudi katika nafasi hiyo alioiacha miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Ilikuwa ni takriban mwaka mmoja tangu alipojiuzulu nafasi ya uenyekiti na kuwa mwanachama wa kawaida, lakini aliporejea kukalia kiti hicho, alikutana na upinzani mkali, lakini Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ikatangaza kumtambua kama mwenyekiti halali wa chama ndipo mgogoro ukazuka.

Aliibua mgogoro kwa sababu aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Self Sharif Hamad, hakukubaliana na uamuzi huo, hali ambayo ilisababisha uhasama hadi kuwapo kwa CUF mbili ya Maalim na Prof. Lipumba.

Wafuasi wa CUF hizo mbili walikuwa na uhasama miongoni mwao, kila upande ukiona mwingine kama adui na walifikia kutishiana na hata kuumizana

Mgogoro huo uliodumu kwa zaidi ya miaka miwili, ulifikishwa mahakamani, ambapo Jumatatu juzi,ulihitimishwa na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kubariki uamuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa wa kumtambua Profesa Ibrahim Lipumba kuwa mwenyekiti wa chama hicho taifa.

Baada ya uamuzi huo wa Mahakama, Maalim aliamua kujitoa CUF kujiunga na chama cha ACT- Wazalendo ili kuendelea na harakati za kisiasa.

Amekaririwa na vyombo vya habari wakati akitangaza kuhama na kusema: "Shusha tanga pandisha tanga, safari inaendelea," huku akiwataka mashabiki wake wote kuungana naye katika chama cha ACT-Wazalendo.

Wakati Maalim akisema hayo, mashabiki wake kwa upande wa visiwa vya Zanzibar, nao walikaririwa na vyombo vya habari wakisema Prof. Lipumba amechukua chama siyo wanachama.

Kauli hiyo inaonyesha kwamba huenda kukawa na mpambano mkali wa kunyang'anyana wanachama kati ya vyama hivyo viwili na hatimaye kusababisha kimojawapo kuyumba.

Hii ni kwa sababu baada ya Maalim kutangaza uamuzi wa kuhamia chama cha ACT-Wazalendo, baadhi ya bendera za CUF zilishushwa katika ofisi mbalimbali za CUF nchini.

Miongoni mwa ofisi hizo ni za visiwani Zanzibar, ambako inaaminika kwamba ilikuwa ni ngome kuu ya CUF wakati huo chama kikiwa hakina mgogoro wa kiuongozi uliosababisha Maalim na Prof. Lipumba kutengana.

Prof. Lipumba amemudu kumuondoa Maalim Seif, je, ataweza mikikimikiki ya kisiasa akiwa na chama kilichogawanyika vipande viwili?

Ikumbukwe kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, kwa mara ya kwanza CUF ilipata wabunge wengi bara, huku mkoa wa Lindi ukiongoza na wabunge wanne ikiwa imegawana idadi sawa na CCM.

Wakati akiwa mwenyekiti wa kamati ya muda ya uongozi CUF, Julius Mtatiro, aliwahi kukiri kuwa chama hicho kilipata wabunge wengi kwa sababu ya kuwa ndani ya Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

Bila ushirikiano wa vyama vingine ataweza kuivusha CUF ikapata mafanikio kama ya mwaka 2015? Moja ya mambo muhimu ambayo wanasiasa wanapaswa kukumbuka ni kwamba umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Maalim ni 'muumini' wa Ukawa na ametangaza kushirikiana na umoja huo ili kuendeleza harakati za kisiasa, lakini hasimu wake, Prof. Lipumba tangu mwanzo hakuonekana kuukubali umoja huo.

Lengo la chama cha siasa ni kushika dola, lakini pia ni muhimu kwanza kishike mioyo ya wananchi wengi ambao ndio watakipigia kura na kukipa ushindi na kukiingiza madarakani kupitia sanduku la kura.

Pengine ni vyema vyama vya siasa hasa vya upinzani kujitathmini iwapo migogoro inaweza kuvifikisha kwenye hatua ya kushika dola kama si kuvisambaratisha.

# BARUA & MJADALA

## Wanaofunga minyororo wanatuonea madereva

***Mhariri***

*POLE na majukumu ya kikazi pia naomba unichapishie barua hii ili viongozi wa wakala wa barabara vijijini (Tarura) Dodoma wajue uonevu tunaofanyiwa na vijana wao wanaohusika na kufunga minyororo magari.*

*Ilikuwa Februari 15, 2019, niliwapeleka viongozi wa Kanisa Anglikana Tanzania kuonana na Makamu wa Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Baba Askofu Chilonga.*

*Ambaye ofisi yake ipo katika jengo la Mackay House ambalo ni jengo la kanisa. Kwa kuwa sehemu zote zilijaa nilibaki ndani ya gari kusubiri gari itakayotoka niegeshe na nilikuwa nimeegesha pembeni karibu na ukuta wa jengo. Wenye jukumu la kufunga walipofika walianza kuifunga gari kibabe na hata nilipoomba samahani na kuwaeleza kwa gari ni la kanisa na jengo hili ni la kanisa pia na nimeleta viongozi hawakutaka kunisikiliza.*


*Kitendo hicho kilisababisha usumbufu mkubwa sana. Tulipowapigia simu waje tulipe watufungulie walikaa zaidi ya saa moja na nusu.*

*Ilibidi viongozi wakodi teksi kuwahi shughuli nyingine za ofisi.*

*Mahali hapo hakuna kibao kinachokataza dereva kuegesha gari, wakumbuke kuwa Dodoma ni jiji na ndiyo mji mkuu wa nchi magari ni mengi na sehemu za kuegesha ni chache.*

*Nawashauri pia sehemu zote ambazo haziruhusiwi wekeni vibao, kitendo cha kuviziana kama paka na panya hakifai na ni uonevu mkubwa kwa madereva.*

***Masaka K.G***
***Anglikana Makao Makuu***
***S.L.P. 899,***
***Dodoma.***




## 'Arumeru wanapochagua mwakilishi wa vikao vitatu'

**Na Salome Kitomari**

**HIVI** karibuni Spika wa Bunge, Job Ndugai, ametangaza kuwa Jimbo la Arumeru Mashariki (Chadema) lipo wazi kutokana na Mbunge Joshua Nassari, kutohudhuria vikao vitatu vya Bunge na kukiuka maelekezo ya katiba.

Katika taarifa hiyo Spika, anaijulisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa jimbo halina mbunge na kinachotakiwa ni kufuata sheria na taratibu za uchaguzi kumpata mwakilishi wa wananchi.

Kalenda inaonyesha kuwa imebaki miezi 19 ili kufikia uchaguzi mkuu mwakani ambao wananchi hutumia haki yao ya kikatiba kuchagua rais, wabunge na madiwani kwa upande wa Tanzania Bara wakati Zanzibar humchagua rais wa Zanzibar, wa Tanzania, wabunge, wawakilishi na masheha.

Tukirejea bungeni, vimebaki vikao vinne vya bunge kwa mwaka huu vikiwamo bunge la bajeti linaloanza mwezi ujao na kikao cha mwezi Novemba.

Kadhalika kwa mwakani, kimebaki kikao cha wiki tatu cha mwezi Februari na bunge la bajeti litakalokaa kuanzia Aprili hadi Juni na baada ya hapo ni uchaguzi na kufikiwa maamuzi ya wapigakura wa Zanzibar na Tanzania Bara.

Yapo mambo mawili yaliyonisukuma kuandika mjadala huu ambayo mosi ni sababu za mbunge huyo kukosa vikao vya kisheria kuwa alikuwa anamuuguza mke wake, jambo ambalo hakuna anayepinga.

Lakini, kilichozua mjadala ni alikuwa anamuuguzia mkewe wapi ndilo lilowafanya baadhi ya wapigakura kuanza kujiona kuwa hawakustahili na hajawatumikia kikamilifu kwa kadri ya matarajio yao.

**Kwa sasa wapigakura watamchagua mtu mwingine awawakilishe kwa kuwa ni utekelezaji wa sheria, lakini ni gharama kwa Mtanzania anayelipia uchaguzi ili Arumeru Mashariki imchague kiongozi wake.**

Wana Arumeru wanaona kwamba licha ya Tanzania kuwa na huduma zote muhimu za afya mwakilishi wao hazitumii. Wapigakura wake jimboni kwake ambao ndiyo waliomwajiri wanaamini kuwa kuna huduma za afya ambazo mbunge wao amewaaminisha wananchi kuwa ni bora na wanapaswa kuzitumia, lakini wanashangaa kuwa haziamini na amekimbilia Marekani.

Kinachowasukuma watu kuandika kwenye mitandao ya kijamii ni kwa kuwa wanaona kuwa waliomwajiri mbunge ambaye aliwaahidi kutekeleza ahadi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa zahanati na kuweka vifaa tiba kwenye hospitali hajafanya hivyo.

Tena amefukuzwa kazi na chombo ambacho alitakiwa kuwawakilisha wananchi, hivyo kuonyesha wazi kuwa hakuwahi kuziamini huduma za afya kwenye jimbo lake pamoja na taifa.

Kwa msingi huo ni vyema wabunge wakaishi kwa mfano kwamba huduma za afya kwenye maeneo yao na taifa zima ziboreshwe kiasi cha kuwawezesha Watanzania kuzitumia na siyo kuwa na huduma za afya kwa ajili yao na familia zao na zile za wananchi ambao ndiyo wenye wajibu wa kupiga kura wakiwa na matumaini makubwa ya kupata huduma bora.

Lingine lililonisukuma kuandika ni kuzungumzia gharama za uchaguzi katika jimbo hilo, kwa sasa fedha ambazo huenda zingeelekezwa kwenye shughuli za maendeleo kama ujenzi wa zahanati, kuongeza vifaa tiba na wataalamu kwenye hospitali zitalazimika kutumiwa kupata mbunge.

Lakini kwa kuwa ni utekelezaji wa sheria, zitakwenda kutumika kugharamia uchaguzi mdogo ili kupata mbunge atakayewawakilisha wananchi katika vikao vitatu pekee vilivyobakia kwa mwaka 2019 na 2020.

Kwa ujumla wanasema demokrasia ina gharama kubwa, lakini wakati mwingine ni vyema kuangalia gharama hizo. Leo hii Nassari ameshindwa kumtibu mkewe nchini kwa kuwa anazozijua mwenyewe, pengine mojawapo ni huduma za afya siyo bora, badala yake kumpeleka nje, fedha zitakazogharamia uchaguzi kwanini zisiboreshe huduma za afya?

Kama fedha hizo zingeelekezwa kwenye huduma za afya naamini kungekuwa na mabadiliko, kuliko zitumike ndani ya muda mfupi kumpata mtu atakayewakilisha ndani ya muda mfupi na huenda akatumia kipindi hicho kujifunza na kusubiri tena kuingia kwenye mchakato mwakani.

Hakuna ubishi kuwa katiba na sheria za uchaguzi zinataka kufanyika kwa uchaguzi mdogo, lakini ifike mahali gharama hizi ambazo anazibeba mwananchi wa kawaida kupitia kodi yake ziepukwe kwa kuangalia jimbo au kata husika iko wazi kwa muda gani uliobakia, ili kutumia kikamilifu pesa za wananchi.

Kwa sasa wapigakura watamchagua mtu mwingine awawakilishe kwa kuwa ni utekelezaji wa sheria, lakini ni gharama kwa Mtanzania anayelipia uchaguzi ili Arumeru Mashariki imchague kiongozi wake.

Gharama ni kubwa zikihusisha vitu vingi na si fedha pekee, bali gharama za muda kwa maana ya kwenda kupiga kura, kuhudhuria mikutano ya kampeni kwa kuwa wapo watakaoacha kazi na kushiriki kampeni hizo na kufuatilia matokeo.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed




**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Maalim Seif atema nyongo

INATOKA UK. 2

kushushwa kwenye majengo ya ofisi za chama hicho maeneo mbalimbali nchini na kusema kuwa huko kunaitwa "kushusha tanga na kupandisha tanga ili safari iendelee".

"Sisi rasilimali yetu ni wanachama wetu, CUF ni maskini sana, hakina fedha lakini kinatisha kwa sababu ya rasilimali watu," alisema.

Maalim Seif aliongeza: "Majengo karibu yote ya CUF si ya chama, wanachama wenyewe wamejitolea au kukodisha majengo yao au kukiazima chama. Sasa kama mwanachama huyo alikuwa CUF na anahamia ACT-Wazalendo, kwa nini aendelee kupeperusha bendera ya CUF?

"Kuna majengo matatu kwa Zanzibar na Bara ambayo yana majina ya CUF -- makao makuu Buguruni, ofisi ya Mtendeni na Kilimahewa ambayo hatujayagusa, tumechukua vitu vyetu mapema. Kama wanaamini chama hujengwa na bendera na majengo, wayachukue, sisi tunaamini chama ni watu."

Alimshukuru Zitto na uongozi wa ACT-Wazalendo kwa kuwapokea ili waongeze nguvu katika ujenzi wa chama hicho na demokrasia nchini.

"Hamkuwa najisi, mkasema milango ipo wazi tuje, tunajua haukuwa uamuzi wa viongozi pekee, bali pia wanachama, namshukuru Venance Msebo kwa kugomboa kadi namba moja ambaye amesema nipewe mimi na amelipa ada ya miaka 10," alisema.

### KUZUNGUKA UKAWA

Alisema wameingia kwenye chama hicho baada ya kuzunguka vyama vinne vinavyounganishwa na Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

"Tumekwenda Chadema, NLD na NCCR Mageuzi, lakini kwa sababu ACT-Wazalendo walishapeleka maombi kujiunga Ukawa, tumekichagua chama hiki ili roho zetu ziridhike. ACT-Wazalendo ni chama makini na kina misingi imara," alisema.

Maalim Seif alidai chama hicho kinafanya siasa na si propaganda na kwamba kimejipambanua ndiyo maana wameona hapo ndipo eneo la kwenda.

Alimsifia Zitto kwa kumwelezea kuwa ana ujasiri wa kipekee, hatoi matamko bila kufanya utafiti na akishaufanya, haogopi kusema hadharani na si kiongozi wa kujikomba kwa wakubwa.

"Ndugu zangu mjiepushe na jambo moja, mtachokozwa hasa kwenye mitandao ya kijamii. Msikubali kuchokozeka wala msijibizane nao, nguvu zao ni pale mnapowajibu. Uhalali wao ni majibizano, tutawale mitandao kwa fikra, wengi wenu mnawaza hayo ni maneno ya mtu mzima," alisema.

### HATIMA WABUNGE CUF

Alisema wabunge wa CUF wanaomuunga mkono wana uhuru wao wa kutafakari faida na hasara za kuhama kwa sasa pamoja na hasara na faida za kutohama chama kwa sasa.

Maalim Seif aliyewahi kushika nafasi za juu za uongozi serikalini, aliulizwa kama atawania tena urais katika Uchaguzi Mkuu mwakani, akasema wakati wa kuzungumzia suala hilo haujafika.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo (Zitto) alisema uamuzi wa Maalim Seif ni somo kwa viongozi wa vyama kuona umuhimu wa kujenga demokrasia na imani ya watu wanaowapa dhamana na wanakuwa tayari kufanya lolote ili wafike walikokubaliana.

Kuhusu kadi ya Maalim Seif, Zitto alisema: "Baadhi ya viongozi wetu waliochukua kadi za 'premier' (za hadhi ya juu) huko nyuma, walikumbwa na dhoruba. Jana (juzi) tulipokuwa tunazikusanya, kiongozi mmoja akasema zipo kadi ambazo zinatakiwa kukombolewa kutokana na viongozi wake kwa sasa kutokuwapo.

"Kadi ya Maalim Seif imekombolewa na mwanachama ambaye ni Mwenyekiti wa Mambo ya Nje, Venance Msebo," alisema.

Uamuzi wa Maalim Seif kujiunga na ACT-Wazalendo pia ulipongezwa na Mwenyekiti wa Chama cha Ukombozi wa Umma (Chauma), Hashimu Rungwe, aliyehudhuria mkutano huo.

Zitto aliwataja baadhi walioijiunga na chama chake na nafasi zao CUF ni Juma Duni Haji (Makamu Mwenyekiti wa CUF (mgombea Mwenza wa urais wa Ukawa 2015), Joran Bashange (Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara) na Nassor Mazrui (Naibu Mkuu wa CUF Zanzibar).

Wengine ni Abubakar Bakary (Jaji mstaafu na mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi), Hamad Hamad (Mjumbe Baraza Kuu la Uongozi Taifa), Kulthum Mchuchuli (Mkurugenzi wa Haki za Binadamu na Sheria) na Mbarala Maharagande (Naibu Mkurugenzi wa Habari na Uenezi).

Pia wamo Ismail Ladhu (Mkurugenzi wa Mambo ya Nje), Omari Shehe (Mkurugenzi wa Mpango na Uchaguzi), Mustafa Wandwi (Mkurugenzi wa Ulinzi na Usalama), Bonifasia Mapunda (mjumbe wa Baraza Kuu Taifa) na Najma Khalfan (mjumbe wa Baraza Kuu Taifa).

### KAULI YA LIPUMBA

Wakati Maalim Seif akichukua uamuzi huo, Mwenyekiti wa CUF, Prof. Lipumba, amewataka wabunge wa chama hicho kuungana na wanachama kukijenga chama.

Alidai kitendo cha Maalim Seif kutangaza kuhamia ACT-Wazalendo ni uharibifu wa chama chao na atakwenda kuharibu huko alikohamia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, alidai kuwa: "Ubinafsi wa Maalim Seif usitufarakanishe. Leo (jana) hii anahama, anakwenda ACT, anawaambia wabunge nao wamfuate.

"Kama alivyowatosa wawakilishi, anataka wao (wabunge) pia, kuonyesha tu ubabe kwamba hawezi kufanyakazi na Lipumba, wabunge msikubali, tuungane kukijenga chama."

Prof. Lipumba pia aliwaomba wanachama wa CUF hususani wa Zanzibar kuendelea kukiunga mkono chama hicho.

"Wito wangu ni kwa wanachama husunani Zanzibar, waendelee kutuunga mkono. Tumetoka mbali katika kudai haki ya nchi yetu, sisi ndiyo tulikuwa mstari wa mbele kudai haki ya katiba mpya, utawala bora na kupambana na rushwa. Wasikubali kushikiwa akili na Maalim Seif, wakaacha haki yao ya kudai haki."

### BOBALI AJIUNGA

Mbunge wa Mchinga, Hamidu Bobali (CUF), jana alitangaza katika mkutano huo wa Prof. Lipumba na waandishi wa habari kuwa, ameamua kuunga mkono juhudi za kukijenga chama hicho.

Bobali ambaye alikuwa miongoni mwa wabunge wa CUF wanaomuunga mkono Maalim Seif, alisema amekubaliana na uamuzi wa Mahakama Kuu, hivyo haoni sababu kuhama chama.

"Kimsingi, tulikubaliana uamuzi wa mahakama uheshimiwe. Tulikubaliana tunakwenda kutafuta haki na baada ya uamuzi tutakwenda kukijenga chama," alisema na kuongeza:

"Sikujua kama upande niliokuwa, ulikusudia ukishindwa, unahama chama, na kama ningejua, nisingekuwa sehemu ya mgogoro."

Mbunge huyo aliwaomba radhi wanachama wote wa CUF na kutoa wito kwa wabunge wenzake, madiwani na wenyeviti waungane kukijenga chama hicho.

"Huko kwingine wanakokimbilia hakuna mwelekeo, yamefanyika maamuzi ya hasira tu," Bobali alisema.

***Imeandaliwa na Beatrice Shayo na Romana Mallya**

# Makinda asimulia alivyotukanwa

INATOKA UK. 2

wakati nikaitwa dikteta," alisema Makinda.

Aliwataka wanawake wasijirudishe nyuma katika shughuli wanazofanya kwa kuhofia kusemwa vibaya au kutukanwa bali wasimamie kile wanachokiamini na kufikia malengo yao.

"Nilitukanwa sana hadi yale matusi nikiyakumbuka leo najiuliza hivi ni mimi au ni mtu mwingine? Lakini sikujali nilisonga mbele, hivyo na nyie msiangalie matusi mnayotukanwa leo bali msonge mbele tu," alisema.

Makinda aliwataka wanawake wajitokeze kwa wingi ukifika wakati wa kuwania nafasi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, uongozi kwenye masoko na kwenye makundi mbalimbali ili washiriki kikamilifu katika ngazi za uamuzi.

Makinda pia aliwataka wanawake hao wajasiriamali wachukue vitambulisho vya wafanyabiashara kwa sababu vitawawezesha kutambulika na kuwa na maeneo rasmi ya kufanyia biashara na kupata mikopo.

Pia aliwataka wanawake hao kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwa ajili ya kupata matibabu watakapougua na kwamba kutofanya hivyo ni kujiweka katika nafasi ya kurudi nyuma kimaendeleo.

"Siku hizi kuna magonjwa makubwa ambayo matibabu yake ni ghali kama huna bima ya afya, amini kuwa utakapougua wewe au mtoto wako, fedha ulizoweka akiba na mtaji wa biashara utaisha, hivyo kuwa na bima ni kuwa na uhakika wa maisha," alisema Makinda.

Aliwasihi wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kuchangamkia bima ya CHF iliyoboreshwa ambayo itaanza kutolewa kwa gharama nafuu kwa familia na mtu mmoja ili wapate huduma za matibabu wakati wowote.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa EFG, Jane Magigita, alisema kupitia mradi wa kuzuia na kupinga matusi kwa wanawake masokoni, wamefanikiwa kuwapa elimu ya kujitambua na kuwania nafasi za uongozi masokoni.

Alisema kampeni hiyo iliyokuwa na kauli mbiu inayosema 'Mpe Riziki si Matusi', imesaidia kupunguza matusi kwa wanawake kwenye masoko na kutambua haki zao wawapo kwenye majukumu ya kazi.

Kampeni hiyo ilizinduliwa jijini Dar es Salaam Februari 27, 2015 na aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Pindi Chana, na hadi sasa imewezesha kuwafikia wanawake katika masoko ya jiji hilo.

# Mengi asimulia alivyoagana na Mkurugenzi Mipango IPP

INATOKA UK. 3

"Kuna kaka mmoja anauza magazeti alikuwa ananisimulia kwamba siku ya mechi ya Simba dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo(DRC) angempitia waende kuangalia mechi, hivi ndivyo alivyokuwa baba yetu."

Mmoja wa Wakurugenzi wa IPP, Joyce Luhanga, alisema Zangira alikuwa mtu aliyekuwa na taaluma ya uchumi kama yeye kwa hiyo muda mwingi walikuwa wanashauriana mambo mengi na kwamba alifanya naye kazi kwa miaka 25.

"Alikuwa mtu wa karibu na kwa sababu alikuwa mchumi kama mimi. Siku za mwanzo tulikuwa tunafanya kazi zinazofanana na kila siku ya Mungu tulikuwa tunaonana ama kusalimiana au 'ku-consalt' kuhusu jambo fulani. Kwa hiyo tulikuwa 'tuna-share' vitu vingi na nashukuru Mungu kwamba alinipa nafasi ya kuwa na mtu wa karibu mwenye busara sana," alisema Luhanga.

Aliongeza kuwa: "Nimejifunza mengi kutoka kwake na nina uhakika watu wengi tulio nao ofisini wamejifunza mengi kutoka kwake. Alikuwa anaishi maisha ya kawaida sana. Mara nyingi alikuwa anapita na usimjue kama ni bosi pale ofisini na ilikuwa rahisi kumchanganya kama mtu wa kawaida, lakini 'that is humble he was' na alikuwa anajiweka nyuma wakati wote labda mpaka utambue kwamba yeye ni bosi."

"Kwa hiyo tumempoteza rafiki wa karibu sana na tutamkumbuka siku zote. Daima alikuwa mtu wa kucheka na kila mtu na najua marafiki zake wengi pale ofisini itawachukua muda mrefu kusahau kwa sababu alikuwa akiingia unatambua kwamba ameingia."

Alisema Zangira baada ya kuanza kuugua, aliwaambia kuhusu hali ya afya yake na aliomba kupumzika.

"Alivyoanza kuugua alikuwa 'anashare' kuhusu hali ya afya yake na akasema kwamba ameamua atapumzika kazi kwa sababu anaona afya yake inadorora. Tukashirikishana kwa hilo na kweli akaruhusiwa kupumzika na kabla haya hayajatimia ndiyo Mungu akamtwaa. Ni masikitiko makubwa kwetu familia ya IPP, tutamkumbuka na kumwombea siku zote," alisema Luhanga.

# Mfumo mpya usajili wapunguza milolongo

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MFUMO mpya wa usajili kwa njia ya mtandao unaofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni nchini (Brela) umeondoa usumbufu wa usajili uliokuwa ukifanywa kwa njia ya makabrasha.

Kutokana na mabadiliko hayo, imeelezwa kuwa kwa sasa namba ya usajili wa wakala huo ndio ambayo inatumika kama namba ya mlipakodi (TIN) kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Ofisa Milki Bunifu kutoka Brela, Suzana Senso, alisema hayo juzi, wakati akizungumza na wadau mbalimbali mkoani Morogoro waliokuwa wakielimishwa kuhusu utaratibu wa kusajili na huduma zingine zinazotolewa na Brela kwa njia ya mtandao ili kurahisisha zaidi upatikanaji wa huduma.

Senso alisema mfumo huo umepunguza mlolongo wa muda mrefu wa kupata huduma uliokuwapo kwa muda mrefu.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Fedha wa Brela, Bakari Mketo, alibainisha kuwa mwitikio wa wanaosajili kampuni kwa sasa umekuwa mkubwa kutoka watu 62 kwa mwezi, hadi 700 kwa mwezi.

"Toka mfumo huu mpya uanze kazi Januari 2, mwaka jana, tumesajili kampuni 4,700 kwa robo mwaka tu. Kati ya Oktoba na Desemba, mwaka jana, tulisajili kampuni 1,678.

"Lakini kabla ya mfumo hadi sasa, tumesajili kampuni 146,622. Ongezeko ni kubwa hasa katika maeneo ambayo tumeshapita na kufanya uhamasishaji," alisema Mketo.

Mketo aliwataka wafanyabiashara wasiogope mfumo huo badala yake wautumie kwa kuwa ni rafiki, una gharama nafuu na unaokoa muda mwingi uliokuwa ukitumika kwenye usajili.

**Toka mfumo huu mpya uanze kazi Januari 2, mwaka jana, tumesajili kampuni 4,700 kwa robo mwaka tu. Kati ya Oktoba na Desemba, mwaka jana, tulisajili kampuni 1,678.**

# Apigia debe ufugaji mbegu za chupa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, ameagiza halmashauri zote nchini kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa kutumia mbegu bora zinazozalishwa kituo cha Taifa cha Uhimilishaji Mifugo kwa Njia ya chupa (NAIC) kilichoko Arumeru, mkoani hapa.

Prof. Ole Gabriel alitoa agizo hilo jana katika ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kutokana na mwamko mdogo wa kutumia mbegu hizo.

Alisema ili kuendana na uchumi wa viwanda ni lazima wafugaji wabadilike na kutumia mbegu hizo ili kupata ng'ombe wenye nyama bora, maziwa, ngozi na kwato zitakazokidhi malighafi za viwanda.

Katibu Mkuu huyo alisema kwa kipindi cha mwaka jana, walitoa mafunzo kwa wafugaji 58,000 kwa nchi nzima hali iliyosababisha kuzalisha ndama 10,000 pekee licha ya kituo hicho kuzalisha mbegu 60,000 kwa wiki.

"Idadi ya wagufaji waliopewa elimu ni ndogo na mwitikio wa utumiaji mbegu hizi hauridhishi kwa wafugaji wetu. Kituo kinazalisha mbegu za kutosha kwa mahitaji ya wafugaji wote nchini, hivyo nawaagiza wataalamu wote watoke ofisini waende kwa wafugaji kutoa elimu juu ya utumiaji mbegu hizi," alisema.

Pia alitumia fursa hiyo kuwataka wafugaji kuondokana na dhana potofu kwamba kutumia mbegu hizo ni kuharibu vizazi vya mifugo jambo ambalo si sahihi.

Naye Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema hali ya usambazaji wa mbegu hizo kwenye vituo vilivyoko kanda saba nchini hauridhishi kutokana na baadhi ya wataalamu kutotimiza wajibu wao wa utoaji elimu kwa wafugaji.

"Serikali inauza mbegu hizi kwa ruzuku ili wafugaji wasiokuwa na uwezo wamudu gharama ya Sh. 5,000, lakini kuna baadhi ya wataalamu wananunua mbegu hizi na kuziuza kati ya Sh. 15,000 na Sh. 40,000," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Mjai, Mahmoud Mgimwa, alisema utumiaji wa mbegu hizo utawezesha wafugaji kufuga kwa tija na kupata soko la uhakika la bidhaa za mifugo yao.

"Kikubwa hapa wafugaji wabadilike kutoka kwenye ufugaji wa mazoea na kufuga kisasa kwa kutumia mbegu hizi, tushiriki uzalishaji wa malighafi za viwanda vyetu vinavyoanzishwa kwa wingi nchini," alisema.

**Serikali inauza mbegu hizi kwa ruzuku ili wafugaji wasiokuwa na uwezo wamudu gharama ya Sh. 5,000, lakini kuna baadhi ya wataalamu wananunua mbegu hizi na kuziuza kati ya Sh. 15,000 na Sh. 40,000.**



Mchuuzi Mohamed Issa akiwaandaa kaa kabla ya kuwakaanga katika soko la samaki la Feri, jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPIGA WETU**

# Wafugaji walia huduma majosho

**Na Dege Masoli,** KILINDI

SERIKALI imeshauriwa kuchukua hatua za haraka kutatua changamoto ya uhaba wa majosho wilayani Kilindi ambayo imeelezwa kuwa tishio kwa maisha ya mifugo.

Akizungumza kwenye sherehe za kimila za wafugaji wa jamii ya Kimasai, Mwenyekiti wa Wafugaji katika Kata ya Masagalu, Saitoti Leipoki, alisema uhaba wa majosho wilayani hapa unatishia magonjwa ya milipuko ya mifugo.

"Mifugo yetu iko hatarini hivyo huduma ya majosho ni muhimu sana, kuikosa ni hatari kwa kuwa ng'ombe, mbuzi na kondoo ni rahisi kupata magonjwa na kufa," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali kwa niaba ya wafugaji wenzake kuwa pamoja na mambo mengine suala hilo ni la msingi kwao na kwamba linapaswa kushughulikiwa na kupatiwa huduma ya majosho.

Naye Daniel Lekapoi aliomba kupatiwa huduma za afya kwenye Kijiji cha Kigunga ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Lekapoi alilalamika wanavyopata shida hususan wajawazito na watoto ambao mara nyingi wanapougua hutumia muda mwingi na fedha kusafiri na wakati mwingine hupoteza maisha.

Kwa upande wake, Katibu Tarafa wa Kwekivu, Mgaya Nyange, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Sauda Mtondoo, alieleza mpango wa serikali kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima ili kuondoa migogoro ya ardhi.

Nyange alisema sambamba na hilo uko mkakati wa hivi karibuni wa kujenga zahanati kwenye maeneo hayo yenye wafugaji ili kuwaondolea adha jamii hiyo kukosa huduma za afya.

# Muheza yadai bil. 1/- kodi

Na Munir Shemweta, MUHEZA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, inadai Sh. bilioni moja kutoka kwa wadaiwa 72 wa kodi ya ardhi katika wilaya hiyo, imefahamika.

Hayo yalibainika juzi baada ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, kufanya ziara ya kushtukiza katika masijala ya ardhi ya halmashauri hiyo.

Mabula alifanya ziara hiyo akiwa katika ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Mkuu wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri hiyo, Salehe Kamnge, alimweleza Naibu Waziri kuwa idara yake imeshawaandalia hati za madai wadaiwa hao na taratibu zinafanyika kwa wale waliokaidi kulipa ili wafikishwe katika baraza la ardhi la nyumba la wilaya.

**Halmashauri hiyo ilijiwekea makadirio ya chini ya makusanyo ya kodi ya ardhi katika kipindi cha mwaka 2018/19 wakati ikielewa ina madeni kutoka kwa wadaiwa wengi wasiolipa kodi.**

Kamnge alisema katika kuhakikisha zoezi la kuwafikisha katika baraza la ardhi na tayari wamewasiliana na Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Kaskazini ili kupatiwa mwanasheria atakayesimamia kesi hizo.

Mabula aliipongeza Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa kuvuka lengo la makusanyo ya kodi ya ardhi.

Kwa mujibu wa Kamnge, halmashauri hiyo hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi huu, imekusanya Sh. milioni 200 zaidi ya malengo yaliyowekwa.

Hata hivyo, Mabula alisema halmashauri hiyo ilijiwekea makadirio ya chini ya makusanyo ya kodi ya ardhi katika kipindi cha mwaka 2018/19 wakati ikielewa ina madeni kutoka kwa wadaiwa wengi wasiolipa kodi.

Aliitaka Idara ya Ardhi katika halmashauri hiyo kujipanga na kuhakikisha majalada ya ardhi yanatunzwa kwa kuzingatia taratibu zote za utunzaji majalada ili kuepuka hujuma.

Pia aliishauri idara hiyo kuwapeleka watumishi wa idara hiyo sehemu ya masijala ya ardhi kwenda ofisi ya Kamishna Msaidizi Kanda ya Kaskazini kwa ajili ya kujifunza ili kuongeza ufanisi kazini.



Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda, akisalimiana na baadhi ya wanawake wajasiriamali jijini Dar es Salaam jana, katika kuiadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani iliyoandaliwa na Shirika Lisilo la Kiserikali la Umoja wa Mataifa unao shughulikia usawa wa kijinsia (UN WOMEN), ambapo kauli mbiu yake ni "Badili fikra kufikia usawa wa kijinsia kwa maendeleo endelevu". **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mamia waacha shule kwa utoro

Na Steven William, MUHEZA

WANAFUNZI 201 wanaosoma shule mbalimbali za sekondari wilayani Muheza mkoani Tanga, wameacha masomo kwa sababu za utoro mwaka 2016.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo, alisema hayo juzi wakati akizungumza na walimu, wanafunzi na wazazi katika Tamasha la Kupinga Mimba za Utotoni lililofanyika katika Shule ya Sekondari ya Magila, lililoandaliwa na Mtandao wa Kupinga Mimba za Utotoni (Fema).

Tumbo alisema takwimu za mwaka 2016 zinaonyesha kwamba wanafunzi wanaosoma shule mbalimbali wilayani Muheza wamekatisha masomo kutokana na utoro uliokithiri katika wilaya hiyo.

Alisema kwa mwaka 2017, utoro uliongezeka na kufikia wanafunzi 332 wamebainika kuwa watoro, hivyo kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi kuwa watoro katika wilaya hiyo.

Tumbo alisema mwaka jana kutokana na serikali kufanya jitihada kupiga vita, utoro ulishuka na kufikia wanafunzi 220 kutoka wanafunzi 332 ambao walikuwa hawaendi shuleni.

Alisema kuhusu mimba kwa wanafunzi wasichana, walipata taarifa kutoka polisi kwamba wanafunzi 101 wamekatisha masomo kwa sababu ya ujauzito, kesi za dawa ya kulevya 67, matukio 84 ya ubakaji kwa watoto na kesi moja ya ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa wilaya alisema Shule ya Sekondari ya Shebomeza iliyoko Amani, iliongoza kwa wanafunzi wasichana kupewa ujauzito wilayani humo.

Alisema kutokana na hali hiyo anataka kusikia mwaka huu hakuna hata mimba moja katika shule ya sekondari, huku akiwataka walimu wa shule hizo kukiri kwamba ni marufuku katika shule zao wanafunzi wa kike kupata mimba.

Tumbo aliwapanga mstari walimu wa shule zote 26 za sekondari wilayani Muheza ili wakiri wenyewe kama mwaka huu wanafunzi hawatapata mimba na shule itakayobainika mwanafunzi amepata mimba itachukuliwa hatua kali.

Alisema katika Mkoa wa Tanga, kuna asilimia 29 katika mimba za utotoni na kwamba ni hali mbaya na sasa katika Wilaya ya Muheza, wamezindua kampeni ya ulinzi na elimu kwa mtoto wa Muheza.

"Kutokana na kampeni hii, ni wajibu wangu mtoto asome na mzazi ampe chakula," alisema.

Katika hatua nyingine, Tumbo alisema kuna viongozi wa ngazi ya juu, walimu na wanaume katika jamii wamekuwa na tabia ya kufanya mapenzi na wanafunzi wa kike na kuonya kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua, hatawajali cheo chake.

# Wauawa katika tukio la ujambazi

Na Liliani Lugakingira, BUKOBA

WATU watatu wanaosadikiwa kuwa majambazi wameuawa katika majibizano ya risasi na polisi, katika eneo la Kiraka Cheusi kijiji cha Nyamalagara, Biharamulo mkoani Kagera.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema juzi mbele ya waandishi wa habari kuwa watu hao waliuawa wakati polisi waliokuwa wakishikilia watuhumiwa wawili wakipelekwa kuonyeshwa walikoficha bunduki wanayoitumia kufanya uhalifu.

Kamanda Malimi alisema walipofika katika pori lililoko eneo la Kiraka Cheusi, ghafla polisi walianza kushambuliwa kwa risasi na wao kuanza kujibu mashambulizi.

Alisema katika majibizano hayo ya risasi, polisi waliwajeruhi watu watatu ambao walifariki dunia wakati wakipelekwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Biharamulo.

Kwa mujibu wa kamanda huyo watu wawili kati ya waliouawa, walitambuliwa kuwa ni Shaaban Mangote (40) mkazi wa Midaho Nyakahura wilayani Biharamulo na Eric Samson (19) mhamiaji haramu kutoka Burundi aliyekuwa akiishi Benaco wilayani Ngara.

"Tukio hili lilitokea Machi 16, mwaka huu, kutokana na Shaban ambaye ametafutwa na Jeshi la Polisi kwa muda mrefu bila mafanikio, baada ya kufanya uhalifu Oktoba mwaka jana ya kukimbilia kijiji cha Midao na baadaye kukamatwa," alisema Malimi.

Alisema baada ya mtu huyo kukamatwa, aliwaeleza polisi mtu anayeshirikiana naye kufanya uhalifu ambaye pia alikamatwa, wakati wakiwapeleka polisi kuwaonyesha walikoficha bunduki ndipo waliposhambuliwa na watu wasiojulikana.

"Tunaendelea na uchunguzi, maana tunaamini hawa walioshambulia polisi hawakuwa peke yao. Ninachotaka kuwaambia majambazi wanaoingia Kagera kufanya uhalifu wajue kwamba wataingia lakini hawatatoka salama," alisema.

Kamanda Malimi alisema katika eneo la tukio kulikutwa bunduki moja ya kivita aina ya AK47, risasi 25 za bunduki hiyo zilizokuwa katika magazini mbili na maganda matano ya risasi.

# Waratibu elimu wapewa mtihani mzito

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAOFISA Elimu Kata katika Halmashauri ya Arusha, wametakiwa kubuni mbinu mbadala za kusimamia shule zao ili kuboresha njia za ufundishaji za walimu kwa lengo la kupandisha taaluma na kuongeza kiwango cha ufaulu.

Hayo yalisemwa na Ofisa Elimu Msingi katika halmashauri hiyo, Hossen Mghewa, wakati akizungumza na maofisa elimu ngazi ya kata, katika kikao kazi kilichofanyika juzi.

Alisema kikao hicho, kililenga kukumbushana majukumu ya kazi, pamoja na kubadilishana uzoefu kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Aliwataka maofisa hao, kusimamia walimu katika maeneo yao ya kazi, kuhakikisha shughuli za ufundishaji zinafanyika kwa ufanisi pamoja na kuwasimamia walimu kufundisha kwa kutumia maarifa.

**Binafsi ninashukuru kuwapo kwa kikao hiki, licha ya kubadilishana uzoefu, kiutendaji tumekumbushana majukumu yetu ya kazi, naahidi kwenda kuyafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa kwa kushirikiana na walimu.**

Aidha, aliwataka walimu kubuni na kutengeneza zana ambazo watazitumia kufundishia kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika mazingira yanayozunguka shule zao, pia kutumia zana hizo kufundishia, kitendo ambacho kitasaidia kurahisisha tendo zima la ufundishaji kwa wanafunzi.

Alisema maofisa hao, wanatakiwa kukaa na walimu kwenye shule zao, kuweka mikakati thabiti ya kuwafundisha wanafunzi kwa kutumia zana rahisi na kuwajengea uwezo wanafunzi wa madarasa ya mitihani kwa kutumia mbinu sahihi ambazo zitawasaidia kujibu mitihani.

Alieleza endapo maofisa elimu kwa kushirikiana na walimu wakitumia mbinu hizo, watafuta alama D na F kwenye matokeo ya mitihani yao, huku akisisitiza jambo hilo linawezekana kama walimu watajituma na kufanya kazi zao kwa bidii na maarifa.

Licha ya kuzungumza hayo, aliwataka maofisa hao, kufanya ukaguzi mara kwa mara kwenye shule, ili kubaini na kutatua changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi katika shule hizo kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi kwa wakati.

"Msikae maofisini tu zungukeni kwenye shule zenu kukagua ufundishaji wa walimu katika maeneo yenu, kagueni kazi za walimu na wanafunzi, kagueni mahudhurio ya walimu na kuhakikisha ufundishaji unafuata misingi na taratibu, hii itawasaidia kubaini changamoto na kuzitatua kwa wakati," alisema.

Kwa upande wa walimu aliwataka kujiwekea utaratibu wa kujadiliana na kupeana uzoefu na mbinu bora za ufundishaji, jambo ambalo litawajengea uwezo walimu wenyewe na kuweka mazingira rafiki ya ufundishaji, kwa ajili ya kukuza ufahamu wa (KKK) tatu kwa wanafunzi kusoma, kuandika na kuhesabu.

Hata hivyo, alishauri kuwapo kwa daftari maalum kwa kila shule, daftari hilo litatumika kutunza kumbukumbu za utendaji kazi ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu pindi zinapohitajika.

"Ninashauri kuwapo kwa daftari maalum kwa kila shule, kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za utendaji kazi wa walimu, naamini taarifa hizo zitaongeza ari kwa walimu katika kufanya kazi kwa bidii na kuwabaini wale wote ambao wanafanya kazi kinyume na maadili," aliongeza.

Mwenyekiti wa Maofisa Elimu hao, kutoka Kata ya Oljoro, Furahini Godson, alisema kikao kazi hicho kimewajenga upya na aliahidi kutumia maarifa aliyopata kufundishia kwenye kituo chake cha kazi sambamba na kupokea maagizo yaliyotolewa kuyafanyia kazi.

"Binafsi ninashukuru kuwapo kwa kikao hiki, licha ya kubadilishana uzoefu, kiutendaji tumekumbushana majukumu yetu ya kazi, naahidi kwenda kuyafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa kwa kushirikiana na walimu katika shule zangu na wadau wengine wa elimu tutayafanyia kazi," alisema.

Kikao kazi hicho kiliwakutanisha maofisa elimu kutoka kata 27 za Halmashauri ya Arusha DC, wanaosimamia jumla ya shule 141 za msingi za halmashauri hiyo.

## Wajasiriamali wapewa mtego bidhaa za viwango

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MTANDAO wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (Mviwata), umewataka wajasiriamali kutengeneza bidhaa bora na zenye viwango ambazo zitauzwa bei nafuu ili kupata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.

Kadhalika wametakiwa kutumia nyenzo na maarifa mbalimbali wanayopata katika mafunzo ya usindikaji wa mazao ya vyakula na mifugo.

Mratibu wa Mviwata mkoani hapa, Richard Masandika, aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya usindikaji wa mazao ya vyakula na mifugo kwa washiriki 23 kutoka wilayani Karatu.

"Nawataka mtumie vizuri mafunzo haya mliyoyapata, msiishie njiani, tumieni weledi kutengeneza bidhaa bora zenye viwango ambazo zitapata masoko kwa urahisi ndani na nje ya nchi hii," alisema.

Mapema Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini, (SIDO), Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, aliwasisitiza wajasiriamali wote kuwa na vitambulisho vya ujasiriamali ambavyo vinatolewa nchi nzima katika kata husika ili warasimishwe rasmi katika biashara na bidhaa zao.

Aliwataka wajasiriamali wote nchini kuhakikisha wanaanzisha viwanda vidogo vidogo na wengine kuajiriwa katika viwanda hivyo lengo likiwa ni kujiongezea kipato na uchumi wa taifa kwa ujumla ikiwamo kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana.

"Nyie wajasiriamali, hakikisheni mafunzo haya mliyoyapata mnatengeneza na kusindika bidhaa zote mlizofundishwa, nawapongeza kwa jitihada mlizoonyesha kwa siku chache mlizokaa hapa mmejifunza zaidi ya kusindika bidhaa 20, hongereni sana, myafanyie kazi kwa vitendo," aliwasihi.



Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, Adam Kobelo, akizungumza baada ya Shirika la ECLAT Foundation kuahidi kutoa matofali ya ujenzi wa madarasa matatu ya Shule mpya ya Sekondari Songambele jana. **PICHA: GIFT THADEY**

## Taasisi yajitosa kuchangia elimu

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

MRUNDIKANO wa wanafunzi madarasani katika Sekondari ya Songambele iliyoko Mji Mdogo wa Mirerani, umeisukuma taasisi ya kijamii kuchangia matofali ya ujenzi wa madarasa matatu.

Jumla ya wanafunzi 200 wameanza kidato cha kwanza mwaka huu shuleni hapo hatua ambayo imeongeza mrundikano wa wanafunzi madarasani.

Mwenyekiti wa Shirika la ECLAT Foundation, Peter Toima, alitoa ahadi ya kuchangia matofali ya ujenzi wa madarasa matatu shuleni hapo.

Alitoa ahadi hiyo wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, kama ishara ya kuunga mkono juhudi za maendeleo.

Alisema katika madarasa hayo matatu pia watajenga na ofisi ya walimu ambayo itakuwa sambamba kwenye ujenzi huo unaotarajia kuanza wakati wowote.

Alisema huo ni mwanzo wa mwendelezo wa ECLAT kufanya maendeleo kwenye mji huo.

"Pamoja na hayo jamii inapaswa kuunga mkono jitihada hizi kwa kuchangia hata Sh. 2,000 au Sh. 1,000 kwa kila mmoja ili kuhakikisha shule hiyo inapiga hatua kubwa zaidi kwa kuwa na majengo mengi," alisema.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alisema wameamua kujenga shule hiyo baada ya watoto wa eneo hilo kutembelea kilomita 20 kila siku ili kufika shule ya jirani.

Alisema Shule ya Sekondari Mirerani Benjamin Mkapa ina wanafunzi wengi, hivyo wanafunzi wa eneo hilo wengine walikuwa wanasoma Shule ya Sekondari Naisinyai ambayo iko mbali na mji huo.

"Tunakushukuru mno kwa hili jambo kubwa ulilotufanyia kwa kuwa tumeanza vizuri na sisi tunakuahidi kukupa ushirikiano wa kutosha kwa lengo la maendeleo zaidi kupitia ECLAT," alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, (CCM), Wilaya ya Simanjiro, Awadhi Omary, alisema ECLAT Foundation inapaswa kupongezwa kwa hilo kwa kuwa hivi sasa jamii haiwezi kushikwa mashati tena kwa kutochangia elimu.



# Viongozi wa dini wapiga kambi kufanya maombi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIONGOZI wa dini 250 kutoka Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), wameamua kupiga kambi na kuendesha ibada maalum katika eneo la Makuru, Wilaya ya Hai, baada ya watu wachache kudaiwa kujipanga kuvamia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya chuo kikuu.

Uamuzi huo wa Wakuu wa Majimbo ya Hai, Siha, Kilimanjaro Kati, Kilimanjaro Mashariki, Karatu na wachungaji wa kanisa hilo, unatokana na madai ya kikundi cha watu wachache kudaiwa kutaka kuvamia eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stephano Moshi (SMMUCo).

Maombi hayo yaliyoongozwa jana na Mkuu wa KKKT nchini, Askofu Dk. Fedrick Shoo ambaye alifuatana na Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Erasto Kweka yalifanyika kwa wachungaji 250 kuzunguka ekari 50 kwa sala kukemea adui anayetaka kuvuruga uwekezaji wa chuo hicho.

**Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kutambua mchango wa kanisa na umuhimu wa elimu kwa maendeleo endelevu ya jamii yetu, walitupa hati miliki ya ile ardhi ambayo iko pale Makuru.**

Akizungumza kabla ya kuanza kwa maombi hayo, Askofu Dk. Shoo alisema tayari wameshapata fedha za ujenzi wa majengo matatu makubwa likiwamo jengo moja la ghorofa tano, ukumbi wa kuendesha mafunzo (malt purpose hall) na ghala la vifaa.

Eneo la Makuru linalodaiwa kuna kikundi cha watu wachache wanaojiandaa kuvamia ardhi, lilitolewa na Vyama vya Ushirika vya Nshara na Uduru kwa Dayosisi ya Kaskazini kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

"Nimesikia kuna maneno ya watu wachache au kikundi cha watu wachache ambao wanataka kuingia kwenye lile eneo, labda nichukue nafasi hii tu kuwaeleza wajue kwamba lile eneo limeshawekwa wakfu kwa ajili ya kazi ya Mungu, na mtu yeyote ambaye anaelewa nani mwamini wa dini yeyote, anaelewa kitu ambacho kimeshawekwa wakfu, huwa kimetengwa kwa kazi ya Mungu.

Juzi, Askofu Shoo ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, amewasihi waumini wa dhehebu hilo kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya Rais Dk. John Magufuli katika kudumisha na kuboresha elimu nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Shoo, baada ya eneo hilo kutengwa, kanisa liliweka wakfu kwa kujenga mnara wa msalaba na kisha kuweka jengo moja mahali ambapo hivi sasa wanataka kujenga ghala kubwa ambalo litatumika kuanza kukusanya vifaa na kwamba kazi ya ujenzi huo itaanza mara moja mwezi huu.

Zaidi ameeleza: "Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kutambua mchango wa kanisa na umuhimu wa elimu kwa maendeleo endelevu ya jamii yetu, walitupa hati miliki ya ile ardhi ambayo iko pale Makuru. Na pia napenda kuishukuru serikali yetu kwamba ilitupa kibali cha kubadilisha matumizi ya ardhi ile kutoka ardhi ya kilimo na kuifanya iwe kwa ajili ya makusudi ya elimu."



Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, akimkabidhi fundi Raphael Atanas, kazi ya ujenzi wa baadhi ya majengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stephano Moshi (SMMUCo), kinachojengwa Makuru, Machame mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wanufaika Tasaf wamkuna DC Warioba

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

IDADI ya wanufaika wa mpango wa uhaulishaji wa fedha kwa kaya maskini katika Manispaa ya Moshi ambao 'wamejiongeza' wenyewe na kuwekeza ruzuku hiyo kwa kufungua miradi midogo midogo ya kujikwamua kiuchumi imemkuna, Mkuu wa Wilaya hiyo Kippi Warioba.

Mpaka sasa walengwa zaidi ya 200 wameanzisha miradi ya ufugaji wa kuku, bata, mbuzi na na biashara ndogo ndogo, huku wengine 300 wakijiingiza kwenye kilimo.

"Mmeweza kunifurahisha ndugu zangu, haya ndio mambo yanayopaswa kufanywa ili kujiongezea kipato na kuondoka katika hali mliyokuwa nayo.

Zaidi alisema," Hatua hii itawawezesha kubadilisha maisha yenu na kuondoka kwenye mlo mmoja mliokuwa wakiupata na sasa kupata milo mitatu kwa siku."

Warioba alikwenda kuwatembelea baadhi ya wanufaika hao jana na kutoa elimu ya awali kabla ya kupewa fedha hizo.

Kutokana na hamasa hiyo, Mkuu huyo wa Wilaya amewataka wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini kutumia fedha wanazozipata kuanzisha miradi midogo midogo ambayo itawawezesha kujikwamua kiuchumi.

"Mchango mdogo wa Tasaf mnaoupata utumieni vizuri, msikate tamaa na kubweteka, endeleeni kuanzisha miradi midogo midogo ya maendeleo ili kuweza kujiinua kiuchumi, kwa kuwa tunategemea baada ya muda msimame wenyewe na kuendesha maisha yenu bila kutegemea msaada wowote," alisema Warioba.

Awali akitoa taarifa kuhusu mpango huo, Mratibu wa Tasaf katika Manispaa ya Moshi, Dennis Robert, alimweleza Warioba na ujumbe wake kuwa jumla ya fedha ambazo zimewafikia walengwa 1,461 wa mpango huo mpaka sasa ni Sh. bilioni 1.5 katika mizunguko 22.

# Marekani yajitosa kusaidia wakulima kahawa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MFUKO wa Maendeleo wa Marekani unaohudumia nchi za Afrika (USDF), umejitosa kuwatoa kimasomaso wakulima zaidi ya 800 wa kahawa katika eneo la Kinyamvuo, Wilaya ya Moshi, baada ya kukubali kugharamia pembejeo za kilimo na miche bora.

Habari zilizopatikana na kuthibitishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Kinyamvuo, Felix Mlay, zimeeleza kuwa pembejeo hizo zitatolewa kwa bei nafuu zaidi ili kukabiliana na walanguzi wa pembejeo.

Mlay alisema miche hiyo na pembejeo zimetolewa na Shirika la USDF ambalo lina lengo la kuboresha kilimo cha zao hilo na kufanikisha malengo ya serikali ya kuongeza uzalishaji.

Mlay alisema tayari wamepewa zaidi ya Sh. milioni 200 na shirika hilo kwa ajili ya kununua miche, kukarabati ofisi na ghala la kuhifadhia kahawa.

Fedha hizo pamoja na mambo mengine zitatumika kununua pembejeo ambazo watauziwa kwa bei nafuu kwa wakulima na kuwawezesha kulima kilimo bora cha kahawa na kuondokana na kilimo cha mazoea.

"Wakulima watapata pembejeo na zinaweza kutolewa kwa mkopo na baadaye mkulima akalipa kutokana na kahawa atakayouza, lakini pia miche mingi ya kahawa imezeeka, na tumepewa fedha kwa ajili ya kununua miche bora, hii ni fursa kubwa kwetu katika kuboresha kilimo hiki ambacho wengi walishakikatia tamaa," alisema Mlay.

Daudi Mariki ambaye ni mkulima wa kahawa katika kijiji hicho, aliwataka wakulima wenzake, kutumia fursa hiyo kuboresha kilimo cha kahawa, na kufanikiwa kujikwamua kiuchumia kupitia kilimo cha zao hilo.

"Tunaishukuru serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikiweka mikakati ya kuboresha zao hili na hata kutuletea wafadhili, ni vizuri sasa wakulima tukajituma katika kazi na kutumia wataalamu tulio nao kuboresha zao hili," alisema Mariki.

Ofisa Ugani wa Kijiji cha Mwika Kinyamvuo, Devotha Assenga, alisema wameendelea kutoa elimu kwa wakulima kubadilisha miti ya kahawa ya zamani na kupanda miche mipya inayotoka Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini TaCRI, ambayo haishambuliwi na magonjwa.

"Tumeshaandika barua TaCRI (Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania), kuomba miche ambayo haishambuliwi na magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani.

"Na mpaka sasa wana mpango wa kutuletea miche 1,500, na tunaendelea kuelimisha wakulima kubadilisha kahawa ya zamani ili kufanikiwa kulima kahawa bora na yenye tija."

Ukurasa 18



MSIMAMO WA KUNDI LA G55 ULIVYOMSHANGAZA NYERERE

**MAKALA:**

Baada ya maelfu kufa baharini, Afrika yaanza kudhibiti uhamiaji



Ukurasa 14

**KIMATAIFA:**



Uhamaji Afrika unafukuza wenye ubunifu, wagunduzi

Ukurasa 20


siasa

JUMATANO MACHI 20, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukawa unavyozidi kutibuka baada ya Lowassa kuibwaga

Ukurasa 15

# Kilichotokea kwa Lipumba, Seif hatima ya kilichoanza mwaka 2015

**Na Beatrice Shayo**

HATIMA ya Maalim Seif Sharif Hamad, sasa ni rasmi kuwa haiko ndani ya CUF bali amepewa makao mapya na chama cha ACT- Wazalendo kinachoongozwa na Zitto Kabwe.

Seif anachukua hatua hiyo baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kutangaza rasmi kuwa Profesa Ibrahimu Lipumba ndiye Mwenyekiti halali wa CUF na kumshinda Maalim aliyempeleka mahakamani kupinga kushika wadhifa huo.

Muda mfupi baada ya kutoka mahakamani juzi, ambako alishindwa katika shauri lake la uongozi wa kisiasa dhidi ya Prof. Lipumba, Maalim Seif, alitangaza rasmi kujiunga na ACT -Wazalendo.

Jana Maalim Seif, aliyeambatana na Kiongozi Mkuu Zitto Kabwe, katika makao makuu ya ACT-Wazalendo,

ENDELEA UK 16



Sharif Hamad (kushoto) pamoja na Prof. Lipumba enzi za uongozi wa CUF.

UCHAMBUZI

# Baada ya maelfu kufa baharini, Afrika yaanza kudhibiti uhamiaji

**Na Salome Kitomari**

KAULI mbiu ya mwaka huu katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika (AU), ni "wakimbizi, wahamiaji na watu wasio na makazi kuelekea ufumbuzi wa kudumu wanaolazimishwa kuyahama makazi yao."

Mkutano huo uliofanyika mwezi uliopita na kuwaleta pamoja wakuu wa nchi za Afrika, ulijadili kwa kina changamoto iliyopo na chanzo cha wahamiaji, wahamaji na wanaolazimishwa kuyakimbia makazi yao kwa sababu mbalimbali.

Ripoti ya hali ya uhamiaji barani Afrika na sera zilizopo inaeleza kuwa chanzo cha uhamiaji ni huduma duni za kijamii, migogoro ya kisiasa na ya kawaida ndani ya nchi husika na kwa baadhi ya jamii imekuwa ni mbinu ya kupata maisha mazuri.

Katika ripoti hiyo Kamishna wa Huduma za Kijamii wa AU, Amira Elfadil, anasema makundi ya vijana wamezikimbia nchi zao kwa kuamini kuwa wanapokwenda Ulaya na nchi nyingine zilizoendelea wana uwezekano mkubwa wa kufanikiwa kimaisha ikilinganishwa na kuendelea kuwapo nchini mwao.

Mwaka 2006 AU ilipitisha Sera ya Uhamiaji jijini Banjul, Gambia na miaka 10 baadaye ilifanyika tathmini ya utekelezaji wa sera hiyo, changamoto na fursa zilizopo na mwaka 2016 wakuu wa nchi waliridhia kuwa suala la wahamiaji ni mtambuka.

Kwa mwelekeo huo wakuu hao wa nchi walikuja na sera ya wahamiaji ya mwaka 2018 hadi 2030 ikiwa ni mwongozo wa kushughulikia changamoto na mafanikio ya kukabiliana na wahamaji, wahamiaji na wanaolazimishwa kuyaacha makazi yao.

Anasema sera mpya imebeba kipaumbele cha sera hiyo dhidi ya agenda ya 2063 ya Afrika Tunayoitaka 'the Africa We Want' na malengo ya maendeleo endelevu (GDGs), ili zisaidie nchi wanachama katika utekelezaji wa sera za wahamiaji kwa kuangalia vipaumbele na rasilimali zao.

Elfadil anasema sera hiyo imeangalia masuala ya utawala wa uhamiaji, elimu na kazi kwa wahamiaji, diaspora, usimamizi wa mipaka, uhamaji usiona utaratibu, wanaolazimishwa kuyahama makazi yao, wahamaji wa ndani na wahamiaji na biashara.

"Kuwa na sera ni jambo moja lakini utekelezaji wake ni kitu kingine, ni wito wetu kwa nchi wanachama wa AU kuiweka sera hii katika utekelezaji na hasa kwenye sera za ndani ya nchi katika kuangalia utawala wa wahamiaji na wahamaji," anasema.

Meneja wa Ukuaji wa Uchumi Mdogo Nchi za Afrika wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Abebe Shimeles, anasema ushirikiano wa nchi wanachama na usawa wa sera ya uhamiaji kwa ajili ya ajira zinaweza kusaidia kukuza ajira na masoko ya kazi ya ndani na nje.

Anasema maendeleo ya teknolojia huwafanya watu kutoka eneo moja kwenda jingine kwa ajili ya kutafuta ajira, na kutokana na ujuzi na maarifa waliyonayo wanaweza kupata kazi kwenye nchi nyingine.

Mtaalamu wa uhamiaji wa Umoja wa Afrika, Idara ya Huduma za Jamii, Peter Mudungwe, anasema kwa siku za hivi karibuni Afrika imeshuhudia mabadiliko ya pande za wahamaji huku kukiwa na ongezeko la vijana, usafirishaji wa binadamu na uhamiaji wa wageni.



Wakimbizi na wahamiaji kutoka sehemu mbalimbali za Afrika wakipambana kuokoa maisha yao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> "Nchi wanachama walisaini mkataba wa Kampala wa kulinda wahamaji na wahamiaji wandani kwamba ni jukumu la nchi husika kuwalinda na kuwatafutia makazi watu wake wanaohama kutoka eneo moja kwenda jingine,"



Anasema zipo familia nchini Ethiopia, ambazo hukusanya fedha kwa ajili ya kumsafirisha mwanafamilia mmoja kwenda kwenye nchi ambazo wanaamini zimepiga hatua kubwa kimaendeleo na anapofanikiwa kufika huko hutakiwa kuanza kuwavuta ndugu zake.

"Kinachofanyika ni kama kujitoa mhanga kwamba familia inajichangisha fedha za kuwezesha kijana wao kusafiri hadi Afrika Kusini au nchi nyingine na akifika huko atafute kazi ajikusanye ili kupata maisha mazuri na akifanikiwa kuanza kuvuta ndugu zake kwa njia aliyopitia au mbinu nyingine," anasema Mudungwe.

Anachambua sera hiyo akisema imelenga kuwezesha usalama, utaratibu na uhamaji wenye heshima, kufanya uragibishi kwenye ustawi wa huduma za kijamii na kiuchumi wa wahamiaji kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na sheria.

"Suala la uhamaji na uhamiaji kwa nchi zetu haukwepeki kutokana na ukweli kuwa zipo nchi ambazo bado zina migogoro ya wenyewe kwa wenyewe kutokana na uchaguzi, migogoro ya ardhi, umaskini na hali ngumu ya uchumi ambayo huwafanya watu kukimbia huku na kule kutafuta maisha na ndiyo maana kwa sasa nchi mbalimbali zinahifadhi wakimbizi," anasema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, mambo yanayoangaliwa ni usalama wa haki za wahamiaji na kushughulikia masuala ya uhamiaji, na ni muhimu kwa utawala bora wa wahamiaji ambazo zitapatikana kutoka na sera za nchi husika na mipango ya nchi husika.

Kuhusu biashara ya binadamu, sera hiyo imechambua kuwa wapo wanaolazimishwa kuwa watumwa kwenye nchi nyingine ambao huchukuliwa kwa kigezo cha kwenda kufanyakazi kwenye maeneo mengine, na sera imelenga kuwalinda na kuchukua hatua dhidi ya biashara hiyo.

"Sera inawataka nchi wanachama kuimarisha sheria zao za ndani na kuheshimu mikataba mbalimbali ya kimataifa kwa kutoa elimu ya utambuzi wa watu wake, ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi na kushirikiana na nchi nyingine katika kukabiliana na biashara ya binadamu," anasema.

Aidha, kuhusu wanaorudi na wanaotafuta makazi mapya, AU inasema ni vyema kukawa na ushirikiano baina ya nchi walizotoka na walizokwenda na isiingiliane kwa namna yoyote na uhuru wa kwenda eneo moja hadi jingine barani Afrika.

Anasema kundi jingine ni waliolazimishwa kuyahama makazi yao kwa sababu mbalimbali wakiwa ni wakimbizi na waliotafuta hifadhi na wasio na makazi wakati wakisubiri hali ya amani kurejea kwenye nchi zao.

Kuhusu wahamaji wa ndani, anasema ongezeko la watu katika eneo fulani linaweza kusababishwa na matukio ya ugaidi, migogoro, majanga ya asili na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yatahitaji jitihada mahususi.

"Nchi wanachama walisaini mkataba wa Kampala wa kulinda wahamaji na wahamiaji wandani kwamba ni jukumu la nchi husika kuwalinda na kuwatafutia makazi watu wake wanaohama kutoka eneo moja kwenda jingine," anasema.

Mudungwe anasema kimataifa kumekuwa na ongezeko la wahamiaji katika historia ya dunia, idadi ya wahamiaji ilifikia milioni 244 mwaka 2015 ikiwa na ongezeko la asilimia 41 toka mwaka 2000.

Aidha, wahamiaji kutoka Afrika wamefikia milioni 34 ikiwa nusu yake ni wanawake na sababu kubwa inayoelezwa ni ukosefu wa ajira na kazi zenye hadhi, umaskini, migogoro, kukosekana kwa usawa wa kujinsia na ukandamizaji, ugaidi pamoja na mabadiliko ya tabia nchi.

Anasema vifo vya wahamaji kwenye bahari ya Mediterranean vimefikia zaidi ya 5,000 waliopoteza maisha mwaka 2016 pekee, huku wanaofariki kupitia njia nyingine ikibaki kuwa kitendawili.

# Ukawa unavyozidi kutibuka baada ya Lowassa kuibwaga

**Na Enock Charles**



Aliyekuwa Mwenyekiti Mwenza wa Ukawa, Profesa Lipumba (kulia), akimkaribisha Edward Lowassa, upinzani baada ya kujiunga na Chadema. Wanaoshuhudia ni Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia (kushoto) na Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KURUDI CCM kwa aliyekuwa Waziri Mkuu mstaafu Edward Lowassa, pia mgombea wa urais wa vyama vya wanachama wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), akitokea Chama cha Chadema, kunafungua ukurasa mpya wa siasa za ushindani nchini na kuhitimisha minong'ono ya muda mrefu kuwa atakihama chama hicho kikuu cha upinzani.

Kuhamia kwa Lowassa upande wa pili kulipokelewa kwa msisimko mkubwa na shamrashamra nyingi na kulisababisha sintofahamu kuhusu nani angegombea urais kupitia Ukawa, ikizingatiwa kuwa kwa wakati huo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema Dk.Wilbroad Slaa alikuwa akitazamiwa kupeperusha bendera ya wapinzani.

Pia, aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, alikuwa miongoni mwa wanaotajwa kutaka kugombea urais kupitia Ukawa.

Hata hivyo, kwa mshangao wa wengi vigogo hao wawili waliwekwa kando na hatimaye Lowassa kupewa nafasi ya kupeperusha bendera ya umoja huo wa vyama wa upinzani.

Ujio wa Lowassa ulileta mpasuko mkubwa kwa vyama vya upinzani na kusababisha baadhi ya vigogo kubwaga manyanga, akiwamo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Slaa, kujiuzulu nafasi yake.

Aidha, alitangaza kuachana na siasa za vyama wa kile alichodai hawezi kumnadi Lowassa ambaye hapo kabla wapinzani walidai kuwa hafai kuongoza nchi.

Kadhalika, aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, ambaye hapo awali alihudhuria mapokezi ya kumkaribisha Lowassa Ukawa, naye alijiuzulu uenyekiti wake kwa madai kuwa nafsi yake inamsuta na kuwa hawezi kumpigia debe kuingia Ikulu kwa sababu zilizofanana na za Dk. Slaa, lakini Profesa Lipumba hakujivua uanachama wake.

Ikiwa ni takriban miaka minne imepita tangu Lowassa ajiunge upinzani na kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu, kurudi kwake CCM kunaacha maswali mengi juu ya uamuzi wake huo, hasa ikizingatiwa kuwa amefikia maamuzi hayo wakati ambapo mwenyekiti wake yupo rumande.

Akizungumzia kurudi kwa Lowassa katika chama chake cha zamani Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, amenukuliwa akimtakia heri na kuongeza kuwa Lowassa alikuwa ugenini na sasa amerudi nyumbani.

"Lowassa mwenyewe amesema amerudi nyumbani. Maana yake ni kwamba alikuwa ugenini tangu Julai 2015 hatukununuliwa kama tulivyowahi kutukanwa huko nyuma," Lissu alisema.

**UPINZANI SI BWERERE**

Ukichambua kwa makini kauli ya Lowasa ya kurudi nyumbani na ile ya Lissu ya kuwa Lowassa alikuwa ugenini tafsiri zaidi inayoweza kupatikana ni kwamba Lowassa mazingira ya upinzani yalikuwa ni mageni kwake na ambayo asingeweza kuyaishi kwa muda mrefu.

Maisha ya kiharakati kuchanganya kukamatwa kamatwa mara kadhaa na vyombo vya dola ni vitu vigeni ambavyo hakuwa akikutana navyo akiwa Chama Cha Mapinduzi akiwa kule hata baada ya kujiuzulu alipata ulinzi kama ilivyo kwa mawaziri wakuu wastaafu.

Aidha, alishiriki shughuli mbalimbali za kichama na kiserikali ambazo hazina bughudha wala kashkash kama ilivyo kwa upinzani kitu ambacho alionekana kuanza kukirudia akiwa upinzani mathalani, hivi karibuni wakati

> Hata aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chadema huko nyuma, Zitto Kabwe na baadaye kufukuzwa uanachama na hatimaye kupoteza ubunge wake kwa sasa ni mshirika mkubwa wa chama chake cha zamani katika mambo mbalimbali na hata kwa wana Umoja wa Katiba ya Wananchi –Ukawa.




aliposhiriki ufunguzi wa maktaba ya kisasa ya kielektroniki ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Katika majukumu hayo kikubwa zaidi kilichojitokeza ni kuanza kusifiwa na viongozi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi.

Akizungumza katika mkutano wa kumkaribisha nyumbani waziri mkuu huyo mstaafu alitaka asiulizwe maswali zaidi ya nini hasa kimemfanya arudi nyumbani na kusisitiza kuwa amerudi nyumbani na si kwa jirani.

"Nimerudi nyumbani wala si kwa jirani, msiniulize nimerudi kufanya nini," Lowassa anasisitiza.

Lowassa ametuacha na maswali ya nini sababu hasa ya kurudi nyumbani hasa ukizingatia malengo yaliyo mfanya kuhamia upinzani hayajatimia. Watu wanajiuliza amekerwa na nini kutoka upinzani au amevutiwa na nini hasa kutoka chama chake cha zamani ambako amekuwa akikilalamikia kwa uonevu mara kadhaa?

Uamuzi huu wa Lowassa na hasa ikizingatiwa kuwa ni mwanasiasa mkongwe unathibitisha maana ya siasa kuwa lengo lake kuu linaweza kuwa zaidi ya moja kwa wakati mmoja.

**WAPINZANI WAPARAGANYIKA**

Kile kilichowafanya wapinzani hasa Ukawa kutengana sasa hakipo tena. Matumaini ya kuendelea kuungana yanazidi kupotea. Kwani licha ya Lowassa kuondoka kilichotokea ni Lipumba kuachana na Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye sasa ni mwanachama wa ACT-Wazalendo, huu ni ufa mwingine mkubwa ndani ya Ukawa, unaoacha maswali mengi.

Licha ya Maalim Seif na CUF kuwa washirika wakuu wa Ukawa pamoja na Chadema, anatangaza kuwa amefanya uchunguzi kwenye vyama vingi vya siasa na akaona kinachomfaa ni ACT- Wazalendo ambacho si mdau wa Ukawa. Vipi waliokuwa wana Ukawa wenzake?

Dk. Slaa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema kwa sasa ni Balozi nchini Sweden. Aliondoka Chadema kwa madai kuwa hakuwa tayari kumnadi Lowassa kama alivyodai, Profesa Lipumba. Je, atakuwa tayari kuachia ubalozi kurejea katika upinzani?

Katika siasa yote yanawezekana kutegemeana na utashi wa wahusika na pia siku moja katika ulimwengu wa siasa inatosha kubadili historia iliyokuwapo hapo kabla, hivyo tutegemee mengi katika siasa.

Hata aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chadema huko nyuma, Zitto Kabwe na baadaye kufukuzwa uanachama na hatimaye kupoteza ubunge wake kwa sasa ni mshirika mkubwa wa chama chake cha zamani katika mambo mbalimbali na hata kwa wana Umoja wa Katiba ya Wananchi -Ukawa.

**HAKUNA ADUI**

Somo linalojiri hapa ni kwamba katika siasa hakuna urafiki wala uadui wa kudumu kwa kuwa ni nani aliyejua kuwa Lowassa na Jakaya Kikwete ambaye alikuwa Rais na kumteua Lowassa kuwa Waziri Mkuu wangeweza kutofautiana?

Ama Profesa Ibrahim Lipumba na Maalim Seif kufikia hatua ya kufikishana mahakamani na mahakama kutoa ushindi kwa Mwenyekiti Lipumba, hatua inayolazimisha Maalim Seif kuhamia ACT -Wazalendo?

Au ni nani aliyejua kuwa Dk. Slaa na Mwenyekiti wa Chadema Freeman Mbowe, hatimaye wangekuja kutofautiana na kufarakana? Ni wazi chama kilichokufukuza leo kinaweza baadaye kukupokea upya kutokana na mazingira ya wakati huo. Mathalani, aliyekuwa Mbunge wa Kigoma Kusini David Kafulila aliwahi kufukuzwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiitwa sisimizi lakini baadaye alikuja kuwa mshirika mkubwa wa Ukawa na hatimaye mkewe ni mbunge wa viti maalum kupitia Chadema.

Kubwa la kujifunza katika siasa ni kuwa kuna mambo yasiyotabirika na ambayo si ya uhalisia, kwa kuwa wanasiasa wanaweza kuhubiri mvinyo lakini kinywaji chao ni maji, aidha wanaweza kuhubiri matumizi ya maji japo ni washiriki wakuu wa mvinyo.

MAKALA

Inatoka Uk.13

# Kilichotokea kwa Lipumba, Seif hatima ya kilichoanza mwaka 2015

Kijitonyama Dar es Salaam, walikuwa na tukio la kugawa kadi nyingi kwa wanachama wapya, wengi wanadaiwa wanatokea CUF.

Haya yanatokea ikiwa ni takribani miaka minne tangu wawili hao Profesa Ibrahimu Lipumba na Maalif Seif waanze kufarakana na katika siku za karibuni Profesa Lipumba anakumbushia kile kilichowagombanisha na kuwasambaratisha, akianza kwa kusema:

"Katika siku ambayo nilikasirika kidogo nirushe ngumi ni kwenye ule mkutano aliokuwa anauongoza Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif mwaka 2015, alituona CUF kama hatuna mkakati kuweka mgombea. Wakati hatujazungumza wala kukubaliana."

Lipumba ambaye amekuwa kiongozi wa chama hicho kwa muda mrefu anasema hayo wiki iliyopo wakati akiwahutubia wanachama wa CUF katika Mkutano Mkuu, ambao ulimchagua kuwa Mwenyekiti wa Taifa, akipata ushindi wa kishindo wa kura 516 sawa na asilimia 88.

Makamu Mwenyekiti wa CUF Bara ni Maftaha Nachuma, aliyepata kura 231 sawa na asilimia 41.9 na Makamu Mwenyekiti Zanzibar ni Abbas Juma Muhuzi, aliyejizolea kura 349 sawa na asilimia 60.

Wakati akiwashukuru wanachama wa CUF baada ya kutangazwa mshindi anagusia tukio la kutaka CUF, licha ya kuwa mwasisi wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), uliovijisha vyama vikuu vya upinzani, asishiriki kwenye kinyang'anyiro cha urais mwaka 2015, badala yake iachie majukumu hayo kwa Chadema.

Anakumbusha kuwa aliumia na kutamani hata kurusha ngumi kwa kuwa kitendo hicho anachokifananisha na kuvuliwa nguo hadharani.

Profesa Lipumba anakumbusha kuwa alifika katika kikao hicho kilichofanyika Dar es Salaam na kumkuta Maalim Seif, akizungumza na viongozi wa Chadema. kuwaeleza kuwa ni lazima wafanye maamuzi ya nani atakuwa mgombea wa urais.

Mwenyekiti mteule huyo. anawakumbusha wajumbe kuwa Maalim Seif alianza kuwahoji CUF iwapo wana mikakati na rasilimali za kutosha za kuwawezesha kugombea urais wa Tanzania mwaka 2015?

Lipumba anasema: "Maana ya kauli hiyo ni kwamba CUF hatuna mkakati wa kuweka mgombea urais kwa mwaka 2015. Anasema hayo wakati anajua kuna nia ya kuweka mgombea urais. Anakuja kunivua nguo hadharani. Hayo mambo yalikuwa ya kuzungumza kwanza na si kueleza kuwa sisi hatuna mpango wowote," anasema Lipumba.

Profesa Lipumba ambaye mara kadhaa amekuwa akipeperusha bendera ya chama hicho kwenye urais, anasema walitakiwa wakubaliane, washauriane wenyewe ndani ya vyama vyao na si mtu mmoja kufanya maamuzi.

Anaongeza : "Tukakubaliana kesho tufanye kikao cha mashauriano asubuhi ofisini Buguruni. Tukamwita Maalim Seif, lakini baadaye akanitumia ujumbe kuwa amepata dharura. Lakini akaahidi kuhudhuria kikao cha saa 9 alasiri siku hiyo. Hii ina maana anataka tuende kwenye kikao cha Umoja wa Katiba ya Wananchi -Ukawa, bila ya kuwa na msimamo wa pamoja wa ndani ya CUF."

Anaelezea kuwa alilazimika kumwambia Hamad kuwa iwapo hatakuja kwenye kikao cha Buguruni naye Lipumba hatashiriki kikao cha Ukawa.

Anakiri kuwa mbele ya wanachama hao kuwa ni kweli katika kipindi hicho ndani ya chama walikuwa hawajajipanga kikamilifu kuhusu mgombea, hivyo alikwenda kukutana na Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Wilbroad Slaa pamoja na viongozi wengine wa chama kujadili zaidi na kukubaliana Dk. Slaa awakilishe Ukawa.

> "Hii ni awamu yangu ya tano kushinda hii nafasi tuna changamoto kubwa, tumeingia katika mgogoro na huu mgogoro nimeuhesabu ni kama vile chuma kimepitishwa kwenye moto kikitoka salama kinakuwa chuma imara zaidi,"



Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (kushoto) muda mfupi baada ya kumkabidhi kadi Maalim Seif (kulia) jana. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF, Prof. Ibrahimu Lipumba kwa miaka zaidi ya 20, akifurahia uongozi.

**KUINGIA LOWASSA**

Mwenyekiti Lipumba anasema wakati wamekubaliana na Dk. Slaa wenzao wa Chadema wakabadilisha gia angani na kumpitisha Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, kuwa mgombea urais wa Ukawa.

"Hapa nilikuwa katika wakati mgumu nikajiuliza hivi kweli Lipumba nizunguke nchi nzima ninamnadi Lowassa kuwa huyu ni mpambanaji."

"Huu mzigo wa kumnadi Lowassa kuwa ni kamanda wa kupambana na ufisadi Tanzania nikaona siuwezi, ndiyo sababu nikaamua kukaa pembeni." Anasema Lipumba.

**KUTOFAUTIANA NA HAMAD**

Profesa Lipumba, anaeleza mambo ambayo walikuwa wanatofautiana na Katibu Mkuu Hamad na kutaja suala la Muungano, akisema msimamo wao ni kuunga mkono mapendekezo ya Tume ya Jaji Francis Nyalali kwamba mfumo utakaokidhi mahitaji yao kwenye Muungano ni ule wa shirikisho la serikali tatu.

Anasema walipokuja kwenye masuala ya kupendekeza mapendekezo ya kupeleka kwenye Tume ya Jaji Joseph Warioba iliyokuwa inakusanya maoni ya wananchi kuhusu katiba mpya, Maalim Seif akapeleka mapendekezo ya CUF kuwa wanataka Muungano wa mkataba jambo ambalo hawakukubaliana.

Profesa Lipumba akumbusha kuwa awali Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, alitaka Chadema ipewe nafasi ya kugombea urais na kama wakishinda nafasi ya Waziri Mkuu itatoka ndani ya CUF.

Anasema Maalim Seif aliliunga mkono na kueleza kuwa katiba ya Zanzibar chama kinachotoa Rais ndicho kinachotoa makamu wa Rais ambaye ndiye kiongozi wa shughuli za serikali.

"Sisi hapa tunashirikiana kilichokuwa tunatakiwa kukifanya ni kuchagua mgombea ambaye wote wanakubaliana na kutekeleza malengo ya Ukawa," anasema Lipumba.

Ukawa ni ushirikiano usiokuwa na malengo ya haki lakini ilivyoonekana wengine walikuwa na mkakati wa kuua vyama vya upinzani.

Anasema kama wangekuwa na mkakati wenye umoja ingesaidia kufikia yale malengo ambayo walikubaliana kuanzisha Ukawa, lakini matokeo yake baadhi ya vyama vililenga kuua vyama vingine, jambo ambalo hawakubaliana nalo.

**VIPI SULUHU**

Aidha, Profesa Lipumba anaeleza bayana kuwa Maalim Seif Sharif, si mtu aliyetaka suluhu katika mgogoro huo.

"Msuguano ndani ya chama ni matokeo ya Maalim Seilf kukataa suluhu jambo ambalo linaonyesha kuwa haitakii CUF mema,"anasema na kuongeza kuwa binafsi alikuwa tayari kwa suluhu na alishafuatwa na viongozi wa dini akawasikiliza, hivyo tatizo lilibaki kwa Maalim Seif.

Katika hilo anamrushia lawama kuwa chama hicho kimekosa nafasi za uwakilishi katika serikali ya Umoja wa Kimataifa, kutokana na misimamo ya Maalim Seif.

**MIKAKATI MIPYA**

Profesa Lipumba anasema maadamu amepewa rungu anakwenda kutibu chama na hatakuwa na msamaha na hao wanaoleta mgawanyiko.

Anayaeleza haya wakati akizungumzia mikakati yake baada ya kushinda nafasi ya uenyekiti kwa mara ya tano, na kusisitiza kuwa anakwenda kutibu majeraha yalitokea ndani ya chama.

"Atakayetaka kuyaendeleza tutamchukulia hatua kali." Anaonya mwenyekiti huyu mzoefu.

"Ninakwenda kukisimamia chama na kuhakikisha kina kuwa imara ili kujiandaa katika Uchaguzi Mkuu wa 2020 kiweze kupata ushindi."

"Hii ni awamu yangu ya tano kushinda hii nafasi tuna changamoto kubwa, tumeingia katika mgogoro na huu mgogoro nimeuhesabu ni kama vile chuma kimepitishwa kwenye moto kikitoka salama kinakuwa chuma imara zaidi," anatamba Lipumba.

**AOTA URAIS ZANZIBAR**

Anaongezea kuwa:"Tunakwenda kutibu majeraha kwa haraka iwezekanavyo tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka 2020 lengo letu kubwa kwa upande wa Zanzibar ni kulinda katiba iliyotupatia serikali ya Umoja wa Kitaifa ili tuwepo katika serikali hiyo na tunataka kushinda uchaguzi wa urais na uwakilishi." Lipumba

Mwenyekiti wa CUF anasema kwa Tanzania Bara watahakikisha wanajenga chama chenye mvuto zaidi na msimamo wa chama ni haki sawa kwa wananchi wote.

Anawapa wajumbe wote waliohudhuria uchaguzi huo, kuhakikisha wanashiriki katika uchaguzi wa serikali za mtaa na kupata ushindi.

**KUIGWA NA CCM**

Aidha, Lipumba anasema, kuna sera zao ambazo zimechukuliwa na CCM, kama elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu, na kwamba CUF ilitangaza tangu 1995.

"Sera ya kuhakikisha tunatumia rasilimali za nchi kama madini kwa manufaa ya nchi ni yetu tangu mwaka 1995 lengo letu sasa ni kuhakikisha haki sawa kwa wote zikiwamo za kiuchumi, kijamii na kisiasa tutayatekeleza kwa kuyajengea hoja," anaahidi mwenyekiti huyu wa CUF.



John Bercow, Spika wa Bunge la Uingereza. **PICHA: DW**

# Mpango wa Brexit wapata pigo tena

MPANGO wa Waziri Mkuu wa Uingereza, kuhusu kujitoa kwenye Umoja wa Ulaya maarufu kama Brexit umepata pigo jipya, baada ya Spika wa Bunge la nchi hiyo kutangaza kwamba, hautapigiwa tena kura bungeni, mpaka utakapofanyiwa marekebisho makubwa.

Katika tangazo la kushtukiza juzi jioni, Spika wa Uingereza John Bercow, alisema wabunge hawawezi kuupigia kura mpango ule ule wa Brexit walioukataa awali katika msimu huu wa Bunge.

Akitumia kigezo cha tukio la mwaka 1604, Spika huyo alisema itakuwa kinyume cha sheria kwa serikali kuwasilisha tena mpango uliokwishapingwa na wabunge.

Tangazo hilo la Spika Bercow limekuja wakati serikali ya Waziri Mkuu, Theresa May, ikihangaika kuwashawishi wabunge kuukubali mpango huo wa Brexit ambao tayari wamekwisha ubwaga mara mbili, ikitarajia kuwa ungepigiwa kura tena wiki hii.

KUIWAJIBISHA SERIKALI

Spika Bercow, alitoa ufafanuzi kuhusu tangazo lake, alisema hataki lichukuliwe kama kauli ya mwisho kwenye mpango wa Brexit, bali kama sharti ambalo serikali inalazimika kulitimiza, ili yeye aweze kuandaa kura ya tatu bungeni kuamua juu ya mpango huo.

Waziri wa Brexit Steve Barclay akijibu tangazo la spika amesema hiyo inamaanisha kwamba yumkini hakutakuwa na upigaji kura wiki hii bungeni, na hiyo ameongeza, inamaanisha kuwa Uingereza itachelewa kidogo kuondoka katika Umoja wa Ulaya.

''Ni uamuzi muhimu, ambao bila shaka unahitaji kutazamwa kwa makini. Tutautafakari kwa kina na tutachukua uamuzi ipasavyo.'' Alisema Barclay.

Chanzo kutoka katika serikali ya Theresa May kimeliambia Shirika la Habari la AFP, kwamba hatua ya Spika Bercow ni ishara kwamba anataka kuchelewesha Brexit kwa muda mrefu, ambapo Bunge litachukua udhibiti wa mchakato mzima likinuia kufikia makubaliano laini na Umoja wa Ulaya.

Kiunzi kingine katika njia ya May kuelekea Brexit

Waziri Mkuu May, alitazamia mpango wake ungeshinda kura ya tatu bungeni hapo kesho Jumatano, kabla ya kusafiri kwenda Brussels ambako ataomba kucheleweshwa kwa tarehe ya Uingereza kuondoka rasmi katika Umoja wa Ulaya, hadi Juni 30, mwaka huu. Wabunge wengi wa chama cha Conservative ambao awali walipinga mpango wa Theresa May, walikuwa wameashiria kuukubali safari hii, kwa masharti mepesi.

Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya hapo jana, walikubaliana na dhana ya kuipa Uingereza muda zaidi, ila walitilia shaka nia ya ucheleweshaji huo.

Ofisa mmoja wa Umoja wa Ulaya (EU), amewaambia waandishi wa habari kuwa umoja huo unaweza kuridhia ombi la Uingereza kutaka muda zaidi wa mchakato wa Brexit, mradi ombi hilo liwasilishwe muda wowote kabla ya Machi 29, 2019 na si baada ya saa 5:00 usiku saa ya London.

Mwanasheria Mkuu wa Uingereza, Robert Buckland, amemkosoa vikali Spika wa Bunge, akisema ameitumbukiza Uingereza katika mgogoro wa kikatiba.

**DW**

# Msimamo wa kundi la G55 ulivyomshangaza Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

TANGU kuibuka kwa vuguvugu la kuundwa kwa serikali ya Tanganyika mwaka 1993, kulikuwa na kila mpango wa kuhakikisha suala hilo linagonga mwamba hata kabla ya kufikishwa ndani ya bunge.

Katika kuhakikisha azima hiyo inafanikiwa, viongozi wa CCM na serikali, akiwamo baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, walifanya kila njia ikiwamo kukutana na baadhi ya wabunge waliokuwa mstari wa mbele kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano, maarufu kama G55.

Vikao kadhaa vilifanyika kikiwamo cha Mwalimu Nyerere na baadhi ya wabunge hao wakiongozwa na mwenyekiti wao Mateo Qaresi (aliyekuwa Mbunge wa Babati) na mratibu wa hoja hiyo, Njelu Kasaka (Chunya).

Baada ya wabunge hao kukutana na Nyerere pamoja na viongozi wa CCM kwa mara kadhaa, Nyerere kupitia aliyekuwa Mbunge wa Bunda, Joseph Warioba, ambaye alikuwa muunganishaji wa mazungumzo hayo, aliwaomba wakutane tena Agosti 15, 1993 nyumbani kwake Msasani.

Kikao hicho kilifanyika saa 4:00 asubuhi huku G55 ikiwakilishwa na Kasaka mwenyewe, John Byeitima (Muleba), Nassoro Malocho (Newala), Mbwete Hombee (Rungwe), Patrick Qorro (Karatu), Qaresi, Arcado Ntagazwa (Kibondo), Jared Gachocha (Ngara), Venance Ngula (Taifa), Lumuli Alipipi Kasyupa (Kyela) na Warioba.

Katika kitabu chake cha 'Njelu Kasaka Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika-G55', Kasaka anasema Mwalimu Nyerere alieleza kuridhishwa kwake na utendaji wa Bunge hasa kutokana na kushughulikia masuala ya kitaifa kama vile sakata la OIC (Zanzibar kujiunga na Jumuiya ya Kiislamu Duniani- OIC), matatizo ya Muungano.

Hata hivyo, alisema kuhusu kutetea taifa, kunahitajika kujitoa mhanga, jambo ambalo Watanzania wengi hawajaonyesha kuwa tayari.

"Nilimuuliza maana ya Watanzania kujitoa mhanga akasema kwa kusema kwa uozo uliopo (wakati huo) serikalini, alitarajia kuona baadhi ya mawaziri wanajiuzulu," anabainisha Kasaka huku akiongeza kuwa alimpongeza Jenerali Ulimwengu kwa kujiuzulu ukuu wa wilaya.

Pamoja na hayo, Kasaka alisema Mwalimu Nyerere hakuridhia kuwapo kwa serikali ya Tanganyika hasa kutokana na kauli ya wabunge wa kundi la G55 kuwa hawako tayari kulegeza msimamo wao wa kudai serikali ya Tanganyika.

"Tulimweleza Nyerere kwamba hadi hapo Zanzibar itakapokoma au kuzuiwa katika madai ya kuwa na mamlaka kamili na kuacha kukiuka Katiba ya Muungano, hatutalegeza msimamo wetu wa kudai Tanganyika," anasema.

"Tulipofika hapo, Mwalimu Nyerere alikubaliana na sisi na kusema tabia na mwenendo wa Zanzibar vilikuwa vinahatarisha uhai wa Muungano. Hata Nyerere mwenyewe, tulibaini kwamba hakuwa na uhakika wa nini kifanyike kukabiliana na tatizo la Zanzibar," anaongeza.

Aidha, anasema katika kikao hicho, Ntagazwa alimweleza Nyerere kwamba mazingira ya kisiasa Tanzania yalikuwa yamebadilika kiasi kwamba mbinu za zamani zilizotumika kuendesha Muungano haziwezi kutumika ikiwamo matumizi ya nguvu ambayo hayakubaliki "katika jamii za leo zinazojiendesha kidemokrasia".

"Siku hiyo pia tuliachana na Mwalimu Nyerere bila kukubaliana kwa kufikia mwafaka wa aina yoyote," anasisitiza.

> "Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaunga mkono hoja kikamilifu na mimi binafsi nikiwa Mbunge wa Urambo, naunga mkono hoja... baadhi ya watu hawakuelewa sababu iliyowasukuma wale walioanzisha hoja hii wakifiriki walikuwa waasi miongoni mwa wanachama wa CCM na miongoni mwa wabunge,"

HOJA KUWASILISHWA

Wakati vuguvugu hilo likiendelea na mkutano wa Bunge la Bajeti kwa mwaka 1993/94 ukiwa unakaribia ukiongoni, hatimaye Ofisi ya Spika ilitangaza kwamba Hoja Binafsi ya Tanganyika itawasilishwa Agosti 23, 1993.

Baada ya tangazo hilo, viliibuka vigingi zaidi kwa serikali kutaka kufanya kila mbinu ili kuhakikisha hoja hiyo haiwasilishwi bungeni kama Ofisi ya Spika ilivyotangaza.

Kigingi kilichowekwa kwa wakati huo ni kwa Kiongozi wa Shughuli za Bungeni, John Malecela, aliitisha kikao cha wabunge wa CCM kujadili uwezekano wa hoja kuondolewa kabla ya kuwasilishwa.

"Ilionekana kwamba viongozi wa serikali na wale wa CCM walikuwa bado na matumaini kwamba wajumbe wa G55 wataiondoa hoja yao kabla ya tarehe ya kusomwa Bungeni. Hata Mwalimu Nyerere alikuwa na mawazo kama hayo," anaeleza Kasaka.

Katika kikao hicho, Kasasa anasema aliyekuwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Samuel Sitta, ambaye alikuwa kiongozi wa timu ya serikali ya majadiliano na G55, alieleza msimamo na matazamio yake kwamba hoja ya Tanganyika itaondolewa kabla ya kusomwa Bungeni.

"Mwenyekiti wa kikao, John Malecela, alinitaka nizungumze mara tu baada ya Sitta kwa niaba ya G55. Hotuba yangu ilikuwa fupi. Nilisisitiza kwamba wabunge wa G55 wanataka serikali ikubali kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano. Bila hilo wabunge hawako tayari kuachana na hoja yao," alisema.

Baada ya kueleza msimamo huo, anasema wabunge waliopata nafasi ya kuzungumza, waliunga mkono msimamo huo huku aliyekuwa Mbunge wa Mahenge, Guntram Itatiro, alimwambia kwa kinagaubaga Malecela kuwa hakuwa na pa kukwepea isipokuwa 'kukinywea kikombe hiki'.

HOJA YAWASILISHWA

Hatimaye hoja iliwasilishwa Agosti 23, 1993 kama ilivyokuwa imepangwa pamoja na kuwapo vuta nikuvutwe ambazo zingesababisha kukwama. Baada ya Kasaka kuwasilisha hoja hiyo, aliyekuwa Mbunge wa Lindi Mjini, Abdalla Said Nakuwa aliunga mkono.



Katika kuwasilisha hoja hiyo, Kasaka alieleza kuwa sababu kuwa ya kufikia hatua hiyo ni tabia na mwenendo wa Zanzibar kama sehemu ya Muungano hususan madai kwamba ni nchi kamili katika Muungano wa nchi mbili, hivyo kilichobaki kwa hilo ni Tanganyika.

Sababu ya pili, kwa mujibu wa Kasaka, ni kuleta usawa kati ya mataifa mawili yanayounda Muungano wa Tanzania.

"Katika Zanzibar, kila kitu ni kwa Wazanzibari lakini kwa Tanganyika ambayo ilikabidhi mambo yote kwa Muungano, kila kitu ni kwa Watanzania wote... kibaya zaidi, Zanzibar inazuia wananchi kutoka Tanzania Bara kushika nyadhifa Zanzibar hata kwa idara za Muungano. Viongozi wake wanataka nafasi zote zijazwe na Wazanzibari tu," anasema.

"Zaidi ya hapo, nilieleza kuwa hata viongozi na watendaji wa serikali ya Muungano wanaotokea Bara, hawafanyi kazi zao kwa uhuru ndani ya Zanzibar," anaongeza.

Baada ya kuwasilishwa kwa hoja hiyo, Sitta kwa niaba ya serikali, aliunga mkono hoja. Kasaka anasema katika hotuba yake fupi, Sitta alisema hoja hiyo ni muhimu na ya busara kwa maendeleo ya nchi kisiasa, kiuchumi na kijamii.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaunga mkono hoja kikamilifu na mimi binafsi nikiwa Mbunge wa Urambo, naunga mkono hoja... baadhi ya watu hawakuelewa sababu iliyowasukuma wale walioanzisha hoja hii wakifiriki walikuwa waasi miongoni mwa wanachama wa CCM na miongoni mwa wabunge," anakuliwa Sitta katika kitabu hicho.

Sitta alimalizia kwa kusema: "Watu hawa ni ndugu zetu, wameimarisha mchakato wa kisiasa wa nchi yetu na wamefanya hivyo kwa busara, uangalifu na kwa kuzingatia demokrasia."

Malecela kwa upande wake alisisitiza maelewano na mshikamano wa kitaifa ili kudumisha Muungano katika muundo mpya utakaobuniwa huku akionya ubinafsi na kulaumiana kwamba vitawagawa Watanzania.

**• Nini kilitokea baada ya hapo? Soma kwa undani zaidi katika kitabu chake na dondoo katika makala ijayo.**

# EAC imsaidie Tshisekedi kukamilisha miradi ya Kabila

**Na Mashaka Mgeta**

SERIKALI mpya ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imeingia madarakani kutokea 'chama kipya' cha Union for Democracy and Social Progress (UDPS) kinachoongozwa na Rais Felix Tshisekedi, huku taifa hilo likigubikwa na migogoro na vitendo vya uporwaji rasilimali za taifa hilo.

Rais Tshisekedi alishinda nafasi hiyo katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Desemba 30, mwaka jana, kwa kupata kura milioni 18 (kabla ya maeneo mengine kupigwa na kuhesabiwa) ikiwa ni sawa na asilimia 38.57 na kumpita mshindani wake wa karibu, Martine Fayulu aliyepata kura milioni 6.4.

Mgombea wa chama tawala cha People's Party for Reconstruction and Democracy (PPRD), Emmanuel Ramazani Shadary, aliyetarajiwa kushinda kutokana na kuungwa mkono na Kabila, aliambulia kura milioni 4.4.

**HALI YA DRC**

Inapotajwa DRC, fikra inayojitokeza kwa haraka ni kuwapo kwa vikundi vya waasi, mapigano yanayosababisha vifo na majeruhi na madai ya kuwapo askari kutoka nchi jirani wanaokwenda kusaidia harakati za waasi nchini humo.

Ingawa ni hivyo, DRC iliyoachwa na Rais mstaafu Joseph Kabila, inaendeleza miradi kadhaa ya maendeleo ya nchi na ustawi wa watu.

Miradi hiyo kama ilivyo kwa mataifa mengine yanayoendelea ni mingi, ikitegemea washirika wake wakiwamo wadau wa maendeleo na nchi majira zikiwamo zile za kikanda. Miongoni mwa washirika wakubwa wa DRC ni kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zilizowahi kuonyesha nia ama kusaini mikataba ya kushirikiana na serikali ya Kabila.

Kuimarika kwa ushirikinao kati ya DRC na nchi za EAC ni jambo lisilokwepeka kwa kuwa licha ya kukuza biashara, uchumi na uzalishaji, pia unachangia kuimarisha usalama wa ukanda huo.

**MAENEO YA USHIRIKIANO**

DRC ina maeneo mengi yenye umuhimu wa kukuza ushirikiano na hivyo kuifanya serikali ya Rais Tshisekedi kuhitaji msaada endelevu kutoka kwa wanachama wa EAC.

Oktoba 2016, Kabila alifanya ziara ya kikazi nchini na kusaini mikataba kadhaa na mwenyeji wake, Rais John Magufuli, hatua hiyo inakuja wakati ujazo wa biashara



Rais mstaafu Kabila, pamoja na Felix Tshisekedi, baada ya kuapishwa kuongoza DRC. **PICHA:MTANDAO**

kati ya Tanzania na DRC ukiwa umekua kutoka shilingi bilioni 23, mwaka 2009 hadi bilioni 394 mwaka 2016.

Kwa mujibu wa ripoti ya Wakala wa Uwezeshaji wa Usafiri wa Ukanda wa Kati (CCTTFA) ya mwaka 2015, DRC ilipitisha tani milioni 11 za shehena kupitia bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni sawa na asilimia 10 ya bidhaa zote zinazoingizwa kupitia bandarini hapo.

Kiwango cha asilimia ya bidhaa za nchi nyingine bandarini hapo ilikuwa ni wenyeji Tanzania asilimia 62, Rwanda 7.0, Burundi 3.0 na Uganda moja nyingine zisizokuwa kwenye ukanda huo zilikuwa na jumla ya asilimia 17.

Pia katika kipindi cha mwaka huo (2005) kiasi cha asilimia 25 ya bidhaa zilizosafirishwa nje kupitia bandari ya Dar es Salaam, zilitokea nchini DRC wakati asilimia 65 zilitokea hapa nchini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, bidhaa za kutoka nchi za Rwanda, Burundi na Uganda zilikuwa katika kiwango cha asilimia 1.6, wakati bidhaa kutoka mataifa yasiyokuwa katika ukanda huo zikiwa na asilimia 9.4.

Katika mazungumzo ya wakuu wa nchi hizo, ilikubaliwa kwamba Tanzania itaongeza muda wa msamaha wa tozo kwa bidhaa zinazoingizwa Dar kwenda DRC kutoka siku 14 hadi 30.

Aidha, ilikubaliwa kwamba Tanzania itatenga eneo la bandari kavu huko Ruvu mkoani Pwani na Dodoma kwa mizigo inayokwenda DRC ili kurahisisha utoaji na usafirishaji wake.

Rais Magufuli akaihakikishia Congo kwamba Tanzania itajenga reli ya kisasa ya standard gauge (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma ili itumike kufikisha mizigo DRC kupitia bandari ya Ziwa Tanganyika mkoani humo.

Katika utekelezaji wa makubaliano hayo na kuongeza ufanisi, Tanzania iliahidi kuziboresha bandari ya Kigoma ili ishirikiane na zile za Kalemie, Kalundu na Moba nchini DRC kusafirisha shehena.

Pia, Tanzania ikapunguza vituo vya upimaji uzito wa magari ya mizigo yakiwamo ya DRC kutoka vinane kufikia vitatu vilivyopo Vigwaza, Manyoni na Nyakahura.

Wakati wa mazungumzo hayo, Kabila alisisitiza kuwa Dar es Salaam ndiyo bandari chaguo kwa ajili ya kuingiza na kusafirisha shehena ya Congo.

Kwa upande wa Uganda, mradi wa SGR unajengwa kutokea Pakwach kupitia vituo vya forodha vya Goli na Vurra huko Arua, haya ni maeneo muhimu ya kuingilia kaskazini mashariki mwa DRC.

Mradi wa SGR unagharimu mabilioni ya dola za Marekani, ukitarajiwa si tu kuunganisha nchi zilizo katika ukanda wa kaskazini, lakini pia kupunguza gharama za kufanya biashara.

**UGANDA NA DRC**

Gazeti la Monitor la nchini Uganda ni miongoni mwa vyombo vya habari vilivyochambua kwa kina nafasi ya Uganda katika kushirikiana na serikali ya Tshisekedi na kwamba hali hiyo inapaswa kuwapo kwa nchi zote za EAC.

"Kutangazwa kwa Tshisekedi kuwa mshindi wa urais kunachagiza matumaini miongoni mwa marafiki zake waliokuwa wakimfanyia kampeni kwa zaidi ya miaka mitano ili aachiwe huru, utawala huo mpya utakuwa tofauti?" Lilihoji gazeti hilo.

Mwaka 2005, Mahakama ya Kimataifa ya Haki iliiamuru Uganda kulipa fidia DRC baada ya kupatikana na hatia ya kuhusika na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu. DRC ilikuwa ikidai fidia ya Dola bilioni 10 za Marekani.

Licha ya madai hayo, DRC na Uganda zimekuwa katika mgogoro wa mara kadhaa unaohusu kuingiliwa kwa ardhi zao na majeshi yanayotoka upande mwingine. Kwa hali hiyo, Uganda bado inaendelea kuwa na umuhimu wa pekee katika kupata suluhu ya changamoto zake kwa DRC.

**KENYA**

Serikali ya Rais Uhuru Kenyatta inajenga SGR kutoka Mombasa hadi Kisumu mahali lilipo Ziwa Viktoria ili kuiungaisha nchi hiyo na mataifa mengine hususani katika nyanja za uchukuzi kwenye uchumi, biashara na uzalishaji.

**ALIPOANZIA KABILA**

Mwaka 2016, Rais huyo mstaafu wa DRC, Joseph Kabila, alitangaza nia ya taifa hilo kuwekeza katika ujenzi wa SGR na kwa mujibu wa jarida la Star Africa, kusudio hilo lilitamkwa pia na Balozi wa DRC nchini Uganda, Jean Pierre Massala, katika mkutano wa 13 wa miradi ya utengamano wa kaskazini (NCIP) uliofanyika jijini Uganda Aprili, 2016.

Miradi ya utengamano ya ukanda wa kaskazini ni jitihada ambazo pamoja na mambo mengine, zinapunguza gharama za kufanya biashara na kuboresha miundombinu kwa nchi zinazotumia bandari ya Mombasa.

Nchi zilizosaini mkataba wa ushirikiano katika ukanda huo ni Uganda, HYPERLINK "http://www.trademarkea.com/countries/rwanda/" \t "_blank" Rwanda, Sudan Kusini na Kenya, wakati DRC, Tanzania na Ethiopia zilikuwa waangalizi.

Jarida hilo lilieleza kuwa mradi wa SGR kwa DRC unahusu ujenzi wa reli ya kisasa, yenye uwezo mkubwa itakayoanzia bandari ya Mombasa nchini Kenya, kupitia Nairobi, Kampala -Kigali hadi Juba nchini Sudan Kusini.

Nchi nne za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutumia viwango sawa vya SGR ingawa kila taifa litajenga kwa upande wake, hivyo ilikuwa mara ya pili kwa DRC kuelezea nia hiyo, ikitanguliwa na tamko lake ililolitoa kwenye mkutano wa 11 wa NCIP uliofanyikia jijini Nairobi, Kenya.

Ingawa taarifa hizo ni kati ya nyingi zinazoyahusu mataifa hayo, umuhimu wa nchi wanachama wa EAC kuisaidia DRC ili ifikie malengo ya maendeleo hasa yaliyoanzishwa na mstaafu Kabila, ambayo yana maslahi kwa pande zote, si jambo la kubeza bali la kulifanyia kazi kwa nguvu zote.

**Makala haya yameandikwa kutoka vyanzo mbalimbali. Maoni 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.**

MAKALA

# Uhamaji Afrika unafukuza wenye ubunifu, wagunduzi

Na Gaudensia Mngumi

SUALA la wahamiaji wa Afrika kukimbia nchi zao na kujipeleka Ulaya na Marekani, licha ya kuonekana kuwa pengine halina athari kwa Afrika, ukweli ni kwamba bara linaathirika vibaya pale linapoondokewa na nguvu kazi, ambayo ingeleta maendeleo kupitia utaalamu, vipaji na ubunifu.

Suala la kuwa na wakimbizi, wahamiaji na waomba hifadhi ni la siku nyingi barani Afrika kiasi kwamba nchi za kusini ya Jangwa la Sahara ni moja ya eneo ambalo wananchi wengi kutoa mataifa ya ukanda huo wanaishi kwa mataifa jirani.

Mfano Tanzania ina raia wengi kutoka Congo DRC, wanaoishi mikoa ya Katavi, Rukwa na Kigoma, lakini pia Afrika Kusini ni makao ya Wazimbabwe, Wazambia wakati Kenya ina wakimbizi, wahamaji na wageni wengi kutoka Sudan, Ethiopia na Somalia. Aidha, Uganda pia ni makao ya Wasudani wanaokimbia nchi yao, lakini pia kuna raia wa Burundi, Rwanda na Congo. Ndivyo pia kuna raia wa Chad na Cameroon wanaoishi Nigeria. Si hivyo tu, kuna mamilioni ya Waafrika wanaoishi Ulaya na Marekani.

Katika mazingira hayo Afrika inaondokewa na wasomi, wataalamu na nguvu kazi ambayo ingehitajika kwa ajili ya maendeleo. Ukweli ni kwamba kuwaachia wananchi kuwa wakimbizi, kuomba hifadhi na kuwa wahamaji kunarudisha nyuma maendeleo.

**CHANZO CHA UHAMAJI**

Kinachochangia Waafrika kuzikimbia nchi zao na kuomba hifadhi kwa majirani au kupanda meli bila kujali kuzamishwa ndani ya bahari ya Mediterranean ili kwenda Ulaya, kwa mujibu wa Bhekunusa Moyo, raia wa Zimbabwe, ambaye anaishi ughaibuni kutokana na changamoto za uhamiaji ni haya.

Umaskini, kukosa ajira kwa vijana na hali mbaya ya uchumi. Anayaita majanga yanayowalazimisha vijana kuondoka kwenye mataifa yao.

"Kingine ni siasa chafu zinazotokana na migogoro ya uchaguzi, viongozi kung'ang'ania madaraka, kuua na kutishia wapinzani wa kisiasa na wanahaharati." Anasema Moyo kwamba yamechangia Waafrika wengi kuhama nchi zao.

Afrika imekuwa pia bara la hofu lisilokuwa na amani kutokana na kuwapo makundi ya kigadi kama boko haramu nchini Nigeria, Al Shabab huko Somalia.

Vita vya chuki za kikabila zinazosababisha kuua mfano kabila la Waoromo nchini Ethiopia kupigana na Wasomali na Waamhari, pia vita vya makabila ya wafugaji na wakulima kugombania ardhi kwa ajili ya ufugaji na kilimo yamechangia.

Chuki nyingine ni za kuwachukia watu wa mataifa ya kigeni kwa mfano vijana Afrika Kusini kuanzisha mapambano dhidi ya wageni kutoka Msumbiji, Zimbabwe na Zambia, zinatajwa.

Moyo anayetoa maelezo hayo kabla ya Mkutano wa Wakuu na Viongozi wa Afrika (AU) kwenye jukwaa la asasi za kiraia na vyombo vya habari vya Afrika, mwezi uliopita huko Addis Ababa, anasema kukiuka haki za binadamu, kutesa watu hasa wanawake, watoto na wanyonge kunawalazimisha kukimbia.



Profesa Wole Soyinka, mshindi wa Tuzo ya Nobel, anayefundisha Marekani baada ya kutishiwa maisha Nigeria. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> "Uchaguzi ni tatizo linalosababisha uvunjifu wa amani na mauaji ya raia wengi barani Afrika, ndiyo maana ACDEG imeelekeza kuwa ni lazima kuwa na tume huru za uchaguzi Afrika,"



Mwenyekiti wa AU, Al Sisi, ana kazi ya kusimamia utekelezaji wa mikataba inayolinda demokrasia na kudumisha amani.

Lakini pia, vyombo vya dola, kama polisi na jeshi kuwatesa na kuwanyanyasa wapinzani wa kisiasa pamoja na kuwaua na kujeruhi raia, husababisha watu kutoroka mataifa yao.

Akiwageukia vijana, kundi hili kutafuta malisho ya kijani na fursa za kiuchumi kunachangia Waafrika kukimbia bara lao na hasa inapotokea hisia kuwa nchi fulani ina maisha bora kuliko nyingine.

**ATHARI**

Moyo anaonya kuwa japo Afrika inachukulia ukimbizi na uhamiaji kuwa ni changamoto, ukweli ni kwamba mamilioni ya nguvu kazi na wataalamu wanatumikishwa na kunufaisha nchi za ughaibuni.

"Hapa kuna wenye vipaji na utaalamu. Wanaiacha Afrika. Wameajiriwa Ulaya na Amerika. Akili, vipaji, ubunifu, ugunduzi vinaondoka kila mwaka. Wawe wasanii, wacheza mpira, wataaluma na watunzi..." anasema Moyo.

Anawataja wasomi kama Profesa Ngugi Wathiong'o wa Kenya, Profesa Wole Soyinka wa Nigeria wamelazimika kuhama nchi zao na vipaji vyao kwa kuhofia usalama wao.

"Akili kubwa na vipaji vya kipekee vinatumika kuendeleza Ulaya na Amerika wakati Afrika inaendelea kurudi nyuma na kuomba misaada." Anaongeza Moyo.

Kuchanganyikiwa ni athari nyingine zinazowapata, waomba hifadhi ugenini na hata wakimbizi kwa kuwa wengi hupitia misukosuko kiasi cha kufadhaika, kupata sononа na kuwehuka.

Ukimbizi umekuwa na athari nyingine za ndani ya Afrika kwa sababu ndicho chanzo cha watu wengi kukimbia vijijini na kuhamia mijini na vijijini.

Wakifika mijini wanakwamishwa na ugumu wa maisha kama, uhaba wa huduma za kijamii; nyumba za makazi, maji, barabara, shule na hospitali.

**UFUMBUZI**

Anakumbusha kuwa, Afrika imeandaa mkataba wa Demokrasia, Uchaguzi na Uongozi (ACDEG) huo ndiyo mwarobaini wa tatizo hilo, anasema Moyo.

Mkataba huo unazungumzia uongozi kwa kuzingatia katiba, utawala wa sheria, haki za binadamu, ushirikishwaji wananchi na uwazi katika masuala yote ya uongozi wa umma.

Hayo ni masuala yanayotajwa katika sura ya nne ya mkataba wa ACDEG.

"Uchaguzi ni tatizo linalosababisha uvunjifu wa amani na mauaji ya raia wengi barani Afrika, ndiyo maana ACDEG imeelekeza kuwa ni lazima kuwa na tume huru za uchaguzi Afrika, anasema Moyo.

Anaongeza : "Mkataba huu unataka uhuru, haki, amani na uwazi kwenye kuchagua viongozi. Pia kuruhusu matokeo kuhojiwa na mchakato kukoselewa mahakamani."

Hivi karibuni uchaguzi na uongozi umekuwa chanzo cha vurugu nchini Togo wananchi wanataka kukomesha uongozi wa ukoo wa Eyadema uliotawala nchi hiyo kwa miaka 50.

Tangu mwishoni mwa mwaka jana, wananchi wanaandamana kumpinga Faure Gnassingbé aliyeingia madarakani 2005 akichukua kijiti kwa baba yake Gnassingbé Eyadema, aliyeanza kuongoza Togo tangu 1967.

Zimbabwe nako kumekuwa na vurumai za kuwakamata watetezi wa haki za binadamu na wasiasa wanaoukosoa uongozi wa Rais Emerson Mnangagwa.

Changamoto za uchaguzi pia zinaitikisa Algeria, wananchi wanataka Rais Abdelaziz Bouteflika, licha ya kutangaza kuwa hana nia ya kugombea tena kiti hicho kwa muhula mwingine, aondoke ikulu.

Wananchi waliandamana na kumshutumu rais huyo mwenye umri wa miaka 82 kwa kurefusha zaidi muhula wake kinyume cha sheria na kung'ang'ania uongozi.

**UMOJA WA AFRIKA**

Mwezi uliopita wakuu wa Umoja wa Afrika (AU) walikutana Ethiopia kwenye mkutano wa kawaida, na kuazimia kuwa Bara la Afrika liunde sera za kuboresha huduma za wakimbizi. Viongozi wa AU walikubaliana kuwa na sera za kuwawezesha wakimbizi na watu waliolazimika kuyahama makazi yao kupata maisha bora na huduma muhimu katika nchi wanazoishi.

Wakiwa na Mwenyekiti mpya wa AU, Abdel Fattah al- Sissi, Rais wa Misri, viongozi wanakubaliana kupata suluhisho la kudumu kwa chanzo cha watu kulazimika kuyahama makazi na mataifa yao.

Al- Sissi, anakumbusha kuwa ni lazima kuwa na nafasi zaidi za ajira kwa vijana, kuongeza ufanisi, kuimarisha uchumi, na kuwasaidia wakimbizi na waliolazimika kuyahama makazi yao kwa kukidhi mahitaji yao, pamoja na kuweka sera kusaidia kuyajenga upya mataifa yaliyoharibiwa na vita.

Yote hayo ni tisa, kumi, masuala ya uongozi ambayo yamo kwenye mkataba wa ACDEG, Afrika ilitarajia kuona al-Sissi, akihimiza kusainiwa kwa mkataba huo ambao una jibu na kila swali linalohusu Afrika.

Kukosekana demokrasia, usalama wa wapinzani, kero za uchaguzi, kuibuka makundi ya kigaidi kumechochea sana uhamiaji haramu na ukimbizi kwa vile hakuna utulivu kwenye nchi nyingi.

Kukosekana uongozi bora, kushamiri rushwa, wizi wa mali ya umma, kupuuza sheria na katiba kumeendelea kusababisha vita na mzozo mingi tangu uhuru hadi sasa, hivyo dawa yake ni kutekeleza mkataba huo wa ACDEG na liwe jukumu la Al-Sissi.



# DC ataka wananchi waache chuki kwa wawekezaji

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi, amewataka wananchi katika Kijiji cha Igodima kilichopo Kata ya Chokaa, wilayani humo, kuacha chuki dhidi ya wawekezaji wa madini kijijini hapo na badala yake washirikiane nao ili na wao waweze kunufaika na uwekezaji huo.

Maryprisca (pichani) alitoa kauli hiyo jana, wakati wa mkutano wa kusikiliza kero za wananchi ambapo alisema kumekuwapo na uhusiano mbaya baina ya wawekezaji wadogo wa madini katika kijiji hicho na wananchi hali ambayo inakwamisha shughuli za uchumi.



Alisema wananchi wa kijiji hicho wana mgogoro wa eneo la madini la mwekezaji Joseph Mwazyele ambaye anadaiwa kumili ekari 10 za eneo la kuchimbia madini.

Wananchi wa kijiji hicho wanadaiwa kuingia na kufanya shughuli za uchimbaji madini katika eneo la mwekezaji huyo bila kibali chake na kwamba wanapokatazwa wanatoa lugha za fedheha na matusi.

"Nimesikia wananchi wa kijiji cha Igodima mmeweka chuki na mwekezaji wa madini katika eneo hilo, wakati yupo kisheria mnashindwa kutumia fursa hiyo kupata ajira ili mjiingizie kipato mnaanza kushindana naye suala hilo halikubaliki," alisema Maryprisca.

Mwekezaji mdogo wa madini katika kijiji hicho, Joseph Mwazyele, alisema wananchi wamekuwa wakivamia eneo lake la madini bila ruhusa na kufanya shughuli za uchimbaji.

Alisema anapojaribu kukaa na wananchi hao kuwaelekeza wanamtolea lugha zisizofaa, huku wakidai kuendelea na shughuli za uchimbaji katika eneo hilo.

# Ntinika amaliza mgomo wa daladala kwa kutoa tamko

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MGOMO wa madereva wa mabasi ya kusafirisha abiria jijini Mbeya maarufu kwa jina la daladala, umemalizika baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya kuingilia kati.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alilazimika kuita wadau wote wa usafirishaji wa abiria jijini Mbeya na kuzungumza nao ambapo wamefikia makubaliano yaliyosaidia kumalizika kwa mgomo huo.

Akitoa taarifa ya makubaliano hayo mbele ya madereva wa daladala na bajaji katika kituo cha daladala cha Kabwe, Ntinika alisema kuwa wamekubaliana bajaj ziondolewe kufanya kazi kwenye barabara kuu na njia zinazotumiwa na daladala na badala yake zikafanye kazi kwenye njia na vituo walivyopangiwa.

**Tumekubaliana na tumeamua kwamba bajaj zote ziondoke kwenye barabara kuu na badala yake zikafanye kazi kwenye maeneo waliyopangiwa tangu zamani.**

"Tumekubaliana na tumeamua kwamba bajaj zote ziondoke kwenye barabara kuu na badala yake zikafanye kazi kwenye maeneo waliyopangiwa tangu zamani," alisema Ntinika.

Ntinika alisema kuwa makubaliano mengine ni kuzitaka bajaj zote za Mbeya kuwekwa mkanda unaoonyesha njia na eneo zinakopaswa kufanya kazi ili zifahamike kwa lengo la kuepusha ukiukwaji wa taratibu, sheria na makubaliano waliyoafikiana.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya alisema kuwa ameliagiza Jeshi la Polisi kusimamia sheria na kukamata bajaj zote zinazovunja sheria na kuzichukulia hatua kali.

Ntinika alisema kuwa kuanzia sasa ni marufuku kwa bajaj kubeba zaidi ya watu wanne ambao wanapaswa kuketi siti ya nyuma na mbele akae dereva pekee.

Pia alisisitiza kuwa madereva wote kuanzia wa bajaj na wale wa daladala ni lazima wawe na leseni inayowaruhusu kuendesha vyombo vya moto kwa mujibu wa sheria za nchi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Ulrich Matei, alisema kuwa wajibu wake ni kusimamia sheria na kutekeleza makubaliano na maelekezo anayopewa na serikali na kwamba utekelezaji wa makubaliano hayo unaanza mara moja.

Alisema kuwa Jeshi la Polisi litasimamia kikamilifu makubaliano waliyofikia na kuhakikisha sheria za usalama barabarani zinafuatwa ili kuhakikisha mgomo kama huo haujirudii tena.

"Mimi jukumu langu ni kusimamia sheria na kuhakikisha makubaliano waliyofikiwa yanatekelezwa ipasavyo, hivyo kuanzia sasa nawaagiza askari wangu kuanza utekelezaji wa kuziondoa bajaj zote barabara kuu na pia nawataka madereva wa daladala kuachana na mgomo wenu na muingize magari barabarani muhudumie wananchi," alisema Matei.

Mwenyekiti wa waendesha bajaj Jiji la Mbeya, Said Ramadhan, alisema kuwa wanayapokea maelekezo ya serikali na wameridhia kuondoa bajaj zao barabara kuu na kupisha njia zote zinazotumiwa na daladala.

Hata hivyo alisema kuwa serikali inapaswa kuwajengea miundombinu katika njia wanazopitia ili na wao wafanye kazi zao kwa utulivu bila kuingiliana na njia za daladala.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Net-Soft Consult, Richard Shirima, akiongea na wadau jijini Dar es Salaam jana, kuhusu faida zinazotokana na mfumo mpya wa kidigital (FMAS) wa kudhibiti wizi na uchakachuaji wa mafuta na bidhaa zingine za petroli katika sekta za umma na binafsi nchini Tanzania. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wahamasishwa kupima saratani

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WANAWAKE mkoani Mbeya wamehamasishwa kufika kwenye vituo vya afya mara kwa mara kwa ajili ya kuchunguza ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi ambao unatajwa kuwa ni tishio kwa wanawake.

Wito huo ulitolewa jana na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Uzazi kutoka katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya Kitengo cha Huduma ya Mama na Mtoto Meta, Dk. Elias Kaminyoge, alisema kinamama wengi hawana utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara.

Alisema faida za kupima mara kwa mara ni nyingi kuliko kuchelewa kugundua tatizo na kwamba mtu akigundulika na dalili za ugonjwa huo anaweza kupata dawa za kuzuia au kumaliza kabisa tatizo.

Dk. Kaminyoge alisema ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi ni hatari kutokana na kusababisha vifio vingi vya kinamama.

"Saratani ya shingo ya kizazi ni saratani inayoongoza kwa kusababisha vifo vya wanawake katika nchi zinazoendelea, huku ripoti ya mwaka 2012 ya shirika la afya duniani ikibainisha kuwa waathirika elfu 50 walifariki dunia barani Afrika," alisema Dk. Kaminyoge.

Alisisitiza pia kinababa kuwa mstari wa mbele kuwahimiza wake zao kwenda kwenye vituo vya afya na hospitali kupima saratani ya mlango wa kizazi.

Alisema endapo kinababa wakiwa sehemu ya kuhamasisha upimaji wa ugonjwa huo kinamama ambao watapimwa na kubainika na maambukizi ya ugonjwa huo watapewa huduma nzuri ili kukabiliana na saratani hiyo.

Baadhi ya wahudumu wa Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya Kitengo cha Huduma ya Mama na Mtoto Meta, walisema miongoni mwa sababu zinazosababisha kinamama kukutwa na maambukizi ya saratani ya mlango wa kizazi ni matumizi holela ya dawa za kujikinga na mimba.

Walisema kinamama wengi wanatumia njia za asili ambazo hazijathibitishwa na wataalamu wa afya kujikinga na mimba ambapo dawa hizo zinatumiwa kiholela na kusababisha madhara kwenye kizazi.





# ATCL kupasua anga Ulaya kutokea Mwanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amesema Shirika la Ndege nchini (ATCL), linatarajia kuanza kurusha ndege kimataifa kutoka Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwenda nchi za Ulaya na Asia.

Kamwelwe alitoa kauli hiyo jana katika uzinduzi wa Ofisi za ATCL mkoani Dodoma uliofanywa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, jijini hapa.

"Karibu tunaanza kurusha ndege ya kimataifa ambayo itatokea Mwanza kwenda Ulaya na Asia, kwa hiyo tupo kwenye hiyo kazi sasa hivi," alisema.

Alisema pia shirika hilo kwa sasa linatakiwa kuanzisha safari zake kwenye nchi ambayo kuna watalii wengi.

**Niwatoe hofu Watanzania kuhusu usalama wa anga letu na watumiaji wa anga letu kutokana na ajali mbili zenye kushabihiana za ndege aina ya boeing 737 max B...**

"Sasa hivi Israeli tunapata watalii 40,000 kwa mwaka, hivyo itasaidia sana kwenye upangaji wa ndege za kimataifa," alisema.

Aliwataka watendaji wa shirika hilo kuendelea kupanua na kuboresha huduma za usafiri wa ndani na nje ili kushinda katika soko la usafiri wa anga katika maeneo hayo.

Kuhusu ajali ya ndege ya shirika la Ethiopia, Kamwelwe aliwatoa hofu Watanzania na akawataka waendelee kutumia huduma za ATCL kutokana na mkakati wa kutunza rekodi za usalama wa anga kwa kuwa huduma za shirika hizo ni za kiwango cha juu.

"Niwatoe hofu Watanzania kuhusu usalama wa anga letu na watumiaji wa anga letu kutokana na ajali mbili zenye kushabihiana za ndege aina ya boeing 737 max B...Watoa huduma wetu hawatumii ndege za aina hiyo na watengenezaji wa ndege hiyo tayari wamechukua hatua kuhakikisha haziruki kokote duniani," alisema.

Alifafanua kuwa hadi hapo uchunguzi utakapokamilika na hatua stahiki kuchukuliwa na wizara imeendelea kutoa kipaumbele cha usalama wa abiria. Kadhalika, alisema serikali itahakikisha ATCL inakuwa na uwezo wa kushinda katika soko la ndani, kikanda na kimataifa kwa kutumia masafa mafupi ya kamati na marefu kwa kutumia mifumo ya kisasa katika kuuza tiketi.

Aliwataka waendelee kupanua mtandao wa usafiri wa anga ndani na nje ya nchi, pia waangalie soko la Mwanza kwa kuanzisha usafiri kutoka Dodoma kwa ajili ya kuhakikisha wanapata usafiri nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema wanataka kuanzisha safari ya kwenda Mtwara, Iringa na Mpanda mara watakapokagua miundombinu muda wowote na kuona inafaa.



Meneja wa Kanda ya Kati Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Musa Kuzumila, akizungumza katika semina ya siku nne ya wadau wa ofisi hiyo, kutoka mikoa ya Iringa, Dodoma, Singida, Tabora na Morogoro, iliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vituo 46,000 vijijini havitoi maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema vituo vya kuchotea maji 46,000 ambavyo vipo kwenye maeneo ya vijijini nchini havitoi maji.

Akizungumza jana wakati akifungua kongamano la mwaka la wanasayansi ambalo limewakutanisha wafadhili na wadau wa sekta ya maji nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema vituo 131,000 vilivyojengwa kwenye maeneo hayo, vituo 85,000 ndivyo vinavyofanya kazi.

Alisema hali hiyo imefanya upatikanaji wa huduma hiyo hadi kufikia Februari mwaka huu kuwa asilimia 64.

Alieleza kuwa vituo hivyo vina uwezo wa kuhudumia watu milioni 31 na kwamba kama vituo hivyo vyote vingefanya kazi wangekuwa wameshapeleka maji vijijini kwa takribani asilimia 85. Alisema kuwa vituo ambavyo vinafanya kazi ni 85,000 vinahudumia watu milioni 25.

"Kwa hesabu hiyo wananchi wanaopata maji vijijini ni asilimia 64 kwa hiyo kuna vituo takribani asilimia 24, ambavyo havifanyi kazi," alisema.

Kadhalika alisema "katika sheria ya wakala wa maji vijijini tumebadilisha muundo wa jumuiya za watumiaji maji katika ngazi ya vijiji. Walikuwa wanakijiji wanakaa pale lakini sasa tumeweka mfumo wa kitaalamu. Katika jumuiya hizi kutakuwa na mtaalamu atakayehusika na sekta ya maji."

Profesa Mkumbo alisema mtaalamu huyo atahusika na matunzo ya miradi hiyo ambayo inajengwa vijijini na kwamba wamefanya hivyo baada ya kugundua kuwa miradi ambayo serikali imekuwa ikiwekeza karibu asilimia 20 hadi 25 siyo endelevu kwa maana kuwa inakufa baada ya kukosekana kwa utaalamu.

Kwa upande wa upatikanaji wa maji mijini, Profesa Mkumbo alisema hadi kufikia Februari mwaka huu ni kati asilimia 78 hadi 80, hali inayotofautiana kati ya mji na mji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uratibu wa Programu ya Sekta ya Maji katika wizara hiyo, Derosia Mulashani, alisema watatumia kongamano hilo kujitathmini kwa kujilinganisha na nchi nyingine duniani katika kukabiliana na changamoto zinazohusu sekta ya maji.

"Tunashirikiana na wadau mbalimbali katika kutathmini huduma ya utoaji wa majisafi na usafi wa mazingira, uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini," alisema.

# Viongozi wa dini waombwa kusaidia maendeleo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Alhaji Ibrahim Molel, amewataka viongozi wa madhehebu ya dini nchini kulisaidia taifa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, badala ya kuendelea kupigana vijembe.

Aidha, aliwataka viongozi hao kuwa na umoja ikiwa ni pamoja na kuvumiliana katika imani ili waweze kusonga mbele na hatimaye kuliwezesha taifa kufikia malengo yake ya uchumi wa viwanda.

Mwenyekiti huyo aliyasema hayo wakati alipokuwa akifungua kikao elekezi na namna ya kuongoza mikoa na wilaya jinsi ya kueneza maridhiano kwa kila eneo kwa viongozi kutoka madhehebu mbalimbali ya dini waliotoka mikoa ya Tanzania Bara kilichofanyika jijini Dodoma.

Alisema kuwa viongozi hao badala ya kupigana vijembe na kushindwa kusameheana watumie muda huo kwa ajili ya kujenga nchi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi yatakayofaidisha kila Mtanzania hapa nchini.

Akizungumza kwenye kikao hicho aliwataka viongozi hao pia kuwa na mioyo ya upendo na amani huku wakivumiliana ili waende kwa pamoja na kudumisha amani iliyopo.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Maridhiano Tanzania, Mchungaji Oswald Mlaya, aliwataka viongozi hao kutojihusisha na siasa badala yake wajikite katika kuiombea nchi na uchaguzi ujao wa viongozi wa serikali ya vijiji, mitaa na vitongoji, unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Naye Mwenyekiti wa jumuiya hiyo mkoani Dodoma, Shekhe Abbakari Omary, alisema kuwa chombo hicho ni muhimu katika taifa ili kuweza kuleta maridhianao na kuwa na nchi yenye mshikamano.

"Katika nchi yetu inahitaji malezi ya kiroho na hakuna mahali panapoweza kupatikana ispokuwa kwenye vyombo vyetu vya dini ikiwamo makanisa na misikiti ili tuwe pamoja tumeanzisha jumuiya itakayotuweka pamoja kwa lengo kudumisha amani," alisema.



# Sekta ya utalii ina nafasi ya kukuza uchumi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

AFRIKA Kusini na Zanzibar zina nafasi kubwa ya kuimarisha ushirikiano katika kuitumia sekta ya utalii kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi hizo.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, wakati akizungumza na Balozi wa Afrika Kusini nchini Tanzania, Thami Mseleku, aliyemtembelea ofisini kwake.

Waziri Kombo alisema hilo litawezekana kwa kuanzisha jukwaa la pamoja litakalojikita katika kuinua sekta hiyo.

Alilitaka jukwaa hilo lijumuishe wizara mbalimbali za serikali na taasisi binafsi zinazojishughulisha na utalii zikiwamo Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar, Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI).

Alimshauri balozi huyo kuangalia uwezekano wa kulitaka Shirika la Ndege la Afrika Kusini (Mango), kuongeza idadi ya safari zake za moja kwa moja Zanzibar ili kuleta wageni wengi zaidi, na hivyo kutunisha mfuko wa fedha za kigeni.

"Kwa sasa ndege ya Afrika Kusini inatua takriban kila siku hapa Zanzibar, mwaka 2018 tulipokea wageni 22,903 kutoka nchi hiyo na mwaka huu tunatumai itapanda zaidi," alisema.

Kuhusu umuhimu wa kuzitunza historia za Afrika Kusini, Zanzibar na Tanzania kwa jumla ili zifahamike na wageni na kizazi cha sasa, Waziri Kombo ameipongeza nchi hiyo, kwa uamuzi wake wa kuanzisha makumbusho jijini Dar es Salaam, yatakayokuwa na historia ya ukombozi wa nchi hiyo.

Kwa upande wake, Balozi Thami Mseleku, alisema hakuna namna yoyote inayoweza kuitenganisha nchi yake na Tanzania, ambayo chini ya Hayati Mwalimu Julius Nyerere, ilitoa mchango mkubwa katika ukombozi wa Afrika Kusini na nchi nyingine za Afrika.

Alisema haitoshi Tanzania na Afrika Kusini kujiona ni marafiki, kwa kuwa kimsingi mataifa hayo ni sawa na ndugu wa mama na baba mmoja kutokana na mambo mengi yanayowaunganisha.

Alieleza kuwa, atatumia nafasi ya uwakilishi wa nchi yake kuwashajiisha wawekezaji zaidi kuwekeza Zanzibar na Tanzania kwa jumla katika miradi ya kiuchumi ikiwamo utalii.

"Naelewa kuwa Zanzibar kuna hoteli sita za Waafrika Kusini, huu ni mwanzo mzuri na katika ziara yangu hii natarajia kukutana nao pamoja na watendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar ili tuzungumze namna ya kuimarisha zaidi sekta hii," alisema Balozi Mseleku.

# Waziri azungumzia afya ya kinywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid, ameitaka jamii kuchukua tahadhari mbalimbali kuhusu afya ya kinywa ili kuepuka athari za magonjwa.

Akizungumza na waandishi wa habari, mjini Unguja, katika Kilele cha Maadhimisho ya Afya ya Kinywa Duniani, alisema tatizo la maradhi ya kinywa ni kubwa na linatokana na jamii kulipuuzia kwa kuona ni jambo la kawaida.

Alisema jamii inapaswa kufika vituo vya afya angalau mara mbili kwa mwaka kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kinywa ili kujikinga na tatizo hilo ambalo linaweza kusababisha kuumwa kwa meno. Alisema maradhi ya kinywa na meno yanaathiri watu wengi na yanaongeza mzigo kwa taifa, ambapo kuyatibu ni gharama kubwa.

**Upo uhusiano baina ya afya ya kinywa na meno na afya kwa ujumla, maradhi ya kinywa yana uhusiano na maradhi yasiyoambukiza kama kisukari, moyo na mfumo wa upumuaji.**

Aidha, alisema serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kuchukua jitihada za kuboresha huduma za afya katika vituo kwa kuweka vifaa na wataalamu.

"Upo uhusiano baina ya afya ya kinywa na meno na afya kwa ujumla, maradhi ya kinywa yana uhusiano na maradhi yasiyoambukiza kama kisukari, moyo na mfumo wa upumuaji, " alisema.

Waziri huyo alisema changamoto zilizopo Zanzibar ina upungufu mkubwa wa madaktari wa meno, ikiwamo kutokuwa na wataalamu wa kutosha wenye kiwango cha kufanya kazi za hospitali.

Alisema wengi wa wataalamu wako katika ngazi za stashahada na hivyo kuna jukumu kubwa la kuwaendeleza kwa ajili ya mafunzo ya shahada ya kwanza na ya pili.

Hamad alisema serikali inashirikiana na wadau mbalimbali katika kuimarisha huduma za afya ya meno ikiwamo jumuiya za kiraia za ndani na nje pamoja na madaktari wa kujitolea ambao wamekuwa mchango mkubwa katika kendelea kutoa elimu na tiba juu ya maradhi ya kinywa.

Kwa upande wake, daktari bingwa wa mpangilio wa meno katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Iddi Othman Iddi, alisema mama wajawazito wapo katika hatari ya kuugua maradhi ya kinywa.

Hivyo aliwashauri wajawazito kufika katika kliniki za meno katika hatua ya mapema kwa ajili ya kinga pamoja na matibabu kwa wale ambao tayari wamegundulika na maradhi hayo.

Kauli mbiu katika siku ya afya ya kinywa ni "tunza afya ya kinywa".



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Mratibu Mkuu wa Programu ya Kujitolea ya "United Nations Volunteers" (UNV), Oliver Adam, alipofika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wizara yakunjua makucha ujenzi majengo ya serikali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haipo tayari kuona majengo ya serikali yanajengwa chini ya kiwango.

Aliyasema hayo wakati wa ziara ya kushtukiza kuangalia maendeleo ya ujenzi wa chuo cha ufundi Makunduchi na Shule ya Sekondari Kibuteni Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema Wakala wa Majengo ya Serikali Zanzibar, wapo kwa lengo la kukagua majengo mbalimbali ya serikali ambapo yatakayokua chini ya kiwango, serikali itaichukulia hatua za kisheria dhidi ya kampuni iliohusika na ujenzi wa majengo hayo.

Pembe alisema lengo la serikali katika kujenga shule pamoja na vyuo ni kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira salama na yenye utulivu.

Aidha, aliwataka makandarasi wanaosimamia ujenzi wa majengo hayo kuhakikisha wanamaliza kwa wakati na majengo wanayoyajenga yanakuwa katika viwango vilivyo bora ili kuepusha usumbufu unaoweza kutokea.

Naye Mkandarasi Omari Hashim Mfangavo wa Kampuni ya Mindset Techniques Ltd, inayosimamia ujenzi wa Chuo cha Ufundi Makunduchi, alisema tatizo la upatikanaji mchanga limechangia kuchelewa kumalizika kwa majengo hayo, ambapo ameahidi kuendelea na ujenzi ili kumaliza kwa wakati.

Kwa upande wake Mkandarasi Seif Sleyum Seif, kutoka Kampuni ya Rans .Co.Ltd anayesimamia ujenzi wa Shule ya Sekondari Kibuteni alisema shughuli hiyo inaendelea vizuri ambapo ameahidi kuyakabidhi majengo hayo mapema mwezi Juni, mwaka huu, baada ya kukamilika.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 18 March**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 19 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 20 March**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 21 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 22 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 23 March**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Be my baby
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 17 March**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 18 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 19 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum: Uongozi
21:30 Kipindi Maalum: Serengeti boys Uturuki
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 20 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kesho Leo rpt
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 21 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi Maalum rpt: Uongozi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
09:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 22 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Serengeti boys Uturuki rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Serengeti boys Uturuki rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 23 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 24 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Hard price
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Hard price 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)







## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

HABARI KIMATAIFA

# Wakenya waitaka serikali iwajibike

**NAIROBI,** Kenya

WAKATI idadi ya watu waliofariki kutokana na ukosefu wa chakula uliosababishwa na hali ya ukame katika Jimbo la Turkana nchini Kenya ikiongezeka, baadhi ya wananchi wameanza kuandika katika mitandao ya kijamii kuitaka serikali kuchukua hatua za haraka.

Hadi jana idadi ya watu waliofariki kutokana na kukosa chakula katika Jimbo la Turkana ilifikia 10.

Wananchi wa Kenya kupitia mtandao wa kijamii wa Twitter walianzisha neno #WeCannotIgnore, ambapo wamekuwa wakiandika kuitaka serikali kuchukua hatua kuwanusuru wananchi wa Jimbo la Turkana wanaotesekana kwa kukosa chakula.

Mjadala huo umeendelea huku idadi ya watu waliokufa kutokana na njaa ikiongezeka, ambapo shule zimefungwa huku wanafunzi wakiwafuata wazazi wao kwenye maeneo ya misitu kutafuta chakula.

Kwenye mitandao ya kijamii wananchi wa Kenya wamekuwa wakiandika kuwa: "Ni nini kilitokea kwa mfumo unaotoa taarifa za mapema za maafa?" "Na kwanini Wakenya wanakabiliana na njaa, katika nchi ambayo usalama wa chakula imekuwa ndio ajenda inayopewa kipaubele zaidi?"

Wengine wamekuwa wakiandika "Tangu juzi, wazee, watoto, wanawake wajawazito na watu wenye ulemavu katika Jimbo la Turkana wanaendelea kuteseka kutokana na ukosefu wa chakula na maji, lakini serikali haichukui hatua zozote."

Masomo ni miongoni mwa huduma ambazo zimekatizwa katika vijiji vingi ambavyo ukame umekithiri.

Katika Shule ya Msingi ya Lotukumo iliyoko katika Jimbo la Turkana ya Kati, wanafunzi wa darasa la nane pekee ndio wako madarasani.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Ebong'on Charles, alisema kutokana na ukosefu wa chakula, wanafunzi wengi wameamua kurudi nyumbani na kujiunga na wazazi wao kutafuta chakula.

Alisema darasa la pili ambalo kwa kawaida huwa na wanafunzi 70, kwa sasa lina wanafunzi 11 tu. Ambapo darasa la kwanza halina mwanafunzi hata mmoja kwa muda wa wiki mbili.

Mbunge Mwakilishi wa Wanawake katika Jimbo la Turkana, Joyce Emanikor, alisema wakati huu ambapo kuna serikali ya jimbo baa la njaa linapaswa kuwa historia.

"Ni aibu sana watu kufariki kutokana na njaa, Serikali ya Jimbo ina uwezo mkubwa kuhakikisha wakazi wanapata chakula cha kutosha wakati wa janga kama hili," alisema Emanikor.

Ripoti kutoka Wizara ya Majanga na Huduma kwa Umma ya Jimbo la Turkana inaeleza kuwa wakazi wengi katika Jimbo la Turkana hutegemea ufugaji ili kujikimu kimaisha na zaidi ya mifugo 30,000 imefariki na wengine 100,000 wamehamishwa nchi jirani ya Uganda.

Mwishoni mwa wiki taarifa iliyotolewa nchini humo, ilieleza kuwa watu kadhaa walikufa kutokana na matatizo yenye uhusiano na njaa katika eneo la Tiaty Jimbo la Baringo.

Pia, familia zilizoathirika zilikuwa zinaishi kwa kutegemea matunda ya msituni ambayo yanachemshwa kwa saa kadhaa ili kumaliza sumu iliyomo kwenye matunda hayo.

Wakati huo huo, Naibu Rais wa Kenya, William Ruto, alisema kuwa Kenya iko katika fursa nzuri sasa ya kukabiliana na ukame ikilinganishwa na miaka iliyopita na kupinga madai kwamba watu wamekufa kutokana na njaa.

Ruto alisema kuwa nchi inachakula cha kutosha na kuongeza kuwa hakuna haja ya kuwa na hofu. **BBC**





Wakazi wa mjini Maputo Msumbiji wakihamisha vitu vyao baada ya nyumba zao kujaa maji kutokana na mvua kubwa iliyoambatana na kimbunga kupiga nchini humo. Kulia ni nyumba nchini Msumbiji zikiwa zimeanguka baada ya kukumbwa na kimbunga Idai. **PICHA: ALLIANCE**

# Kimbunga chaua watu 1,000 Msumbiji

**MAPUTO,** Msumbiji

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, amesema idadi ya watu waliofariki kutokana na kimbunga kiitwacho Idai nchini humo imefikia 1,000.

Rais Nyusi alitoa taarifa hiyo jana baada ya kuzunguka kwa ndege katika maeneo yaliyoathirika zaidi, ambapo alisema aliona miili mingi ya watu ikielea juu ya maji.

Mbali na idadi hiyo, kimbunga hicho pia kimesababisha watu zaidi ya 100,000 kukosa sehemu za kuishi, huku mito katika maeneo yaliyoathirika ikivunja kingo zake na kuingia katika makazi ya watu.

Kimbunga hicho kilikumba eneo la kaskazini mwa Msumbiji Machi 15, mwaka huu na kusababisha uharibifu mkubwa wa nyumba, shule, hospitali na miundombinu.

Kimbunga hicho kilishuka katika Mji wa Bandari wa Beira Alhamisi wiki iliyopita, kikiwa na upepo wenye kasi ya hadi kilomita 177 kwa saa, lakini mashirika ya misaada yalifika katika eneo hilo Jumapili.

Taarifa iliyotolewa na serikali ya Msumbiji ilieleza kuwa takribani watu 600,000 wameathiriwa, huku 1,000 wakidaiwa kupotea, watu 100,000 wakihitaji msaada wa dharura mjini Beira.

Mkuu wa Operesheni wa Shirika la Save the Children nchini Msumbiji, Machel Pouw, alisema kiwango cha madhara kinazidi kuongezeka kila saa huku wasiwasi mkubwa ukiwa kwa watoto.

Umoja wa Mataifa (UN) ulieleza kuwa kila nyumba mjini Beira- ambapo ni mji wenye makazi ya watu 500,000 ziliharibiwa.

Gerald Bourke, kutoka Shirika la Chakula Duniani (FAO) alisema hakuna nyumba ambayo haikuathiriwa, hakuna umeme wala mawasiliano yoyote katika mji huo.

Alisema barabara zimejaa magogo ya nyaya za umeme. Paa za nyumba zimeng'oka, nyumba zimeanguka, raia wengi wa mji huo wamepoteza makazi yao.

Shirika la Msalaba Mwekundu limeelezea kuwa uharibifu huo ni mbaya zaidi na wa kutisha na kwamba watu wamelazimika kuokolewa wakiwa juu ya miti.

Wakati huo huo, taarifa iliyotolewa na serikali ya Zimbabwe ilieleza kuwa takribani watu 98 wamefariki, huku 217 wakiwa hawajulikani waliko mashariki na kusini.

Kati ya watu waliofariki wapo wanafunzi wawili wa Shule ya St' Charles Lwanga katika Wilaya ya Chimanimani, ambao walifariki baada ya bweni lao kuathiriwa kutokana na mawe yaliosombwa na maji hayo katika mlima.

Kadhalika, nchi ya Malawi nayo imeathiriwa vibaya ambapo mafuriko nchini humo yaliyosababishwa na mvua kabla ya kimbunga hicho kuwasili yalisababisha vifo vya watu 122.

**BBC**

## Waziri Mkuu aapa kutolitamka jina la muuaji

**WELLINGTON,** New Zealand

WAZIRI Mkuu wa New Zealand, Jacinda Ardern, amesisitiza bungeni kwamba hatolitamka jina la mtu aliyehusika na mauaji ya watu 50 baada ya kuwashambulia waumini wa dini ya Kiislamu ndani ya misikiti miwili katika mji wa Christchurch nchini New Zealand. Ardern amesema kuwa mtu huyo atakabiliwa na hatua za kisheria kikamilifu.

Alitoa tamko hilo wakati ndugu wa watu waliofariki kwenye shambulio hilo kuanza kuwasili kutoka sehemu mbalimbali kuhudhuria mazishi ambayo tayari yamecheleweshwa kwa zaidi ya saa 24 baada ya vifo kutokea.

Wakati huo huo, raia wa New Zealand wameanza kuitikia wito wa serikali unaowataka kuzirudisha silaha zao. Hata hivyo, polisi bado haijatoa idadi kamili ya silaha zilizorudishwa tangu kutangazwa kwa tangazo hilo. Waziri Mkuu Ardern alisema maelezo juu ya sheria za umiliki wa bunduki yaliyopendekezwa na serikali yake, yatatangazwa wiki ijayo. **DW**

## Tshisekedi apiga 'stop' maseneta wapya kuapishwa

**KINSHASA,**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, amesitisha zoezi la kuwaapisha maseneta wapya waliochaguliwa wiki iliyopita na kuagiza kufanyika kwa uchunguzi kuhusu madai kuwa, uchaguzi huo uligubikwa na visa vya rushwa.

Kadhalika, ameagiza uchaguzi wa magavana uliokuwa umepangwa kufanyika Machi 26, mwaka huu, kuahirishwa kwa muda usiojulikana.

Hatua hii imekuja baada ya muungano wa kisiasa wa Rais wa mstaafu Joseph Kabila, kushinda karibu viti vyote vya useneta huku muungano wa Rais Tshisekedi ukilalamikia matokeo hayo.

Rais Tshisekedi ameahidi kukutana na tume ya uchaguzi na maofisa wengine mwanzoni mwa wiki ijayo kujadiliana kuhusu suala hilo.

**RFI**

# Waziri Mkuu aagiza msako waliomwibia mkandarasi

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Mwanza, ihakikishe inafanya msako kuwakamata watu wote waliohusika na wizi wa fedha na vifaa katika eneo la ujenzi wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Misungwi mkoani humo.

Alitoa agizo hilo jana, wakati akiweka jiwe la msingi, akitumia fursa hiyo kuiagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kuimarisha ulinzi katika eneo la mradi.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo baada ya kupokea taarifa ya kuwapo kwa vitendo vya uvamizi wa mara kwa mara kwenye eneo la mradi huo unaojengwa katika Kijiji cha Nyahiti wilayani Misungwi.

"Hawa waliofanya tukio hilo la uvamizi katika eneo la mradi, si tu wanamhujumu mkandarasi na kampuni yake, bali wanahujumu jitihada za serikali ili miradi ya maendeleo kwa wananchi isikamilike, hatutakubali, wananchi tushirikiane katika kuwabaini wote waliohusika," aliagiza.

Mradi huo ni utekelezaji wa Sera ya Maji na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015/2020 inayoelekeza serikali kuwapatia huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 95 wakazi waishio mijini na waishio vijijini asilimia 85 ifikapo mwaka 2020.

Awali, Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alisema ujenzi wa mradi wa maji katika Mji wa Misungwi unatekelezwa kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Ziwa Viktoria, unaotekelezwa katika miji ya Mwanza, Musoma, Bukoba, Magu, Misungwi na Lamadi kwa gharama ya Euro milioni 104.5 (Sh. bilioni 276).

Alisema kuwa kati ya fedha hizo, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) wanachangia Euro milioni 90 (Sh. bilioni 238) ambazo ni mkopo wa masharti nafuu, na Serikali ya Tanzania inachangia Euro milioni 14.5 (Sh. bilioni 38).

Alisema mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya M/S China Civil Engineering Construction Cooperation (CCECC) ya China chini ya Mhandisi Mshauri Kampuni ya Egis ya Ufaransa na unasimamiwa na Mamlaka ya Maji jijini Mwanza (Mwauwasa). Ulianza Mei, 2017 na unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasha trekta aina ya Ursus, wakati alipokabidhi matrekta16 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 kwa wenyeviti wa baadhi ya vyama vya ushirika vya msingi mkoani Mwanza, katika hafla iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), katika Mtaa wa Posta, jijini humo jana. **PICHA: OWM**

# NEC yajipa muda uchaguzi Arumeru

**Na Salome Kitomari**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imesema inasubiri muda ufike itangaze rasmi kuwa Jimbo la Arumeru liko wazi na kuanza mchakato wa uchaguzi wa mdogo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Athuman Kihamia (pichani), alisema wamepokea barua ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, ikiwataarifu kuwa jimbo hilo liko wazi.

"Tumeshapokea barua ya spika na hivi karibuni tutatoa taarifa kwa umma juu ya hatua inayofuata kuhusiana na jimbo hilo," Kihamia alisema.

Machi 14, mwaka huu, Spika Ndugai alimwandikia barua Mwenyekiti wa NEC akieleza kuwa Joshua Nassari amepoteza sifa ya kuendelea kuwa mbunge wa jimbo hilo kutokana na kutohudhuria mikutano mitatu ya Bunge bila ruhusa na taarifa kwa spika.

Taarifa ya Bunge ilieleza kuwa Nassari hajahudhuria mfululizo wa mikutano ya Septemba 4-14, mwaka jana, Novemba 6-16, mwaka jana na wa Januari 29 - Februari 9, mwaka huu.

Ofisi hiyo ilieleza kuwa uamuzi huo umefikiwa kwa kuzingatia Ibara ya 71(c) ya Katiba ya Tanzania ya Mwaka 1977, inayosema kwamba iwapo mbunge hatahudhuria vikao vitatu mfululizo, ataondolewa katika nafasi hiyo.

Kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi, jimbo au kata inapotangazwa rasmi kuwa iko wazi, uchaguzi unatakiwa kufanyika ndani ya siku 90 kuziba nafasi husika.





## Rais ateua Posta Masta Mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli (pichani juu), amemteua Hassan Mwang'ombe kuwa Posta Masta Mkuu.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ilieleza kuwa uteuzi wa Mwang'ombe ulianza Machi 12, mwaka huu.

Kabla ya uteuzi huo, Mwang'ombe alikuwa akikaimu nafasi hiyo.

## Tanzania yazisaidia nchi

INATOKA UK 2

magonjwa ya tumbo, dawa za kutuliza maumivu, dripu, shuka, blanketi, magodoro na vyandarua.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya nchi yake, Balozi wa Msumbiji nchini, Monica Mussa, alimshukuru Rais Magufuli na Tanzania kwa msaada huo, akieleza kuwa utasaidia kunusuru maisha ya watu wengi ambao hawana chakula na wanahitaji dawa na malazi.

Balozi wa Malawi nchini, Glad Chembe Munthali, pia alimshukuru Rais Magufuli na serikali kwa msaada huo na kueleza kuwa ni wa haraka na umedhihirisha undugu, ujirani na umoja wa dhati uliopo kati ya Tanzania na Malawi.

Kaimu Balozi wa Zimbabwe nchini, Martin Chavenika, mbali na kutoa shukrani zake za dhati, alimhakikishia Rais Magufuli na serikali kwa ujumla kuwa msaada huo utawafikia walengwa.

Mkuu wa Mafunzo na Utendaji Kivita wa Kamandi ya Jeshi la Anga, Brigedia Jenerali Francis Shirima, alisema jeshi litahakikisha msaada wote uliotolewa unafika kwa nchi hizo na kukabidhiwa kwa wahusika.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**WAFANYAKAZI WA HOTELINI**, Wanatakiwa wafanyakazi wa Usafi, Wahudumu, Wapishi na Meneja. Bagamoyo mjini, wawe na vyeti na uwezo wa kuongea Kingereza. kwa Mawasiliano piga namba: 023-2440004/0657, 233970/0768 296667

**NAFASI ZA KAZI UALIMU / CERTIFICATE** au diploma / english/mathematics na science 0656490706/0655628640


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA VYETI




**Faraja Raphael Punda** anatangaza kupotelewa na cheti cha Astashahada ya Sheria chenye namba ya usajili **CL.2011/T.1585** kilichotolewa mwaka 2011 na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na Stashahada ya Sheria chenye namba ya usajili namba **8DL.2012/T.2415** kilichotolewa mwaka 2014 na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa : WMB/RB/3398/19**

115125802

## KUPOTEA KWA CHETI



**Tresphory Kisakali** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0443/0560** kilichotolewa na Baraza la Mitihani mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Meta.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

Polisi Taarifa: **NJ/RB/136/2019**

215124502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LINUS NICODEMU TAIRO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 705 CEZ SUZUKI CARRY.** Chassis namba **DD51T116975.** Engine namba **5238347.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1671/2019.**

115125702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;74/2019**

**Ombi la GLORIA LEONARD NA BETRIDA REUBEN Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LEONARD KASALA LUHEMEJA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/03/2019.

215126602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MIKONGENI**

**Usimamizi wa mirathi No;03/2019**

**Ombi la HADIJA ERNEST Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ERNEST KINGALU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/03/2019.

215126602

## KUPOTEA KWA CHETI



**Susan H. Othuman** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0274/0047** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2005 katika Shule ya Sekondari Mailimoja,

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: KJN/RB/1666/2019**

115124802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 12/03/2019.

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano itarehe **20-03-2019** kampuni ya **BADI KHALIFA BADI** itasafirisha Mzigo wake wenyevipimo vikubwa
2. Kutoka **Dar es salaam** kuelekea **MTWARA kupitia MKURANGA** gari hizo zenye namba za usajili:

   **T771 AWR/ T694 ASV**
3. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - mita | 23.00 |
| Upana | - mita | 3.5 |
| Kimo | - mita | 5.20 |

Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanziasaa 12:30 Asubuhimpakasaa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215125102

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**ARUSHA**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI SHAURI NAMBARI 07 LA MWAKA 2019**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**RICHARD BUJIJI ANTHONY..............MAREHEMU**
**NA**
**JACKLINE ANTHONY KIJIJI..................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA (KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua za usimamizi wa mirathi kwa Mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapinduzi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 29 mwezi wa April Mwaka wa 2019.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 15 Mwezi Februari Mwaka wa 2019.

25125402

## UPOTEVU WA NYARAKA

Upotevu wa Nyaraka za Ununuzi wa Viwanja Vifuatavyo:

1. WAZO CHINI TEGETA
2. BUNJU "A" BURUMAWE
3. IHEMBE WARD KARAGWE

Viwanja vyote havijapimwa zawadi nono itatolewa na Joshua JoyBoy Mungereza. Simu 0784 629947. Kwa yeyote atakayeziona atoe Taarifa Kituo cha Polisi Kilichopo karibu na wewe.

Polisi Taarifa: **KJN/RB/1653/2019**

215124602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LILIAN ISAAC MAGESA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 545 CWC TOYOTA - SALOON. Chassis namba NCP610034024. Engine namba **INZA644801.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1671/2019.**

115125502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LIDYA CELESTINE RWABIZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 197 DFZ TOYOTA PORTE.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1671/2019.**

115125602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 12/03/2019.

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe **21-03-2019** kampuni ya **MM Corp. Ltd** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa Dar es salaam kuelekea Kwala, gari hilo zenye namba za usajili:

   **T 898 APY HORSE / T 933 AFZ TRAILER**
2. Garihilolinavipimovifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - mita | 22.00 |
| Upana | - mita | 3.00 |
| Kimo | - mita | 4.80 |

3. Njia itakayotumika :Kibaha hadi Kwale kupitia Vigwaza,

Gari itasafiri muda wa mchana tu (**kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

15124402


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# ZLATAN awabwatukia wakongwe Manchester United

**NEW YORK,** Marekani

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United anayeichezea LA Galaxy ya Marekani, Zlatan Ibrahimovic, amewakosoa wachezaji wakongwe wa timu yake hiyo ya zamani.

Zlatan amedai kwamba wachezaji hao wa Man United hawakupenda Paul Pogba ahame mwaka 2012 na kurudi tena kwa mara nyingi.

"Hawachezi tena pale (Man United), lakini wapo kwenye televisheni wanalalamika muda wote kwa sababu hawapo tena katika timu," alisema Zlatan wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Kama unataka kwenda kufanya kazi katika klabu, nenda katafute hiyo kazi, Pogba alikuwa Man United wakati anachipukia, halafu alihama na baadaye akarudi tena katika utawala wa Ferguson hakuwa anapenda hilo.

"Walikuwa hata hawaongei kama Ferguson anakuwa hajawaruhusu kufungua vinywa, hivyo kwa sasa ninavyowaona wanaongea sijui kama Ferguson kawaruhusu au la.

Kundi la Class of 92 linawajumuisha wachezaji wa zamani wa Man United kama Garry Neville, Paul Scholes, Nicky Butt, Phil Neville na Ryan Giggs kwamba walikuwa hawaongeiongei chini ya Sir Alex Ferguson.

Lakini wamekuwa wakimkosoa Pogba ambaye alizua gumzo baada ya kuposti picha fulani hivi iliyokuwa inahisiwa kuwa anafurahia Jose Mourinho kufukuzwa kazi ndani ya Man United, huku Neville akiwa kinara.

# XAVI aponda timu 48 Kombe la Dunia Qatar

**DOHA,** Qatar

NGULI wa soka wa Hispania na balozi wa Kombe la Dunia 2022, Xavi (pichani chini), anaamini kuwa michuano hiyo kushirikisha timu 48 nchini Qatar 'haitakuwa vizuri'.

Mwaka 2017, Fifa ilipiga kura na kuchagua kuwapo kwa ongezeko la timu zingine 16 kwenye michuano ya Kombe la Dunia 2026, ambayo itafanyika kwa ushirikiano wa nchi tatu, Marekani, Canada na Mexico.

Lakini kwa fainali hizo za Qatar bado ratiba yake inaonyesha zitafanyika kati ya Novemba 21 na Desemba 18, mwaka 2022 ikishirikisha timu 32, ila Rais wa Fifa, Gianni Infantino, anatoa msukumo wa ongezeko la timu.

Katika mkutano wa Baraza la Fifa uliofanyika Miami juzi, Jumatatu, bodi ya baraza hilo imeamua kufuta uamuzi wa mwisho wa ongezeko la timu.

Xavi, mshindi wa Kombe la Dunia 2010, ambaye kwa sasa anacheza soka katika Ligi Kuu ya Qatar, akiitumikia Al Sadd, anaamini timu 32 ni 'zaidi ya kutosha' kwa Qatar.

"Ni nyingi sana na muda mrefu," alisema Xavi.

"Fikiria timu 48 ndani ya Qatar, haitakuwa vizuri kwa maoni yangu.

"Bado ni suala la waandaaji kuamua, ila kwa sasa Qatar kila kitu inajiandaa kwa timu 32 na itakuwa vigumu kubadili hilo kuongeza timu zaidi.

"Pia ni vizuri kwa soka kuwa na timu 32. Hiyo ni zaidi ya kutosha."



# Ndugu ampeleka Mbappe Madrid

**PARIS,** Ufaransa

NDUGU wa mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe, amesema anamuona siku moja nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, akichezea Real Madrid.

Uvumi hivi sasa umeenea kwamba, mchezaji huyo amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Real Madrid wakati wa kipindi kijacho cha majira ya joto.

Real Madrid ambayo ilianza vibaya msimu huu, hivi sasa imemrudisha kocha Zinedine Zidane, huku Rais wa klabu hiyo, Florentino Perez, akiwa tayari kuwaleta nyota kama Mbappe na Neymar.

"Kama angeenda pale Madrid akiwa na umri wa miaka 18, angefanya nini akiwa na umri wa miaka 23?" Alisema akiliambia Jarida la Le Journal du Dimanche.

"Namuona Mbappe akiichezea Real Madrid."

'Los Blancos' hao wanatarajia kufanya usajili mkubwa wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho, hasa wakati huu wakiwa wamemrejesha Zidane ikiwa ni miezi michache tangu aachane na klabu hiyo.

Pia wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili winga wa Manchester City, Raheem Sterling, pamoja na nyota wa Tottenham, Christian Eriksen.

Lakini pia wanajipanga kufanya usajili mkubwa zaidi kwa kumchukua mshindi huyo wa Kombe la Dunia, Mbappe, ambaye anatajwa kwamba thamani yake ni pauni milioni 120.



## HABARI MICHEZO



# HUDSON-ODOI
## aitwa kikosi cha England

**LONDON,** England

WINGA wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, ameitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha timu ya taifa ya wakubwa ya England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, awali alikuwa akiichezea timu ya taifa ya umri chini ya miaka 21, lakini sasa amejiunga na kikosi hicho kinachonolewa na kocha Gareth Southgate, wakati wakijiandaa na mchezo wa kufuzu michuano ya Ulaya dhidi ya Jamhuri ya Czech kwenye dimba la Wembley Ijumaa, na mchezo wa ugenini dhidi ya Montenegro Jumatatu.

Hudson-Odoi amekuwa na nafasi ndogo ya kucheza pale kwenye dimba la Stamford Bridge msimu huu na bado hajaanza mchezo wa Ligi Kuu, lakini amefunga mabao matano katika mechi 19 alizocheza kwenye mashindano yote.

"Imekuwa siku ya kufurahishwa kwa kuitwa kwa mara ya kwanza kwenye timu ya taifa," alisema Hudson-Odoi.

"Leo (jana) imekuwa siku ndefu kwa upande wangu kwa sababu nililazimika kusafiri kwenda Bristol kwanza kwa ajili ya timu ya taifa chini ya umri wa miaka 21 na baadaye nikaambiwa natakiwa pale St. George's Park kwenye kambi ya timu ya taifa ya wakubwa, lakini nimehamasika mno na kuitwa huko kuwa hapa.

"Ingawa kocha wa timu ya vijana (Aidy Boothroyd) alikuwa akinitania, nilishtuka nilipoambia kwamba nimeitwa timu ya taifa ya wakubwa, sikuamini. Lakini ilinipa hamasa kwani ndoto yangu imekuwa ya kweli."

# Barcelona yapata pigo kwa Suarez

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona ya Hispania imetangaza kwamba, mshambuliaji wake wa kimataifa wa Uruguay, Luis Suarez, watamkosa katika michezo kadhaa baada ya kupata majeraha katika mchezo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, dhidi ya Real Betis Jumamosi.

Barcelona walimtoa Suarez uwanjani dakika za mwisho wakati wa mchezo dhidi ya Real Betis uliomalizika kwa FC Barcelona kupata ushindi wa mabao 4-1, Jumapili hiyo usiku Suarez alifunga bao lake la 18 la La Liga msimu huu.

Kutokana na majeraha aliyoyapata ni wazi Barcelona wametangaza kuwa atakuwa nje ya uwanja kwa siku kati ya 10 hadi 15.

Hivyo Suarez pamoja na kwamba alikuwa kaitwa katika kikosi chake cha Timu ya Taifa ya Uruguay kutokana na kuumia kifundo cha mguu ameondolewa kikosini.





# Simeone amponza Ronaldo

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Cristiano Ronaldo, amechukuliwa hatua za kinidhamu na Uefa baada ya kushangilia 'visivyo' ushindi wa klabu yake dhidi ya Atletico Madrid katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo walifuzu hatua ya robo wiki iliyopita.

Nyota huyo raia wa Ureno mwenye umri wa miaka 34, alionekana kumkejeli kocha wa Atletico, Diego Simeone (picha ndogo), huku akiwageukia mashabiki wa klabu hiyo na kujishika sehemu zake za siri.

Ronaldo alifanya kosa hilo wakati akishangilia 'hat-trick' yake iliyoifungia Juventus wakati ikipindua matokeo na kuifunga Atletico mabao 3-0.




Uefa itatoa uamuzi wa kesi hiyo Machi 21, mwaka huu. Ronaldo aliifungia Juventus mabao matatu, hat-trick' wakati wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Atletico Madrid, baada ya mchezo wa kwanza kufungwa 2-0.

Juventus walifungwa kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano ya timu 16-bora.

Na sasa Uefa imemfungulia mashtaka na ataanza kuchunguzwa kutokana na staili hiyo ya ushangiliaji.

Ronaldo anaweza kukumbana na adhabu kutoka Uefa, ambapo itakuwa pigo kwa Juventus ambao wanaweza kumkosa kwenye mchezo wa robo fainali dhidi ya Ajax.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MOURINHO: MBAPPE ANA THAMANI KULIKO MESSI, CR7

**PARIS,** Ufaransa

JOSE Mourinho anaamini umri na uwezo wa "kushangaza" wa mshambuliaji Kylian Mbappe, unamfanya kuwa na thamani zaidi hata ya Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain, Mbappe ametwaa Kombe la Dunia, ubingwa wa Ligue 1 mara mbili, amefunga mabao 55 katika Ligi Kuu na ameshika nafasi ya nne kwenye tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] vyote hivyo ikivipata kabla ya kutimiza miaka 21.

Na ni ujana wake ambao kocha huyo wa zamani wa Manchester United, Mourinho aliona kama tofauti kubwa wakati akilinganisha thamani yake katika soko la uhamisho kwa nahodha wa Barcelona Messi, 31, na nyota wa Juventus, Ronaldo, mwenye umri wa miaka 34.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Inter na Real Madrid anadhani nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa anaweza kuhitaji ada kubwa kuliko mchezaji ghali zaidi duniani kwa sasa wanayecheza naye hapo PSG, Neymar.

"Kwa mchezaji kama Mbappe, wakati unapozungumza kuhusu mustakabali wa baadaye, huhitaji kusema atakavyokuwa muda wa miaka mitano ijayo, kwa kipindi cha miaka 10," Mourinho aliiambia beIN Sports.

"Kwa kuzingatia tu sasa. Yeye ni wa ajabu kabisa.

"Nadhani ukigeukia umri wake [na kuzingatia] umri wa Cristiano, wa Messi, [wote] ni zaidi ya miaka 30, Neymar ana miaka 27... wakati unakwenda sokoni kiwango na umri pia ni kigezo, nadhani ni mchezaji mwenye thamani zaidi duniani.

"Katika uhamisho wa kufikiri, yeye ni mchezaji ghali sana katika soka kwa sasa.

"Kwa upande wa ubora, [anao] wakushangaza. Neno moja linatosha. Inamaana kila kitu."

Mbappe alifunga bao la kwanza wakati PSG ikishinda 3-1 dhidi ya Marseille kabla ya kujiunga na kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa kujiandaa na mechi yao ya ufunguzi kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Moldova na Iceland.

Akizungumza katika mkutano na wanahabari Jumatatu, Kocha wa Ufaransa 'Les Bleus', Didier Deschamps, alikubali ukomavu wa mshambiliaji huyo kijana na uwezo wa kumudu kuchukua tahadhari ya karibu kutoka kwa wachezaji wa upinzani.

"Ana uwezo huo ambao labda anaweza kukabiliana nao katika upinzani mgumu uwanjani. Yupo tayari kukabiliana na kitu cha aina hiyo," Deschamps alisema.

## KWA UFUPI

### ZIDANE AMTAKA MANE REAL
KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anataka kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Msenegal, Sadio Mane, 26, katika dirisha la majira ya joto. **(France Football)**

### MANOLAS ANUKIA KUTUA UNITED
Manchester United inaweza kumsajili beki wa Roma na Ugiriki, Kostas Manolas, 27, kwa ada inayozungumzia majira haya ya joto. Katika mkataba wa Manolas kuna kipengele kinachomruhusu kuuvunja kwa pauni milioni 30.8. **(Calciomercato, via Manchester Evening News)**

### BECKHAM AMTAKA MESSI, RONALDO
DAVID Beckham ana ndoto za kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi, 31, ama wa Juventus, Cristiano Ronaldo, 34, kwenda kuitumikia klabu yake ya Inter Miami kwenye Ligi Kuu ya Marekani [Major League soccer]. **(Fox Sports)**

### HAZARD AWEKEWA NGUMU CHELSEA
CHELSEA imekataa ofa ya awali kutoka kwa miamba ya La Liga, Real Madrid kwa kiungo mshambuliaji wao, Mbelgiji Eden Hazard, 28. **(Daily Record)**

### ARSENAL KUMREJESHA SUAREZ BARCA
ARSENAL itamrejesha kiungo Mhispania Denis Suarez, 25, Barcelona majira haya joto kufuatia kushindwa kumvutia kocha Unai Emery. **(Sun)**

### VARANE AJIPANGA MADRID
BEKI wa Real Madrid, Raphael Varane, 25, anazingatia mustakabali wake wa baadaye kwa miamba hao wa Hispania, licha ya kurejea Mfaransa mwenzake, Zinedine Zidane kuinoa klabu hiyo. **(L'Equipe, via Mirror)**

### BENITEZ KUFUNGWA NEWCASTLE
KOCHA wa Newcastle United, Rafael Benitez, amepokea kwa maandishi ofa ya kuongeza mkataba baada ya msimu huu. **(Chronicle)**

### JUVE, REAL VITANI KWA ERIKSEN
JUVENTUS ipo tayari kutoa upinzani kwa Real Madrid katika vita ya kumsajili kiungo mshambuliaji wa Tottenham na Denmark, Christian Eriksen, 27. **(Calciomercato, via Mail)**

### SANCHEZ AWINDWA JUVENTUS
MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez, 30, anaweza kujiandaa kutua Juventus majira ya joto kama raia huyo wa Chile amejiandaa kupunguza mshahara wake wa pauni 500,000 kwa wiki. **(Calciomercato, via Express)**

### PEREIRA KUTOLEWA KWA MKOPO
MANCHESTER United inataka kumruhusu kiungo Mbrazil Andreas Pereira, 23, kuondoka kwa mkopo kwa msimu mzima ujao ili kwenda kupata uzoefu. **(Sun)**

### ARSENAL YAMPIGIA HESABU MARTINS
ARSENAL inapanga kutoa ofa majira ya joto kwa mshambuliaji wa kimataifa wa Ureno, Gelson Martins. Kwa sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anacheza kwa mkopo Monaco akitokea Atletico Madrid. **(A Bola, via Talksport)**

### LIVER, NEWCASTLE ZAMTAKA BRAHIMI
LIVERPOOL na Newcastle zote zinavutiwa kumsajili winga wa kulia wa Middlesbrough, Bilal Brahimi, 18, ingawa miamba ya Ligue 1, Rennes pia inamhitaji Mfaransa huyo. **(Teamtalk)**

# MINZIRO APEWA MIKOBA YA POPADIC SINGIDA UTD

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Klabu ya Singida United umetangaza kumsimamisha kazi kocha wa timu hiyo, Dragan Popadic na nafasi yake kuchukuliwa na Fred Felix Minziro.

Mkurugenzi wa timu hiyo, Festo Sanga, aliliambia Nipashe jana kwamba kumekuwa na msuguano kati ya Popadic na wachezaji wa timu hiyo hali iliyosababisha uongozi wa Singida kuamua kumsimamisha kocha huyo.

"Kwa sasa timu tumemkabidhi Minziro 'Baba Isaya', ambaye ataiongoza timu kwa kipindi hiki kilichobaki," alisema Sanga.

Inaelezwa wachezaji wa timu hiyo hawafurahishwi na uongozi wa kocha Popadic ambaye amekuwa mkali na asiyetaka ushauri wa mtu.

Singida United imekuwa kwenye hali mbaya ndani ya uwanja tangu kuondoka kwa kocha Hans van der Pluijm na baadhi ya nyota wake ambao pamoja na Pluijm walijiunga na Azam FC.

Hata hivyo, Pluijm hakukaa na Azam baada ya uongozi wa klabu hiyo kuamua kumtimua pamoja na msaidizi wake Juma Mwambusi kutokana na matokeo mabaya.

## TUFURAHI...



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (kushoto), Kylian Mbappe na kiungo Tanguy Ndombele (kulia) wakiwa katika utani wakati wa mazoezi ya kujiandaa na kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Moldova Ijumaa na baadaye Iceland. **PICHA: DAILY MAIL**

# Samatta atangaza vita kuipeleka Stars Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Mbwana Samatta, amesema Tanzania ina nafasi ya kucheza fainali za Afrika kama kila mmoja atapambana ipasavyo kwenye mchezo dhidi ya Uganda Jumapili.

Stars itashuka Uwanja wa Taifa Jumapili kuivaa Uganda ikiwa na kumbukumbu ya kulazimisha sare ugenini walipokutana na timu hiyo inayoongoza msimamo wa Kundi L ambayo pia tayari ina tiketi mkononi ya kushiriki Afcon Juni mwaka huu nchini Misri.

Samatta ambaye amewasili nchini juzi akitokea Ubelgiji kwa ajili ya mchezo huo, alisema kama wachezaji watapambana uwanjani kuhakikisha wanapata ushindi kwenye uwanja wa nyumbani.

"Hii ni mechi muhimu sana kwetu..., kila mchezaji anafahamu umuhimu wa mchezo huu..., mimi naamini kama tutapambana dakika zote tunaweza kufanya vizuri," alisema Samatta.

Aidha, aliwataka mashabiki na Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwasapoti kwenye mchezo huo muhimu.

Katika kundi lao, Stars ina pointi tano sawa na Lesotho, huku Cape Verde ikiburuza mkia kwa alama zake nne.

Uganda tayari imefuzu kushiriki fainali hizo na kuzifanya Tanzania, Cape Verde na Lesotho kuwania nafasi moja kuungana nayo.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.Simba | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4.Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.Ruvu Shooting | 30 | 8 | 11 | 11 | 27 | 35 | 35 |
| 17.Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Wadau wa filamu washushiwa fursa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya MultiChoice Tanzania imetangaza fursa ya kipekee kwa wadau wa tasnia ya filamu Tanzania na barani Afrika kwa ujumla ijulikanayo kama 'MultiChoice Talent Factory Portal' iliyodhamiria kuleta mapinduzi ya hali ya juu katika uandaaji wa filamu zenye viwango vya kimataifa kutoka barani Afrika.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa programu hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka MultiChoice Tanzania, Johnson Mshana, alieleza kuwa programu hiyo ni mwendelezo wa programu maalum iliyodhamiria kuleta mabadiliko katika tasnia ya filamu barani Afrika.

"MultiChoice Talent Factory ambayo ni programu mama ilizinduliwa rasmi mapema Mei mwaka jana na imedhamiria kuleta mabadiliko chanya kwenye tasnia ya filamu hapa nyumbani Tanzania na Afrika kwa ujumla.

"Tulianza kwa kupeleka vijana wanne katika kambi maalum ya mafunzo ya uandaaji filamu kwenye akademia maalum kule Nairobi nchini Kenya, kisha mafunzo maalum kwa magwiji wa sauti yaliyofanyika Januari mwaka huu na hatimaye leo hii tumekuja tena na jukwaa maalum lenye dhamira ile ile ya kuleta mapinduzi katika tasnia ya filamu barani Afrika," alisema Mshana.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Joyce Fisoo, aliishukuru sana Kampuni ya MultiChoice kwa kuwa imekuwa mstari wa mbele katika kuleta mapinduzi kwenye tasnia ya filamu hapa nyumbani.

"Binafsi nilishuhudia uzinduzi wa programu ya MultiChoice Talent Factory mapema mwaka jana kule mjini Dodoma na leo hii tunazindua tena sehemu nyingine ya programu hiyo hiyo. Hakika ni fursa ya kipekee na ninapenda kuchukua nafasi hii kuwahamasisha wadau wote waliopo katika tasnia hiyo kuitumia nafasi hii ipasavyo ili kuweza kujifunza, kubadilishana ujuzi na hatimaye kupata kazi zenye maudhui ya hali ya juu kutoka hapa hapa Afrika," alisema Fisoo.

Naye Ofisa Uhusiano wa MultiChoice Tanzania, Grace Mgaya, alimalizia kwa kueleza kuwa ukurasa huu ni wa wazi kwa watu wote hususan wadau wa filamu waliopo hapa nyumbani na Afrika kwa ujumla.

"Tunaamini kwa kupitia programu hii tutaweza kuwafikia wadau wengi zaidi na tunatarajia kazi zenye ubora wa hali ya juu kutoka barani Afrika kwa siku zijazo kutokana na matokeo chanya yatakayoletwa na programu hii ya MultiChoice Talent Factory," alisema Grace.

# Michezo

Jumatano Machi 20, 2019

Nipashe


## Mourinho: Mbappe ana thamani kuliko Messi, CR7




HABARI UK. 30

## Yanga yaitafutia pumzi Alliance

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya mapumziko ya siku tatu, kikosi cha Yanga leo kinaanza mazoezi kujiwinda na mchezo wao wa Kombe la Shirikisho (FA), dhidi ya Alliance ya Mwanza.

Yanga baada ya mchezo wao dhidi ya Lipuli, wachezaji walipewa mapumziko mafupi na leo wanarejea kwenye mazoezi chini ya kocha msaidizi, Noel Mwandila.

**Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema kuwa Yanga inatarajia kwenda Mwanza Machi 28, mwaka huu tayari kwa mchezo huo.**

"Kesho (leo), tunaanza mazoezi chini ya kocha Mwandila kwa ajili ya mchezo wetu wa Kombe la FA," alisema Saleh.

Aidha, alisema kocha mkuu wa timu hiyo, Mwinyi Zahera anatarajia kurejea nchini mara baada ya mchezo wa timu ya Taifa ya Congo dhidi ya Gabon utakaochezwa Jumapili ijayo.

"Kwenye mchezo wa Mwanza atakuwapo, lakini kwa sasa benchi la ufundi lipo chini ya kocha msaidizi," alisema.

Mchezo huo wa Kombe la FA utachezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza ambapo mshindi atasonga mbele hatua inayofuata.

Bingwa wa michuano hiyo ya FA ataiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**AMEREJEA...**



Lionel Messi (katikati) akiwa mazoezini jana na wechezaji wenzake wa Argentina kujiandaa na mechi ya kirafiki dhidi ya Venezuela keshokutwa, kabla ya kuvaana na Morocco Jumanne. Hiyo ni mara ya kwanza kwa Messi kujiunga na kikosi hicho tangu michuano ya Kombe la Dunia. **PICHA: MTANDAO**

# CHAMA AWATULIZA MASHABIKI SIMBA

## Ni wakati droo ya robo fainali Caf ikipangwa leo, asema hata wakija Esperance...

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Simba, Clatous Chama, amesema hawana hofu na timu yoyote watakayopangwa nayo kucheza hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati droo ya hatua hiyo itakapochezeshwa leo jijini Cairo, Misri.

Akizungumza na Nipashe jana, Chama, alisema kwa hatua waliyofikia kwa sasa ni vita na wapo tayari kukabiliana na timu yoyote.

"Tutajipanga, kufika hatua hii tumefanya kazi kubwa na bado tuna kazi mbele yetu, hatujui tutacheza na nani, lakini tupo tayari kukabiliana na timu yotote," alisema Chama.

Nyota huyo ambaye alifunga bao la ushindi kwenye mchezo dhidi ya AS Vita walioibuka na ushindi wa mabao 2-1 na kutinga robo fainali, alisema kila timu iliyotinga hatua hiyo ni bora.

"Kila mchezo una mipango yake, baada ya droo kocha atapanga nini cha kufanya kuhakikisha tunaingia hatua inayofuata," alisema Chama.

Mbali na Simba, timu nyingine zilizotinga hatua hiyo ni

Esperance ya Tunisia, Wydad Casablanca ya Morocco, TP Mazembe ya Congo, Mamelod ya Afrika Kusini, Horoya ya Guinea, Asec Mimosa ya Ivory Coast na Al Ahly ya Misri.

Hata hivyo, uwezekano mkubwa upo kwa Simba kukutana na Esperance, Wydad Casablanca ama TP Mazembe.

Simba imefika robo fainali baada ya kuanzia hatua ya awali ya michuano hiyo kwa kuichapa Mbambane Swallow ya Swaziland kwa sasa Eswatini, kwa mabao 4-1 Uwanja wa Taifa kabla ya kwenda kwao na kuifumua 4-0, na kusonga mbele kwa jumla ya tofauti ya mabao 8-1.

Katika mechi ya mtoano, kuwania kutinga hatua ya makundi, ilikubali kipigo cha mabao 2-1 ugenini Zambia kutoka kwa Nkana FC kabla ya kushinda 3-1 katika Uwanja wa Taifa jijini Da es Salaam, hivyo kusonga mbele kwa jumla ya tofauti ya mabao 5-2.

Kwenye hatua ya makundi, ilianza kwa kushinda nyumbani mabao 3-0 dhidi ya JS Saoura na kisha ikachapwa 5-0 ugenini DR Congo dhidi ya AS Vita na kipigo tena kama hicho kutoka kwa Al Ahly ikiwa nchini Misri.

Hata hivyo, Simba iliendeleza moto wake ikiwa nyumbani kwa kuichapa Al Ahly bao 1-0 na kisha kwenda ugenini Algeria ambapo ilikubali kulala kwa mabao 2-0 dhidi ya JS Saoura kabla ya kurudi Uwanja wa Taifa kumalizia hasira zake kwa kuifumua AS Vita mabao 2-1.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >